# ILANI YA UCHAGUZI YA ASASI ZA KIRAIA YA MWAKA 2024/2029

*"Tanzania Tuitakayo"*



SEPTEMBA 2024

# ILANI YA UCHAGUZI YA ASASI ZA KIRAIA YA MWAKA 2024/2029

SEPTEMBA 2024

Funded by
the European Union

# YALIYOMO


**DIBAJI** vi

**SHUKRANI** vii

**SURA YA KWANZA** 1

**KUHUSU ILANI YA AZAKI** 1

1.0 KUHUSU SURA HII 1
1.1 Chimbuko la Ilani ya AZAKI 1
1.2 Malengo ya Ilani ya AZAKI ya Mwaka 2024-2029 2
1.3 Muundo wa Ilani Hii 2
1.4 Utaratibu wa Kuandaa Ilani ya AZAKI ya Mwaka 2024/2029 3
1.5 Jitihada zilizofikiwa katika Ilani AZAKI ya mwaka 2019-2024 4
1.6 Ni kiongozi yupi anaweza kutupeleka katika Tanzania tuitakayo 6
1.7 Vipaumbele vikuu vya AZAKI kwa mwaka 2024-2029 7
1.7.1 Katiba Mpya 7
1.7.2 Sera ya Uchumi Jumuishi na Maendeleo Endelevu 7
1.7.3 Usimamizi wa Rasilimali za Umma na kutokomeza Rushwa 8
1.7.4 Haki za Binadamu, Utawala wa Sheria na Mgawanyo wa Madaraka 8
1.7.5 Ulinzi wa Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi 8
1.8 Dhana na Umuhimu wa Uchaguzi Huru 8
1.9.Tunu za Taifa 9

**SURA YA PILI** 11

**UHURU, HAKI ZA KIRAIA NA ZA KISIASA** 11

2.1 KUHUSU SURA HII 11
2.2 UTEKELEZAJI WA HOJA ZA ILANI 2019-2024 11
2.2.1 Uhuru wa Kujieleza 11
2.2.2.Uhuru wa Kukusanyika na Kujumuika 13
2.2.3 Ushiriki wa Wananchi katika Uongozi na Maendeleo 14
2.2.4 Uchaguzi Huru na Haki 15
2.3 TAMKO LA ILANI 16
2.3.1 Uhuru wa Kujieleza 16

2.3.2 Uhuru wa Kukusanyika na Kujumuika 17
2.3.3 Matukio ya Kuteswa na Kutekwa 17
2.3.4 Ushiriki wa Wananchi Katika Uongozi na Maendeleo 18
2.3.4 Uchaguzi Huru na wa Haki 18

**SURA YA TATU** **20**

**UKUU WA KATIBA, UTAWALA WA SHERIA, NA UTAWALA BORA** **20**

3.0 KUHUSU SURA HII 20
3.1 UTEKELEZAJI WA ILANI YA AZAKI 2019/24 21
3.1.1 Utawala Bora na Mgawanyo wa Madaraka 21
3.1.2 Ukatiba na Katiba Mpya 22
3.1.3 Utawala wa Sheria 23
3.2 TAMKO LA ILANI 24
3.2.1 Utawala wa Sheria 24
3.2.2 Ukatiba na Katiba Mpya 25
3.2.3 Utawala Bora na Mgawanyiko wa Madaraka 26

**SURA YA NNE** **28**

**UCHUMI JUMUISHI NA MAENDELEO ENDELEVU** **28**

4.0 KUHUSU SURA HII 28
4.1 UTEKELEZAJI WA ILANI YA AZAKI 2019-2024 28
4.1.1 Uchumi Jumuishi 28
4.1.2. Maendeleo Endelevu 31
4.1.3 Mazingira na Mabadiliko ya Tabia nchi 33
4.2 TAMKO LA ILANI 37
4.2.1.Tamko kuhusu Maendeleo Endelevu 38
4.2.2.Tamko Kuhusu Uchumi Jumuishi 38
4.2.3 Tamko kuhusu Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi 40

**SURA YA TANO** **42**

**RUSHWA, UWAJIBIKAJI NA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UMMA** **42**

5.0 KUHUSU SURA HII 42
5.1 UTEKELEZAJI WA HOJA ZA ILANI YA AZAKI YA MWAKA 2019-2024 43
5.1.1 Rushwa na Uwajibikaji 43
5.1.2 Uwajibikaji kwa Jamii (Corporate Social Responsibility) - Tanzania 45
5.1.3 Usimamizi wa Rasilimali za Umma 46
5.4 MATAMKO KUHUSU RUSHWA, UWAJIBIKAJI NA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UMMA 49

**SURA YA SITA** 52

**USAWA WA KIJINSIA NA MAKUNDI MAALUM** 52

6.0 KUHUSU SURA HII 52
6.1 UTEKELEZAJI WA ILANI YA AZAKI 2019-2024. 52
6.1.1 Usawa Wa Kijinsia 52
6.1.2 Ulinzi na Ustawi wa Wazee 53
6.1.3 Haki, Ulinzi, Usalama na Ustawi wa Mtoto 54
6.1.4 Haki, Ustawi na Ujumuishwaji wa Vijana 55
6.1.5 Haki, Ulinzi na Ustawi wa Watu wenye Ulemavu 56
6.2 MATAMKO YA ILANI 58
6.2.1 Tamko Kuhusu Usawa wa Kijinsia 58
6.2.3 Tamko Kuhusu Watoto. 59
6.2.2 Ulinzi, Usalama na Ustawi wa Wazee 60
6.2.4 Tamko Kuhusu Vijana 60
6.2.6 Haki na Ujumuishwaji wa Watu wenye Ulevamvu 61

**SURA YA SABA** 63

**KUIMARISHA UPATIKANAJI WA HUDUMA MUHIMU ZA KIJAMII KWA WANANCHI WOTE** 63

7.0 KUHUSU SURA HII 63
7.1 SEKTA YA AFYA 63
7.2. UPATIKANAJI WA HUDUMA YA MAJI, USAFI NA MAZINGIRA 66
7.3. ELIMU 67
7.4. UHIFADHI WA JAMII 69
7.5 MATAMKO 70
7.5.1 Tamko la Ilani kuhusu huduma za Afya 70
7.5.2 Tamko kuhusu upatikaji wa maji safi, usafi na mazingira 71
7.5.3 Matamko kuhusu Elimu 72
7.5.4 Matamko Kuhusu Hifadhi za Jamii 74

**SURA YA NANE** 76

**AMANI, USALAMA, UMOJA NA MSHIKAMANO WA TAIFA** 76

8.0 KUHUSU SURA HII 76
8.1 HALI YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA AZAKI YA MWAKA 2019-2024 77
8.1.1 Amani na Usalama 77
8.1.2 Umoja na Mshikamano 78

8.2 TAMKO LA ILANI KUHUSU AMANI, USALAMA, UMOJA NA MSHIKAMANO 80
8.2.1 Amani na Usalama 80
8.2.2 Umoja na Mshikamano 81

**SURA YA TISA** **83**
**DIPLOMASIA NA MAHUSIANO YA KIMATAIFA** **83**

9.0 KUHUSU SURA HII 83
9.1 UTEKELEZAJI WA ILANI YA AZAKI YA MWAKA 2019-2024 83
9.1.1 Uwakilishi wa Nchi Katika Mikutano ya Kikanda 83
9.1.2 Ushiriki wa Tanzania Katika Michakato ya Kimataifa 85
9.1.3 Diplomasia ya Uchumi 87
9.2 TAMKO LA ILANI 89
9.2.1 Tamko Kuhusu Uwakilishi wa Nchi Katika Michakato na Mikutano ya Kimataifa na Kikanda 89
9.2.2 Tamko Kuhusu Diplomasia ya Uchumi 90

**SURA YA KUMI** **91**
**WITO KWA MAKUNDI MBALIMBALI** **91**

10.1 KUHUSU SURA HII 91
10.2 Wito kwa kwa makundi mbalimbali 91
10.2.1 Wananchi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Tanzania Bara. 91
10.2.2 Kwa Vyama vya Siasa 92
10.2.3 Kwa Wagombea 93
10.2.4 Vyombo vya Kusimamia Uchaguzi INEC, ZEC na TAMISEMI 93
10.2.5 Vikosi vya Majeshi na Usalama 94
10.2.6 Washirika wa Kimataifa 95
10.2.7 Watumishi wa Umma 95
12.2.8 Vyombo vya habari 95
10.2.9 Viongozi wa Dini 96
10.2.10 Msajili wa Vyama vya Siasa 96

# DIBAJI

Sisi ni Asasi za Kiraia (AZAKI) za nchini Tanzania (Bara na Zanzibar) zilizoundwa na kutambulika kisheria na zinazofanya kazi katika masuala mbalimbali ya kisheria, kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na haki za binadamu. Kwa umoja wetu tunasimamia na kuhimiza utawala wa sheria na haki za binadamu na masuala yote ya kimaendeleo ili kuhakikisha maisha ya mtanzania yanakuwa bora katika nyanja zote. Katika masuala binafsi, kila asasi au kwa makundi yao wanayo ilani inayogusia masuala yao kitasisi, lakini kwa pamoja masuala yote yenye masilahi ya pamoja kama wananchi kwa maendeleo ya Taifa tumeyawasilisha kupitia ilani hii ya uchaguzi ya pamoja.

Kwa ujumla sisi ni watanzania, wazalendo, wapenda maendeleo endelevu, watetezi wa haki za binadamu na wasimamizi wa utawala bora na utawala wa sheria.Uchaguzi ni sehemu kuu ya michakato ya kidemokrasia duniani kote. Sisi asasi za kiraia tukiwa ni watetezi na wasimamizi wa demokrasia, utawala bora na haki za binadamu, hatumuungi mkono mgombea yeyote wala chama chochote cha kisiasa kinachotafuta kuingia madarakani wala hatulengi kuchukua dola.

Kwa ujumla wake, uchaguzi huundwa na wadau wengi lakini makundi makuu mawili ni wapiga kura na wapigiwa kura. Ili wapiga kura waweze kuchagua kiongozi atakayeweza kusimamia maendeleo ya nchi na kuhakikisha amani ya nchi inazidi kudumu hawana budi kujua vigezo vya kiongozi bora na mahitaji ya msingi ya Taifa. Ilani hii inabeba hoja za wananchi ambazo tungependa wanasiasa waziweke katika ilani zao za uchaguzi.

AZAKI tumekuwa wadau wakubwa katika kusukuma gurudumu la maendeleo hapa nchini pamoja na kuwa wasimamizi na waangalizi wazuri wa michakato ya kidemokrasia na uchaguzi hapa nchini. AZAKI tunaamini ili kuweza kufikia Tanzania tuikakayo, viongozi wanaochaguliwa katika michakato ya uchaguzi wana nafasi kubwa sana katika hili. Lakini viongozi wataweza kutufikisha katika safari hii endapo wataweka ajenda za msingi za wananchi katika ilani zao na badaye kuzitekeleza watakapoingia madarakani.


AZAKI TANZANIA

# SHUKRANI

Kwa namna ya kipekee, tunatoa shukrani zetu kwa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) kwa Kushirikiana na Foundation for Civil Society (FCS) kwa uratibu wa shughuli zote za maandalizi ya ilani hii katika hatua zake zote. Tunawashukuru wawakilishi kutoka AZAKI zaidi ya 300, wananchi wa kawaida, wanaharakati, wataalamu, na viongozi wa jamii kutoka pembe mbalimbali za Tanzania kwa kutoa maoni yao. Maoni haya yamesaidia kuchakata vipaumbele vya watanzania katika ilani hii.

Shukrani zetu za dhati pia ziwaendee wajumbe wa timu maalum ya wana AZAKI kutoka asasi zifuatazo: THRDC, Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Kituo Cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), HakiElimu, Tanganyika Law Society (TLS), Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania (CCBRT); Tanzania Gender Networking programme (TGNP); Nguruka Development Agency (NDA); Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA); Jumuiya ya Mashirika yasiyokua ya Kiserikali Zanzibar (ANGOZA); na Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) kwa kushirikiana katika uandishi wa ilani hii. Tunawashukuru pia wote waliojitoa kupitia na kuhariri kazi hii,

# “Tanzania Tuitakayo”



SURA YA
**KWANZA**

# KUHUSU ILANI YA AZAKI

## 1.0 KUHUSU SURA HII

Sura hii inaelezea kwa undani kuhusu ilani hii ya AZAKI kwa kufafanua tunu za Taifa, nia , chimbuko na malengo ya AZAKI kuandaa ilani za uchaguzi wakati wa kuelekea chaguzi. Sura hii pia inafafanua aina ya viongozi ambao watanzania wakiwachagua watakuwa na mchango mkubwa katika kubeba ajenda za wananchi katika uongozi wao. Pia sura hii inaelezea umuhimu wa wananchi kushiriki uchaguzi na vigezo vya uchaguzi bora wenye kuzingatia usawa na uhuru.

## 1.1 Chimbuko la Ilani ya AZAKI

Asasi za kiraia ni wadau wakubwa wa masuala ya kijamii kama vile maendeleo , ustawi wa jamii, haki za binadamu , utawala bora pamoja na demokrasia. Kwa kuzingatia umuhimu na majukumu ya AZAKI kwa jamii , mwaka 2014 kwa mara ya kwanza AZAKI ziliamua kuwa na utaratibu wa kuandaa mwongozo wa pamoja kuhusu mambo ya msingi kuelekea kwenye chaguzi. Ilani ya kwanza iliandaliwa mwaka 2014/15 na ilani ya pili mwaka 2019/20. Ilani hii ni ilani ya tatu ya AZAKI kuelekea katika chaguzi za 2024/25.

Ilani ya AZAKI toka mwaka 2015 imekuwa ikisimamia ajenda ya "**Tanzania Tuitakayo"** kwa kuweka vipaumbele vya msingi vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi. Ilani hii imekuwa ikiandaliwa na wana AZAKI wenyewe na badaye kushirikisha wadau wote muhimu kwa ajili ya utekelezaji kama vile vyama vya siasa, wananchi, viongozi wa taasisi zinazosimamia uchaguzi na wadau wa maendeleo. Msingi mkubwa wa uwepo wa Ilani ya AZAKI imekuwa ni kutoa nafasi ya wana AZAKI na watanzania kuandaa yale mambo ya msingi ambayo yanapaswa kuzingatiwa na vyama siasa wakati wanapoandaa ilani zao lakini pia kutoa mwongozo wa mambo ya msingi ya kuzingatiwa katika mchakato wa usimamizi wa uchaguzi.

AZAKI ni tasisi huru zilizosajiliwa hapa nchini na zenye majukumu ya kushiriki katika michakato yote inayogusa maisha ya watanzania kwa njia mbalimbali ikiwepo kushauri , kukemea na kusaidia pale inapobidi. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania , watanzania kupitia taasisi zao wanawajibu na haki ya kushiriki katika michakato mbalimbali ya kitaifa kwa kuwa Tanzania ni nchi ya kidemokrasia na uongozi unatokana na watu. Serikali itawajibika kwa watu na watu watashiriki katika mambo ya umma kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi.

### 1.2 Malengo ya Ilani ya AZAKI ya Mwaka 2024-2029

Ilani hii imeandaliwa kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 pamoja na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Pamoja na mambo mengine ilani hii imelenga mambo ya msingi yafuatayo yatakayo pelekea kuwa na Tanzania tuitakayo;

a) Kutoa mwongozo kwa viongozi wa kisiasa na vyama vya kisiasa vitakavyoshiriki chaguzi za serikali za mitaa pamoja uchaguzi mkuu kuhusu hoja ambazo AZAKI na wananchi kwa ujumla wanapenda ziwepo katika ilani zao cha uchaguzi.

b) Kutoa mwongozo kwa wananchi kuhusu umuhimu wa uchaguzi, aina bora ya uchaguzi pamoja na sifa za viongozi bora watakaotuletea Tanzania tuitakayo.

c) Kutoa mwongozo kwa wananchi na vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2024/25 kuzingatia Katiba, sheria za nchi na haki za binadamu katika mchakato mzima wa uchaguzi mkuu. Ni dira na mwongozo kwa wananchi, wagombea, vyama vya siasa, serikali na wadau wengine kuzingatia mchakato wa uchaguzi ulio huru, wa haki na amani.

d) Pia ni mwongozo kwa wanaoomba ridhaa ya kuongoza kwa kuzingatia masuala ya msingi ya kijamii, kiuchumi, haki za binadamu, kisiasa na kiutamaduni yenye tija na maslahi kwa umma kwa maendeleo ya Taifa kama yanavyoainishwa katika ilani hii.

### 1.3 Muundo wa Ilani Hii

Kimuundo, ilani hii ina sura kuu 11. Sura hizi zinaelezea kuhusu ilani hii, tathimini ya utekelezaji wa ilani iliyopita ,mafanikio, changamoto za sasa pamoja na matamko kuhusu Tanzania tuitakayo.

a) Sura ya kwanza inaelezea kwa ujumla kuhusu ilani hii ya AZAKI , malengo ya ilani pamoja na umuhimu wa uchaguzi.

b) Sura ya pili inazungumzia kuhusu uhuru wananchi, uhuru wa watu na taasisi kwa kuangalia zaidi uhuru wa kujieleza, uhuru wa kujumuika na uhuru wa kushirikiana.

c) Sura ya tatu inafafanua zaidi kuhusu umuhimu wa kuzingatia Katiba, utawala bora na utawala wa sheria hapa nchini.

d) Sura ya nne inaelezea masuala ya maendeleo endelevu na uchumi jumuishi hapa nchini.

e) Sura ya tano inazungumzia masuala ya rushwa, uwajibikaji na usimamizi wa rasilimali za umma

f) Sura ya sita inazungumzia kuzingatia masuala ya jinsia, ujumuishi na makundi maalum

g) Sura ya Saba, inasisitiza upatikanaji na ufikiwaji wa huduma muhimu za kijamii kama vile afya , elimu, maji na hifadhi ya jamii.

h) Sura ya Nane – inaelezea masuala ya Amani, Usalama , Umoja na Mshikamano wa Taifa.

i) Sura ya Tisa, Diplomasia na Mahusiano ya Kimataifa.

j) Sura ya Kumi inatoa wito kwa makundi mbalimbali na hitimisho.

### 1.4 Utaratibu wa Kuandaa Ilani ya AZAKI ya Mwaka 2024/2029

Ilani hii imeandaliwa kwa ushirika mkubwa wa asasi za kiraia hapa nchini. Mchakato ulianza kwa kuandaa timu ndogo ya wataalam wa AZAKI toka mashirika machache walioweza kukaa na kuandaa rasimu ya mwongozo wa Ilani ya AZAKI. Kabla ya kuanza kuandika ilani hii , dodoso la maswali kuhusu Ilani hii iliandaliwa na kusambazwa kwa wana AZAKI. Takriban wana AZAKI 300 kutoka mikoa na wilaya zote za Tanzania walijaza dodoso na kutoa maoni yao kuhusu Ilani hii. Mapendekezo yote ya AZAKI yamezingatiwa katika Ilani hii. Baada ya kupata rasimu ya Ilani ya AZAKI , wana AZAKI walishirikishwa tena tarehe 21/08/2024 kupitia rasimu hiyo na kutoa maoni kabla ya kufikia hatua za mwisho za maandalizi ya uzinduzi wa ilani hii.

Machapisho na taarifa mbalimbali za AZAKI na serikali zilifanyiwa marejeo ili kuandaa Ilani yenye kukidhi haja za Watanzania kwa ujumla. Pia sera, taarifa za maendeleo na mikakati mbalimbali ya serikali ilichambuliwa ili kuona kama yale ambayo AZAKI walipendekeza katika ilani ya 2019/2024 yalifanyiwa kazi. Ilani hii pia imezingatia mipango ya sasa ya maendeleo Tanzania bara na Zanzibar pamoja na mikakati mbalimbali ya kimataifa kama mipango endelevu ya maendeleo (SDGs)

### 1.5 Jitihada zilizofikiwa katika Ilani AZAKI ya mwaka 2019-2024

Sehemu kubwa ya mapendekezo ya Ilani ya AZAKI ya 2019/24 yamefanyiwa kazi na serikali ya awamu ya sita kuanzia mwaka wa 2021 hadi sasa. Ujio wa Rais Samia umechangia kwa sehemu kubwa kufanya matamko ya ilani ya AZAKI kutekelezwa kwa kiasi kikubwa pamoja na kwamba bado kuna changamoto zingine zinaendelea nchini kama watu kutekwa, kukamatwa kwa wapinzania na changamoto zingine kama kule Ngorongoro na maeneo mengine yenye migogoro ya ardhi. Bado Tanzania Tuitakayo hatujaweza fikia pamoja na kwamba miaka miwili ya Mwanzao ya Rais Samia , tulianza kuona dalili za kuelekea katika Tanzania tuitakayo. Pamoja na mafanikio haya bado kiu ya wana AZAKI kufikia Tanzania tuitakayo haijafikiwa kwa kiwango kinachotakiwa.

a) Katika Ilani ya AZAKI 2019-2024 kipengele namba 2.4.5.3, na kipengele 10.3.3 tulidai uhuru wa kukusanyika na utawala wa kidemokrasia nchini, hii imedhihirika na kutelekelezwa kwa kuondolewa kwa zuio la kufanyika kwa mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa na kufunguliwa kwa vyombo vya habari ikiwemo magazeti kama vile, Mawio, Tanzania Daima na wanahalisi. Pia AZAKI zimeweza kuendelea kufanya kazi zao bila changamoto za kuzuia mikutano na kazi zingine. Baadhi ya sheria za uchaguzi zimefanyiwa maboresho kama tulivyopendekeza katika Ilani zilizopita.

b) Ilani ya AZAKI 2019-2024 kipengele namba 3.5.1.3 kilijikita katika kudai kukua kwa utawala wa kisheria na upatikanaji wa haki nchini Tanzania, kufuatia utekelezaji huu, Serikali imekuwa ikifanya maboresho katika sekta ya haki jinai, kufungulia akounti za benki za wote ambao walifungiwa katika awamu iliyopita, Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, falsafa ya R nne. (4R), na kuendelea kwa taratibu za katiba mpya, Vyote vikiwa na dhumuni la kukuza utawala wa kisheria, demokrasia na haki. Rais pia amekuwa akihubiri maswala la utawala wa sheria na utawala bora ikiwemo viongozi kuheshimu haki za binadamu.

c) Ili kuwa na uchumi jumuishi na maendeleo endelevu, ilani ya AZAKI 2019-2024 ilishinikiza na kudai viongozi kusimamia suala la ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa hadi 10%, ni dhahiri kwamba japo asilimia hii bado kufikiwa, kumekuwa na ukuaji wa uchumi unaoridhisha ambapo taarifa ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Uwekezaji) wa June 2024 ilisema pato la ndani la Tanzania (GDP) lilikua kwa Sh7.1 trilioni mwaka wa 2023, na kufikia Sh148.3 trilioni mwaka 2023.hii ni pamoja na ukuaji wa pato halisi la Taifa kufikia 5.4% mwaka 2024 kutoka matarajio ya ukuaji wa 5.2% mwaka 2023. Miradi ya maendeleo imeendelea kufanyika kwa ufanisi hapa nchini na kuwafikia watanzania wengi.

d) Katika dhana ya kukuza uchumi, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya AZAKI 2019-2024, Zanzibar imepiga hatua katika sekta mbalimbali za kiuchumi na maendeleo endelevu kupitia Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, na kupelekea kukua kwa sekta mbalimbali ikiwemo Kuongezeka kwa watalii waliotembelea Zanzibar kufikia watalii 638,498 mwaka 2023 kutoka watalii 548,503 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 16.4; ambao wameingiza kiasi cha TZS 59.7 bilioni ukilinganisha na TZS 51.32 bilioni kwa mwaka 2022. Hali hii imechangia Pato halisi la Taifa (GDP at constant price) kuongezeka na kufikia thamani ya TZS 3,758.8 bilioni mwaka 2023 kutoka thamani ya TZS 3,499.0 bilioni mwaka 2022 sawa na kasi ya ukuaji wa asilimia 7.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2022.

e) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), katika utekelezaji wa ilani ya AZAKI 2019-2024 kipengele namba 5.4.5.3 (iii), imeanzisha mwongozo wa udhibiti wa mabadiliko ya Tabia Nchi kwa kutekeleza Mikataba ya kimataifa (Paris Agreement 4 November 2016) ambapo kwa sasa Tanzania inatekeleza kupitia taasisi na Miongozo mbalimbali ikiwemo (2022 National Carbon trading guidelines) inayowezesha jamii kutunza misitu na kujipatia fedha nyingi kupitia biashara ya hewa ukaa. Mikakati mingi ya kumbambana na madaliko ya Tabia nchi imeendelea kuanzishwa hapa nchini.

f) Ilani ya AZAKI 2019-2024 kipengele namba 6.4.6.2 (i), ilidai viongozi kuhakikisha marekebisho ya Sheria ya ndoa vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 vinavyoruhusu mtoto wa miaka 14 kuolewa. ni dhahiri kwamba utekelezaji wa ilani hii umefanikisha harakati za watetezi mbalimbali wa haki za watoto na kufanikisha kuifanya Mahakama kutekeleza ilani hii kwa kutoa hukumu ya kubatilisha vifungu hivyo. Pia Mtoto wa Kike alyepata ujauzito akiwa shuleni sasa anaruhisiwa kuendelea na masomo.

g) Katika utekelezaji wa ilani ya AZAKI 2019-2024 kipengele namba 7.3.2.3 (Vi), AZAKI zilidai uboreshaji wa miundombinu za Afya hususani vijijini kwa masilahi mapana ya wananchi wa Tanzania, ni dhahiri kwamba kupitia utekelezaji wa ilani hii, serikali imeweza kufanya uwekezaji unaoridhisha katika miundombinu ya kutolea huduma za afya ambapo vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 8,549 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 9,610 Machi 2024. Hii ni sawa na ongezeko la vituo 1,061.

h) Katika utekelezaji wa ilani hii, serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imejidhatiti kuimarisha matumizi ya tekonolojia katika kufundishia na kujifunzia kwa kuweka kipaumbele kwa bajeti ya fedha 2024-2025 kuziunganisha na mkonga wa taifa taaasi za Elimu zikiwemo; skuli 217

za Sekondari, Vituo vya walimu 12 na Vituo vya Ubunifu wa Kisayansi (Hubs) 22 pamoja na kuzipatia vifaa vya TEHAMA. Hii ni hatua pia katika utekelezaji wa ilani ya AZAKI kuhusu huduma za elimu kipengele namba 7.3.1.3 (ii) na teknolojia kipengele namba 11.4.2 cha Ilani hiyo

i) Kipengele 8.3.3 (i),cha ilani tulidai viongozi kuhakikisha ulinzi na usalama wa raia unaimarika nchini, Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Bungeni wakati wa uwasilishaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya 2024/2025, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 makosa makubwa ya Jinai yaliyoripotiwa katika Vituo vya Polisi yamepungua kutoka 45,485 hadi 43,146 sawa na asilimia 5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Hii inaonyesha kuimarika kwa jitihada za kuhakikisha ulinzi wa raia na mali zao kunakopelekea amani kutawala nchini na kuwezesha wananchi kufanya kazi zao za kiuchumi na kijamii.

j) Ili kukuza Diplomasia nchini, ilani ya AZAKI 2019-2024 kipengele namba 9.6 (i), kilijielekeza katika kuhimiza viongozi wajao kutekeleza Mikataba mbalimbali yakimataifa, na kikanda, kufuatia wito huu, Tanzania imewasilisha ripoti kuhusu utekelezaji wa mikataba ya kikanda kama vile UPR, Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) na kuanza mchakato wa uwasilishaji wa taarifa kuhusu Mkataba wa Mapambano Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia na Unyanyasaji (Maputo Protocol)

### 1.6 Ni kiongozi yupi anaweza kutupeleka katika Tanzania tuitakayo

Asasi za Kiraia (AZAKI) kwa umoja wetu tunakumbusha kuwa kiongozi anayefaa kuiongoza Tanzania tuitakayo ni mwenye sifa zifuatazo;

a) Mtetezi na mlinzi wa katiba na haki za binadamu. Hii ni sifa kuu kwa kiongozi yeyote yule kuanzia ngazi za chini za serikali mpaka ngazi za juu.

b) Ambaye yupo tayari kuleta Taifa pamoja, kujenga Tanzania upya, kueneza mshikamano na kuhamasisha umoja wa kitaifa uliojengeka kwa misingi ya kikatiba.

c) Kiongozi bora ni yule anayeweza kusimamia, kutetea na kulinda haki za binadamu.

d) Awe na utashi na busara za kiuongozi na asiyekubali kupitisha na kusimamia sheria mbovu zenye kukandamiza utawala bora, demokrasia na haki za binadamu.

e) Ni muwazi katika utendaji kazi wa serikali na anayethamini ushirikishwaji wa wananchi katika mipango ya umma kwa maendeleo ya Taifa

f) Kiongozi anapaswa kuwa muumini wa maendeleo shirikishi yatakayoweza kuinua uchumi na kutengeneza mazingira rafiki ya ajira kwa maendeleo endelevu.

g) Ni muwajibikaji na aliye tayari kufanya maamuzi yenye tija kwa Taifa pamoja na kuwawajibisha viongozi wengine wa umma wanaposhindwa kutekeleza majukumu yao bila kuvunja sheria za nchi.

h) Ni mwadilifu, asiyetoa wala kupokea rushwa, mzalendo kwa nchi yake na aliye tayari kuondoa mifumo ya rushwa na ubadhirifu nchini.

i) Ni mahiri katika kusimamia na kulinda rasilimali za nchi yetu ikiwemo kupinga mikataba ambayo haina tija kwa nchi yetu.

j) Anayeamini kwa dhati katika misingi ya usawa wa kijinsia,ushiriki na ujumuishi.

### 1.7 Vipaumbele vikuu vya AZAKI kwa mwaka 2024-2029

#### 1.7.1 Katiba Mpya

Tukukumbuke kuwa mchakato wa kuandaa Katiba mpya ulikwisha anza na umetumia pesa nyingi za Watanzania. Ni wazi kuwa hadi tunapokwenda kupiga kura Octoba 25 mwaka huu mchakato wa Katiba mpya hautakuwa umekamilika, kwa mantiki hiyo sisi wana AZAKI tunawataka wagombea wanaotafuta ridhaa ya uongozi watumie muda wa kampeni kuwahakikishia watanzania kuwa wataendeleza mchakato wa upatikanaji wa Katiba ya wananchi. Pia wahakikishie wananchi kuwa watarurudisha misingi ya upatikanaji wa Katiba kwa kuweka mazingira yatakayoheshimu maoni ya wananchi na kujali ushiriki wa wananchi wote katika kutunga Katiba. AZAKI tunasisitiza rasimu ya Katiba iliyoandaliwa na Tume ya Jaji Warioba ipewe kipaumbele katika kupata katiba mpya kwa kuwa ndio rasimu pekee ambayo imebeba maoni ya wananchi.

#### 1.7.2 Sera ya Uchumi Jumuishi na Maendeleo Endelevu

Tunataka kiongozi ambaye anatambua kwamba pamoja na kuwa kwenye uhuru zaidi ya miaka 60 watanzania wengi bado ni masikini licha ya kuwa Taifa hili lina utajiri mkubwa.Tunamhitaji kiongozi atakayeweza kuja na sera ya Uchumi wa Taifa yenye malengo ya kulikwamua Taifa kiuchumi kwa kujenga mazingira sawa na wezeshi ya kiuchumi kwa watanzania wote bila kuweka matabaka ya walionacho na wasionacho. Tunahitaji kuona Sera ya Taifa ya Uchumi Jumuishi na Maendeleo Endelevu itakayosaidia kuliinua Taifa kutoka Taifa linalotegemea misaada na kuwa Taifa linalojitegemea kiuchumi kwa kuongeza uzalishaji wa ndani, kukuza viwanda vya ndani na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya serikali.

### 1.7.3 Usimamizi wa Rasilimali za Umma na Kutomeza Rushwa

Tanzania ni mojawapo ya nchi zilizobarikiwa kuwa na rasilimali nyingi kwa mfano ardhi, madini, gesi asilia, mafuta, bahari, maziwa, mito, wanyama pori na misitu asilia. Katika miaka ya hivi karibuni, ulinzi thabiti wa rasilimali za nchi hususani kwa mamlaka husika umekosekana nchini hali inayosababisha upotevu na ubadhirifu wa rasilimali za nchi kwa mfano, uvunaji haramu wa rasilimali misitu na bahari, umilikishwaji wa ardhi ya wazawa kwa wageni kinyume na sheria pamoja na ujangili wa wanyamapori. Pia rushwa na ufisadi vimeshamiri nchini, uingiaji wa mikataba ya uwekezaji uvunaji na wa rasilimali isiyo na tija kwa Taifa. Tunawataka viongozi wote wenye kuwania nafasi za uongozi kutamka na kuweka bayana namna watakavyosimamia na kulinda rasilimali za nchi ili zitumike kwa manufaa ya Taifa na watu wake na kutomekeza aina zote za rushwa hapa nchini.

### 1.7.4 Haki za Binadamu, Utawala wa Sheria na Mgawanyo wa Madaraka

Kwa muda mrefu sasa, Tanzania imekuwa na changamoto kubwa kuhusu utawala wenye kufuata misingi ya sheria, haki za binadamu na mgawanyo wa madaraka. Tunahitaji kuona Tanzania yenye viongozi watakaoweza kusimamia utawala wa sheria, kulinda haki za binadamu, usalama wa watoto, haki za wanawake, haki za watu wenye ulemavu, demokrasia na misingi ya mgawanyo wa madaraka. Tunawataka viongozi watakaochaguliwa waweke nguvu zaidi kwenye kuboresha huduma za msingi za kijamii kama vile elimu, afya, maji na miundombinu.

### 1.7.5 Ulinzi wa Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi

Kutokana na changamoto ya sasa ya dunia kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na uharibifu wa mazingira, Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea kupata madhara ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Kwa malengo ya kukabiliana na changamoto hii, tunawataka viongozi kuweka ajenda hii ya ulinzi wa mazingira pamoja na kuipitia na kutekeleza mikakati inayoendana na madhara ya kimazingira ya wakati huu ili kupambana na mabadiliko ya tabia nchi hapa Tanzania.

## 1.8 Dhana na Umuhimu wa Uchaguzi Huru

Haki za kisiasa na kiraia zinafafanua uchaguzi wa kidemokrasia kuwa ni mchakato mzima wa kupata viongozi wa ngazi mbalimbali za serikali kwa kuchaguliwa na wananchi. Tanzania hufanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa kila baada ya miaka mitano (5) na Uchaguzi Mkuu hivyo hivyo.

Tunataka viongozi wajao wasimamie misingi ya uchaguzi huru ikiwemo, uwazi, usawa, uwajibikaji, uandikishwaji wa wapiga kura kwa wakati, kutolewa kwa elimu ya uraia na mpiga kura, mchakato sawa wa uteuzi wa wagombea, wagombea

kupata fursa sawa za kufanya kampeni zao na kwa uhuru, wananchi kupiga kura kwa wakati na kwa uhuru, maboresho ya sheria za uchaguzi na vyama vya siasa ili kuweka mazingira sawa kwa wagombea kwenye vyombo mbalimbali vya kiuchaguzi ikiwemo fursa sawa kwa vyombo vya habari, ushiriki na ushirikishwaji wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika hatua zote za uchaguzi, vyombo vya dola kutoingilia mchakato wa uchaguzi, utangazaji wa matokeo ya uchaguzi bila kuchelewesha, kukubali au kukataa matokeo ya uchaguzi pamoja na upingaji wa matokeo ya uchaguzi.

### 1.9. Tunu za Taifa

Tunu za Taifa ndio kichocheo muhimu cha kufikia malengo ya Tanzania tuitakayo. Tunu hizi za kitaifa zinaelezwa zaidi katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 katika sehemu ya pili, ibara ya tisa inayohusu malengo ya Taifa. Katika eneo hili linasistiza uongozi unaozingatia udugu , amani kwa kuzingatia mazingira yaliyomo na ya nchi yetu. Tunu za Taifa zinasisitiza pia umuhimu wa kuzingatia utamaduni wetu. Kwa hiyo kwa mujibu wa Ibara ya 9 ya Katiba, mamlaka ya nchi na vyombo vyake vyote vinawajibika kuelekeza sera na shughuli zake zote.

Kwa kuzingatia Ibara ya 9 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Sisi wana AZAKI tunapendekeza mambo yafuatayo kuwa ndio Tunu za Taifa zinazopaswa kuzingatiwa wakati na baada ya uchaguzi na viongozi wote;

a) Umoja
b) Utu na Ubinadamu
c) Mshikamano na Undugu.
d) Amani na Utulivu
e) Uzalendo kwa Taifa
f) Uadilifu
g) Haki za Binadamu na Usawa
h) Uwazi
i) Uwajibikaji
j) Lugha ya Kiswahili
k) Maendeleo ya Watu na Uchumi Jumuishi
l) Rasilimali asili za Taifa na Utamaduni



# SURA YA PILI

# UHURU, HAKI ZA KIRAIA NA ZA KISIASA

## 2.1 KUHUSU SURA HII

Kiujumla, sura hii inaeleza mambo ambayo asasi za kiraia zinatarajia kuona katika kufikia Tanzania Tuitakayo, ikiwemo kuimarishwa kwa haki za msingi za kiraia na kisiasa na kukomeshwa kwa vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu ili kuchochea maendeleo ya nchi yenye wananchi wenye furaha na uhuru wa kufanya shughuli mbalimbali. Ingawa amani imekuwepo kwa miaka mingi, bado imeendelea kughubikwa na vitendo vinavyoathiri haki za kiraia na kisiasa kama vile mauaji, uminywaji wa uhuru wa vyombo vya habari, vurugu, vikwazo vya upatikanaji wa haki, na changamoto za mfumo wa haki jinai. Vitendo hivi vyote vinaathiri wananchi, sifa na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Kwa upande mwingine sura hii inaikumbusha Tanzania kuwa, mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu imeweka misingi ambayo inazitaka nchi wanachama kutimiza wajibu wao wa kulinda haki za binadamu na kujiepusha na vitendo vya utekaji pamoja na mauaji, kuchukua tahadhari mahususi na za kimkakati wakati wa utekelezaji wa shughuli pamoja na operesheni mbalimbali, kufanya uchunguzi rasmi na wa kina kuhusu matukio mbalimbali dhidi ya ukiukwaji wa haki, ikiwemo matukio ya mauaji na kupotea kwa watu, kuchukua hatua mahususi za kulinda haki za makundi maalumu, kuhakikisha usalama wa watu ambao wapo chini ya ulinzi wa vyombo vya dola na kuhakikisha watu wote wanaokiuka misingi ya haki za binadamu wanafikishwa mahakamani na kuchukuliwa hatua stahiki.

## 2.2 UTEKELEZAJI WA HOJA ZA ILANI 2019-2024

### 2.2.1 Uhuru wa Kujieleza

#### a) Jitihada Zilizofikiwa

i) Kumekuwa na mafanikio katika uhuru wa kujieleza kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibari. Itakumbukwa wakati wa maadhimisho ya siku ya uhuru

wa vyombo vya habari Duniani mwaka 2023 huko Unguja - Zanzibar, Serikali kupitia Wazara ya Habari Zanzibar, ilisema kwamba mchakato wa kutunga sheria ya habari umeshafikia asilimia 80% na umejumuisha asilimia 99% ya mapendekezo ya wadau.

ii) Kwa upande wa Tanzania Bara, hali ya uhuru wa vyombo vya habari imeimarika kwa kiasi kwa kufunguliwa kwa vyombo vya habari vilivyofungiwa katika awamu ya Tano ikiwemo, gazeti la MwanaHalisi, Mawio, Mseto na Tanzania Daima.

iii) Pia mkakati wa Serikali wa kurekebisha mfumo wa haki jinai ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliunda Tume maalaumu ya kupitia mfumo wa haki jinai nchini, ambayo ilitoa mapendekezo mbalimbali ikiwemo kufuta sheria gandamizi.

iv) Kufanyika kwa maboresho madogo ya sheria za habari hapa nchini kama ambavyo ilani ya AZAKI ya 2019/24 ilivyosisitiza.

**b) Changamoto**

i) Kwa kipindi cha miaka mitano tangu kutolewa kwa ilani ya Azaki ya uchaguzi ambayo iliweka matamko mahususi ya uimarishwaji wa Haki za Kirai na Kisiasa, Tanzania imepita katika vipindi mbalimbali ya kupanda na kushuka katika viwango vya kimataifa pamoja ulinzi wa Haki za Binadamu kama ilivyoanishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Mathalani mwaka 2021 hadi 2022 Tanzania ilipanda kwa nafasi moja (1) katika viwango vya Kielelezo cha Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani kwa mujibu wa Waandishi wa Habari Wasio na Mipaka (RSF), hata hivyo mwaka 2023 Tanzania ilishuka kwa kiasi kikubwa kwa nafasi 20 hadi kwa nafasi ya 143.

ii) Aidha kwa upande wa upatikanaji wa Habari, bado kumekuwa na changamoto hasa Sheria ya upatikanaji wa Habari ya 2016 ambayo inaweka kosa kwa mtu kutoa habari, pia changamoto za kiutendaji zinazopelekea mlolongo na muda mrefu wa kujibu maombi ya mtu kupata taarifa fulani kutoka katika taasisi ya umma.

iii) Kwa upande wa Zanzibar hadi kufikia mwaka 2024 bado wadau wa vyombo vya habari walionesha changamoto wanazokumbana nazo kufuatia uwepo wa Sheria ya Kanuni ya adhabu ya Zanzibar Na.6, 2004 kuwa ni Sheria inayopunguza uhuru wa vyombo vya habari hususani kifungu cha 44 (1) cha Sheria hiyo ambacho kinakataa kusema, kuandika au kuchapisha maudhui ya "uhaini" bila kutoa maana ya neno "uhaini"

iv) Mwaka 2020 wakati wa Uchaguzi Mkuu, Tanzania ilipitia changamoto ya upatikanaji wa mtandao ambayo iliteta madhara ya wananchi kutopata taarifa kwa wakati na kufikia huduma zilizohitaji matumizi ya mtandao.

v) Aidha, mwaka 2023 haki ya upatikanaji wa habari ilikumbana na vikwazo vya kutopatikana kwa jukwaa la kijamii (ClubHouse) linaloendeshwa kwa program ya mtandao wa kijamii ambapo wananchi walikuwa wanalitumia jukwaa hilo kuendesha mijadala na kutoa maoni mbalimbali juu ya uendeshwaji wa nchi, changamoto na vipaumbele vyao wanavyovitaka.

vi) Kwa vipindi tofatuti kati ya mwezi Februari na Agosti 2023, mtandao wa Clubhouse uliingia kwenye changamoto ya kutopatikana bila ya matumizi ya programu ya Virtual Private Network (VPN). Hali hii imeaathiri kwa kiwango kikubwa uhuru wa kujieleza mitandaoni kwa kuwanyima wananchi fursa ya kujadili mada mbalimbali za kijamii, kisiasa, na kiuchumi.

vii) Kwa upande mwingine, Agosti na September 2023 iliripotiwa kufungiwa kwa nyimbo za baadhi ya wasanii ikiwemo wimbo wa "Amkeni" na "Mnatuona Nyani". Nyimbo hizi zilipigwa marufuku kwa madai ya uchochezi. Wasanii walioimba nyimbo hizi walishitakiwa chini ya Sheria ya Makosa ya Mtandao ya 2015.

viii) Tunapoelekea chaguzi za 2024/2025, uhuru wa kujieleza umeendelea kuminywa, tukishuhudia matukio mbalimbali ya kutekwa na kupotea kwa wananchi ambao wanatumia mitandao ya kijamii kukosoa vitendo vya Serikali. Jaribio la hivi karibuni la mauaji ya mwanaharakati wa mtandaoni limezua taharuki za kiusalama kwa wananchi.

ix) Vitendo vya ukandamizaji dhidi ya wanachama wa siasa wa upinzani na wakosoaji wa serikali vimeongezeka, huku polisi wakiwakamata bila kufuata sheria kwa mashtaka kama "kuhatarisha amani." Hali hii inahitaji mamlaka kuchukua njia ya kimaendeleo zaidi kutatua changamoto kuliko kuminya uhuru wa kujieleza.

### 2.2.2. Uhuru wa Kukusanyika na Kujumuika

#### a) Jitihada zilizofikiwa

i) Uhuru wa vyama vya siasa umeanza kumarika kwa kiasi kwa vya siasa kufanya shughuli zao na maandamano kwa uhuru. Rais Samia alifanya maamuzi ya kuondoa zuio la kufanya mikutano ya kisiasa iliyowekwa mwaka 2016. Pendekezo hili liliwekewa mkazo na ripoti ya kikosi kazi cha kupitia hali ya demokrasia ya vyama vingi nchini Tanzania mwaka 2022 kilichoundwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni mkakati wa kuimarisha hali ya demokrasia nchini.

ii) Baada ya kuondolewa kwa marufuku ya mikutano ya kisiasa vyama vya siasa vimekuwa vikifanya mikutano mbalimbali ya hadhara kwa uhuru.

iii) Rais Samia aliingia madarakani na kuanzisha falsafa ya R nne ambazo alizitumia vizuri kurudisha umoja wa kitafa na mshikamano. Alikutana

na vyama vya siasa na kuanza mchakato wa maridhiano na wengi wao wakarudi katika kazi zao za kisiasa kwa uhuru na waliokuwa nje ya nchi walirejea na wengine kufutiwa mashauri mbalimbali.

**b) Changamoto**

i) Pamoja na jitihada zilizofanywa kwenye uhuru wa vyama vya siasa bado kumekuwa na matukio na malalamiko yaliyoripotiwa ya kuweka kizuizi cha uhuru wa kukusanyika na kushirikiana, ikiwemo kufanya mikutano kama ilivyoripotiwa na baadhi ya vyama vya siasa ikiwemo ACT Wazalendo ambao walilamika kunyimwa haki ya kufanya maandamano ya amani kupinga ubadhirifu na usimamizi mbovu wa fedha za umma uliofichuliwa kwenye ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

ii) Kwa upande mwingine, kumefanyika marekebisho ya sheria na kanuni kuu zinazosimamia uhuru wa kukusanyika na kushirikiana, ikiwemo Sheria ya Vyama vya Siasa (iliyorekebishwa mwaka 2019), Sheria ya NGOs ya 2002 (iliyorekebishwa mwaka 2019), na Sheria ya Msingi ya Haki na Wajibu (BRADEA), iliyorekebishwa mwaka 2020, mabadiliko hayo yamesababisha vikwazo vya utekelezaji wa haki za msingi. Kwa mabadiliko haya ya sasa, Asasi za Kiraia haziwezi tena kufungua kesi kwa niaba ya raia ikiwa kuna uvunjifu wa Haki za Binadamu, Sheria ya BRADEA inaweka sharti la kuwa ili shauri hilo lifunguliwe ni lazima taasisi hiyo ioneshe maslahi na athari binafsi dhidi ya tukio hilo. Hivyo, ni sawa na kusema kwamba, mabadiliko ya sheria hiyo yananyima uhuru wa taasisi kushirikiana.

iii) Matukio ya watu kuteswa yaliripotiwa wakati na baada ya uchaguzi wa mwaka 2020, matukio hayo yalirekodiwa katika mikoa ya Dodoma, Songwe, Mbeya, Mara, Mwanza, Arusha, Kigoma na Dar es Salaam. Matukio hayo yanajumuisha malalamiko ya unyanyasaji kwa wanajamii ya Kimasai waliokamatwa katika Wilaya ya Ngorongoro na watoto kutoka kwa maafisa wa polisi. Mwaka 2023 kuliripotiwa vitendo vya mateso yalifanywa na walinzi wa Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) dhidi ya wakazi wa vijiji katika Wilaya ya Mbarali na vijiji katika maeneo yanayopakana na hifadhi za Taifa.

### 2.2.3 Ushiriki wa Wananchi katika Uongozi na Maendeleo

**a) Jitahada Zilizofikiwa**

i) Wananchi wamekuwa wakishiriki katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa katika ngazi ya Serikali ya Mitaa kupitia miundo ya kamati mbalimbali za utekelezaji wa miradi hiyo.

ii) Pia, wananchi wamekuwa wakipata taarifa mbalimbali juu ya utekelezaji wa mipango hiyo kupita taarifa kutoka Ofisi ya Msemaji Mkuu wa Serikali pamoja na njia mbalimbali za kuhabarisha umma kupitia taasisi husika zinazotekeleza miradi hiyo, mathalani ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere, Reli ya Treni ya Umeme (SGR), ununuzi wa ndege, Ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Uganda pamoja na miradi mingine ya maendeleo.

**b) Changamoto**

i) Bado kumekuwa na changamoto ya ushirikishwa kwa wananchi katika hatua za awali za kupanga vipaumbele vya maendeleo kabla ya kuandaa mradi husika. Hivyo, wananchi hupewa taarifa ya miradi iliyopangwa na serikali badala ya kushiriki katika maandalizi ya mradi husika.

ii) Hata hivyo, kwa kiwango kikubwa, kundi la watu wenye ulemavu wamekuwa na malalamiko mengi hasa kutoka katika mikoa ya Singida, Dodoma, Tabora, Pwani, Tanga, Rukwa na Kigoma kuhusu kutojumuishwa katika kufanya mipango ya maendeleo katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) kwa dhana potofu ya kuwa kundi hilo ni watu wasumbufu.

iii) Kwa upande mwingine, kundi la vijana linakabiliwa na changamoto mbalimbali hususani katika suala la ushiriki katika siasa na miradi ya maendeleo kwa tuhuma za kuwa na tamaa na uchu wa madaraka.

iv) AZAKI zimekuwa hazishirikishwi ipasavyo katika mipango mbalimbali ya maendeleo na zingine zimekuwa zikikumbana na vikwazo vingi vya kutakiwa kuomba vibali.

### 2.2.4 Uchaguzi Huru na Haki

#### a. Jitihada Zilizofikiwa

Katika uchaguzi wa 2020, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilitumia *Biometric Voter Registration (BVR)* kwa ajili ya uhakiki wa wapiga kura. Tukiachilia changamoto zilizojitokeza, mfumo huu uliongeza usahihi katika orodha za wapiga kura, ambapo takriban wapiga kura milioni 29.9 walihakikiwa.

#### b. Changamoto

i) Katika uchaguzi wa 2020, vituo vya habari kama Kwanza TV vilifungiwa kwa muda kwa madai ya kuripoti habari za uchochezi, na Clouds TV ilipewa onyo kali. Matukio haya yalipunguza upatikanaji wa habari huru, jambo lililokosolewa na taasisi ya Human Rights Watch.

ii) Vyama vya upinzani kama CHADEMA na ACT-Wazalendo vilikumbana na changamoto kama mikutano ya kampeni kuzuiliwa na viongozi kukamatwa. Tundu Lissu (CHADEMA) alikabiliwa na vikwazo vingi, hali iliyoathiri usawa wa kisiasa.

iii) Kulikuwa na taarifa nyingi za matumizi ya nguvu dhidi ya wafuasi wa upinzani, kama tukio la Zanzibar ambapo watu walijeruhiwa na kufariki.

iv) Licha ya juhudi za kuhamasisha, asilimia ya wapiga kura waliojitokeza ilikuwa 50.7%, ikilinganishwa na 67.3% mwaka 2015. Vijana wengi walikosa hamasa kutokana na hofu ya kutokuwepo kwa usawa katika uchaguzi.

v) Mashirika ya kiraia yalinyimwa vibali vya kufuatilia uchaguzi, jambo lililopunguza ushiriki wa CSOs katika kutoa ripoti za uwazi na haki, na kudhoofisha imani ya umma katika mchakato wa uchaguzi.

vi) AZAKI nyinngi zilishindwa kushiriki kwenye shughuli za uchaguzi kutokana akaunti zao za fedha kufungiwa wakati wa uchaguzi

## 2.3 TAMKO LA ILANI

### 2.3.1 Uhuru wa Kujieleza

a) Kupitia upya sheria na kanuni zote zinazohusiana na uhuru wa kujieleza ili kuhakikisha zinaendana na viwango vya kimataifa vya uhuru wa kujieleza kwa lengo la kulinda haki za binadamu.

b) Kuwepo kwa mwongozo kwa vyombo vya habari binafsi na vya umma wa kuweza kuanzisha programu zinazoweka fursa sawa ya ushiriki wa wananchi katika mambo yanayowahusu, hii itaboresha kiwango cha uhuru wa kujieleza nchini.

c) Viongozi watimize wajibu wao wa kufanya mikutano ya kila mwezi katika maeneo yao ili kuwezesha jamii kupata taarifa kuhusu shughuli za serikali.

d) Kufanya marekebisho ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 kulingana na uamuzi wa Mahakama ya Haki za Binadamu ya Afrika Mashariki wa mwaka 2019.

e) Kufanya marekebisho ya Sheria ya Kupata Taarifa na Sheria ya Makosa ya Mtandao ili ziendane na viwango vya kimataifa vya Haki za Binadamu.

f) Kukamilisha na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Haki za Binadamu ili kuimarisha ulinzi wa uhuru wa kujieleza.

g) Kufanya marekebesho ya sheria ya makosa ya mitandaoni kama ilivypendekezwa na AZAKI katika hatua mbalimbali.

### 2.3.2 Uhuru wa Kukusanyika na Kujumuika

a) Kufanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ili iweze kuendana na viwango vya kimataifa vya Haki za Binadamu.

b) Kuridhia Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala (ACDEG) wa mwaka 2007.

c) Kutekeleza kwa vitendo mapendekezo ya Tume Maalumu ya Kuangalia jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai (Tume ya Haki Jinai) na Kikosi Kazi kilichoundwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano kuhusu Hali ya Demokrasia ya vyama vingi.

d) Kukamilisha na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Haki za Binadamu ili kuimarisha ulinzi wa uhuru wa kukusanyika na kujumuika.

e) Kufanya maboresho ya sheria za AZAKI pamoja na sheria zingine zinazofifisha utendaji wa AZAKI hapa nchini.

### 2.3.3 Matukio ya Kuteswa na Kutekwa

a) Kuimarisha ushirikiano wa kijamii katika kuzuia na kupambana na uhalifu nchini.

b) Kulinda haki za watu waliyochini ya ulinzi wa vyombo vya dola kama, Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji, TAKUKURU, Majeshi ya Hifadhi na vyombo vingine vya dola.

c) Kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kuwekeza katika matumizi ya CCTV na teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) katika kugundua na kuzuia uhalifu ili kukomesha vitendo vya mateso.

d) Kutekeleze mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai kuhusu vitendo vya mateso.

e) Kuridhia kwa Mkataba wa Kimataifa dhidi Vitendo vya Mateso (CAT) na Mkataba dhidi Utekaji wa Binadamu (UN Convention against Enforced Disappearance).

f) Kukamilisha na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Haki za Binadamu ili kuimarisha ulinzi wa uhuru wa kujieleza.

g) Kuimarisha na kuipatia fedha za kutosha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG) ili iweze kutimiza majukumu yake kikamilifu na kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya mateso.

### 2.3.4 Ushiriki wa Wananchi Katika Uongozi na Maendeleo

a) Kufanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuongeza ushiriki wa Wanawake, Watu wenye Ulemavu na Vijana katika maamuzi ndani ya vyama vya kisiasa ili kuongeza ushiriki wa makundi hayo.

b) Kuridhia Mkataba wa Nyongeza wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu juu ya Haki za Watu wenye Ulemavu barani Afrika wa mwaka 2018.

c) Vyombo vya habari viimarishe mifumo ya kutoa, kufichua matukio ya ukiukwaji wa Haki za Binadamu ili kuongeza uelewa wa umma juu ya Haki za Binadamu, Uongozi na Maendeleo.

d) Kupanua wigo wa AZAKI kushiriki mipango mbalimbali ya maendeleo.

e) Kuteua mwakilishi wa AZAKI kwenda bungeni kutoka kwa AZAKI moja kwa moja na sio kutoka kwa vyama vya siasa ili awajibike kwa AZAKI.

f) Kuondoa vikwazo vinavyokwamisha uhuru wa AZAKI kufanya kazi zao mbalimbali hapa nchini.

### 2.3.4 Uchaguzi Huru na wa Haki


a) Serikali inapaswa kuhakikisha uhuru wa vyombo vya habari bila vitisho wala vizuizi. Vyombo vya habari vipewe nafasi ya kuripoti kwa uwazi na usawa kuhusu uchaguzi na shughuli za kisiasa.

b) Serikali na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) zinapaswa kutoa mazingira yanayowezesha vyama vya upinzani kushiriki kwa usawa kwenye kampeni na uchaguzi bila vizuizi au manyanyaso.

c) INEC iwe na utaratibu wa uwazi wa kutangaza matokeo kwa wakati na kwa usahihi ili kuimarisha imani ya wapiga kura na wadau wengine katika mchakato mzima wa uchaguzi.

d) Serikali, vyama vya siasa, na CSOs ziongeze juhudi za kuhamasisha wapiga kura, hasa vijana, kwa njia za ubunifu kama kampeni za mitandaoni na programu za elimu

e) Serikali inapaswa kuweka mazingira wezeshi kwa CSOs kupata vibali kwa wakati na kushiriki kikamilifu katika ufuatiliaji wa uchaguzi na kutoa elimu ya uraia. Ushirikiano kati ya serikali na CSOs utaboresha uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa uchaguzi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIBA YA JAMHURI
YA MUUNGANO WA TANZANIA
YA MWAKA 1977
2008

SURA
YA **TATU**

# UKUU WA KATIBA, UTAWALA WA SHERIA, NA UTAWALA BORA

## 3.0 KUHUSU SURA HII

Tanzania ni Taifa la kidemokrasia, linalohitaji kujengwa juu ya misingi imara ya kuheshimu Katiba, Utawala wa Sheria, na Utawala Bora. Misingi hii ndiyo inayoimarisha utawala wa kidemokrasia na kuhakikisha uwajibikaji wa viongozi na ustawi wa wananchi. Ilani ya AZAKI 2019/2024 ilieleza kwamba ili Tanzania iwe na maendeleo endelevu na ustawi wa wananchi, inahitaji viongozi wanaoamini na kuheshimu misingi hii. Kila mhimili wa dola, ikiwa ni pamoja na Serikali, Bunge, Mahakama na taasisi zake, lazima zifanye kazi kulingana na mgawanyo wa madaraka kama unavyoainishwa katika Katiba na sheria za nchi. Viongozi hawa wanapaswa kutambua majukumu na mipaka yao ili kuwajibika kikamilifu bila kuingiliana au kugongana katika kutekeleza wajibu na haki za kila mmoja.

Sura hii pia inasisitiza umuhimu wa kufanya mabadiliko ya Katiba ambayo itaboresha utawala wa kidemokrasia na ustawi wa Taifa. Katiba ya sasa ina mapungufu ambayo yanadumaza uwajibikaji na maendeleo. Mchakato wa kupata Katiba mpya ulianza rasmi mwaka 2011 chini ya Tume ya mabadiliko ya Katiba (ikijulikana sana kama Tume ya Warioba) na kukwama mwaka 2014. Madai ya mabadiliko ya Katiba kwa watanzania ni ya muda mrefu ambapo Tume mbalimbali ambazo ziliundwa huko nyuma zilikuja na mapendekezo ya mabadiliko ya Katiba ikiwemo Tume ya Jaji Nyalali mwaka 1992, Tume ya Jaji Robert Kisanga mwaka 1998. Pamoja na kukwama kwa mchakato rasmi wa kupata Katiba mpya bado Katiba imekuwa kilio kisichoisha cha watanzania, wadau wa demokrasia n.k. Kwa hiyo, viongozi watakaoingia madarakani wanapaswa kutilia maanani hitaji la wananchi la mabadiliko ya Katiba ili kudumisha utawala bora na wa kidemokrasia ili kuheshimu matakwa ya watanzania.

### 3.1 UTEKELEZAJI WA ILANI YA AZAKI 2019/24

#### 3.1.1 Utawala Bora na Mgawanyo wa Madaraka

**a) Jitihada zilizofikiwa**

i. Katika awamu ya sita ya utawala wa Rais Dr. Samia Suluhu Hassan ulioingia madarakani mnamo mwezi wa 3 mwaka 2021 mpaka sasa mwaka 2024, kumekuwa na hatua kadhaa zinazotia matumaini ya kuboresha utawala wa kidemokrasia nchini. Rais Samia amejipambanua kwa **falsafa ya "R4"** iliyojikita katika dhana ya maridhiano, ustawi wa watu, mageuzi, na uwajibikaji. Falsafa hii inalenga kuimarisha umoja wa kitaifa, kukuza maendeleo, na kurekebisha mifumo ya kiutawala kwa ajili ya ustawi wa Watanzania wote.

ii. Rais aliteua Tume ya Haki Jinai ili kuboresha sheria zinazoathiri upatikanaji wa haki nchini. Zanzibar, Rais Hussein Mwinyi alianzisha kikosi kazi maalum (Oktoba 2022) kukusanya maoni ya wadau kuhusu hali ya kisiasa na kutoa mapendekezo ya kisera na kisheria.

iii. Katika utawala bora, Corruption Perception Index ilionyesha maboresho ya kupambana na ufisadi, ambapo Tanzania ilipanda nafasi saba, kutoka ya 94 (2022) hadi 87 (2023).

iv. Utawala wa Sheria kwa kiasi fulani hapa nchini umeonekana kuanzia mwaka 2021 hadi sasa.

**b) Changamoto**

i. Changamoto katika utawala bora zimeendelea kuwa changamoto ya maendeleo ya watanzania. Tukianza na ubadhirifu, ripoti ya CAG 2022/2023 ilibaini ubadhirifu wa zaidi ya TZS bilioni 6, huku 2023/2024 ikionyesha ubadhirifu wa TZS bilioni 5 katika miradi na malipo yasiyo halali.

ii. Ukandamizaji wa Haki za Binadamu, kukamatwa na kufungwa kwa wanaharakati wa haki za binadamu na waandishi wa habari imeendelea kuwa jambo la kawaida huku hali hii ikididimiza utawala bora.

iii. Kukamatwa kwa viongozi wa upinzani kama Freeman Mbowe wa CHADEMA, aliyewekwa kizuizini kwa miezi kadhaa kwa mashtaka ya ugaidi ambayo yalionekana kama njia ya kuzuia shughuli za kisiasa za upinzani ni kiashiria cha utawala wa kibabe na uongozi mbovu.

iv. Mhimili wa mahakama umekosa imani kwa wananchi, baadhi ya maamuzi ya mahakama yanaonekana kuegemea upande wa serikali na chama tawala, hali inayozua hofu kuhusu uhuru wa mahakama.

v. Kwa upande mwingine kumekua na mwingiliano wa Mihimili ambapo Bunge linaonekana kuingilia majukumu ya mahakama. Mfano ni pale Bunge lilipomuita Jaji Mkuu kutoa maelezo kuhusu mwenendo wa kesi za ufisadi, hali iliyozua maswali kuhusu uhuru wa mahakama. Serikali inaendelea kuingilia maamuzi ya mahakama katika baadhi ya kesi za kisiasa, hali inayosababisha mashaka kuhusu uhuru wa mahakama na uwajibikaji wa serikali.

vi. Mifano hii inaonyesha changamoto mbalimbali zinazokabili utawala bora nchini Tanzania katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni, na inahitaji juhudi za pamoja kutoka kwa wadau wote ili kuzitatua.

vii. Bado matukio ya watu kufanyiwa ukatili na baadhi ya watendaji wa vyombo vya usalama hasa polisi bila serikali kuchukua hatua yameendelea kushamiri.

viii. Dhana ya utawala bora haizingatiwi katika maeneo kadhaa nchini hasa katika serikali za mitaa. Viongozi wamekuwa wakitenda kinyume na misingi ya utawala sheria na utawala bora. Katika Wilaya Ngorongoro huduma yingi za jamii zilisitishwa kinyume cha sheria na utawala bora na kuwaacha wananchi takriban laki moja bila huduma kwa muda wa miaka mitatu(3).

### 3.1.2 Ukatiba na Katiba Mpya

#### a) Jitihada Zilizofikiwa

i. Hatua kadhaa zimechukuliwa, ikiwa ni pamoja na kuunda kikosi kazi ambacho kilikuja na mapendekezo kuhusu hitaji la mabadiliko ya Katiba.

ii. Lakini pia Rais mwenyewe, pamoja na wasaidizi wake, katika nyakati tofauti wamekuwa wakitoa kauli mbalimbali zinazoonyesha matumaini ya kufufua mchakato wa Katiba Mpya.

iii. Aidha, mapema mwaka 2023 Rais Samia alitoa agizo la kuanzishwa kwa mchakato wa Katiba Mpya, Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria ilitoa tamko la kufufua mchakato wa Katiba Mpya kwa kutoa elimu ya Katiba kwa wananchi kwa muda wa miaka mitatu (3).

**b) Changamoto**

i) Ukosefu wa Maridhiano ya Kisiasa. Mchakato wa katiba mpya umekwama kutokana na mgawanyiko wa kisiasa kati ya vyama vya siasa, hususan kati ya chama tawala (CCM) na vyama vya upinzani. Upinzani umekuwa ukilalamikia kuwa mchakato haukuhusisha wadau wote kwa usawa, na kwamba matakwa yao hayakuzingatiwa kikamilifu.

ii) Kuahirishwa kwa Mchakato. Mchakato wa katiba mpya ulioanzishwa mnamo 2011 ulisimama mnamo 2014 baada ya Bunge Maalum kushindwa kufikia makubaliano kuhusu rasimu ya pili ya katiba. Serikali imekuwa ikiahidi kuufufua mchakato huo, lakini hadi sasa hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa, jambo linalosababisha kukwama kwa mabadiliko yanayohitajika.

iii) Mazingira ya Haki za Binadamu na Uhuru wa Kujieleza. Uhuru wa kujieleza na haki za binadamu ni vipengele muhimu katika mjadala wa katiba mpya. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kuhusu kuminya uhuru wa vyombo vya habari na wanaharakati wa haki za binadamu, hali inayozuia upatikanaji wa maoni tofauti na mjadala mpana kuhusu katiba mpya.

iv) Utaratibu wa Kurejea Rasimu za Zamani. Rasimu ya Warioba, ambayo ilitayarishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba, inasifiwa kwa kuwa na maoni ya wananchi wengi. Hata hivyo, tofauti na rasimu ya pili iliyopitishwa na Bunge Maalum, haijawahi kutumika rasmi kama sehemu ya mjadala wa katiba mpya, na suala hili limekuwa chanzo cha mvutano mkubwa.

v) Changamoto hizi zimeathiri sana mchakato wa upatikanaji wa katiba mpya nchini Tanzania, na bila maridhiano na uwazi, upatikanaji wa katiba mpya unaendelea kusuasua.

### 3.1.3 Utawala wa Sheria

**a) Jitihada zilizofikiwa**

i) Marekebisho ya Sheria ya Takwimu mwaka 2020 kwa lengo la kuboresha uwazi na usalama wa data. Kati ya 2020 na 2024, kuna ongezeko la upatikanaji wa taarifa za umma, ikiwa ni pamoja na ripoti za matumizi ya fedha na takwimu za maendeleo. Hii imeongeza uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma.

ii) Uimarishaji wa Mfumo wa Mahakama ikiwa ni pamoja na kuanzisha mahakama mpya za Kanda kama Morogoro ili kupunguza msongamano wa kesi na kuongeza upatikanaji wa haki kwa wananchi wa kanda hiyo.

iii) Lakini pia kumekua na uboreshaji wa Mifumo ya Teknolojia (e-Court) ulioanza kufanya kazi 2022 kuwa wezesha wahusika katika kesi kufuatilia maendeleo ya kesi zao mtandaoni. Hii imesaidia kupunguza muda wa kusikiliza kesi na kuboresha uwazi.

iv) Katika kupambana na ufisadi, mwaka 2022 TAKUKURU iliwakabili maafisa wa serikali katika kesi kubwa ya ufisadi. Kwa mfano, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi alikabiliwa na mashitaka ya ubadhirifu wa fedha za umma zinazokadiria zaidi ya bilioni 2.

**a) Changamoto**

i) Aidha, kuna matukio yanayodhoofisha utawala wa sheria na utawala bora, kama vile ukamataji usiofuata sheria na kutoheshimiwa kwa amri za mahakama.

ii) Kumekua na matumizi mabaya ya sheria za uhaini, uchochezi, na zingine zimekuwa zikitumiwa kuzuia wapinzani wa kisiasa, watetezi wa haki za binadamu na wanaharakati wa kijamii. Mfano ni kukamatwa na kushtakiwa kwa wanachama wa vyama vya upinzani na wanaharakati wa haki za binadamu kwa tuhuma za uchochezi na uhaini.

iii) Ufisadi umeendelea kuwa tatizo kubwa linaloathiri utawala wa sheria. Rushwa imeendelea kuathiri upatikanaji haki katika mfumo wa mahakama, polisi, na magereza.

iv) Serikali imekuwa ikitumia sheria za usalama na amri za kimamlaka kudhibiti mikusanyiko ya amani na uhuru wa kujieleza.

v) Sheria nyingi bado hazijarekebishwa ili kuendana na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi. Hii inafanya baadhi ya sheria kuwa kandamizi na kutoendana na haki za binadamu. Mfano ni Sheria ya Habari ya 2016 ambayo imekosolewa kwa kudhibiti uhuru wa vyombo vya habari.

vi) Kutokuchuliwa hatua kwa baadhi ya watu kutoka taasisi za usalama wanaotuhumiwa kuhusika katika matukio ya kihalifu dhidi ya raia na wanaharakati, hasa matukio ya utekaji na upigaji wa raia.

## 3.2 TAMKO LA ILANI

### 3.2.1 Utawala wa Sheria

Sisi AZAKI, kupitia ilani hii, tunataka viongozi watakaochaguliwa katika chaguzi za 2024/2025 kuzingatia masuala yafuatayo **ili tuweze fikia Tanzania tuitakayo;**

a. Kuheshimu na kutii Katiba, Sheria, na Utawala Bora.

b. Kuhakikisha kuwa mamlaka na taasisi za serikali zinatii, kuheshimu, na kuzingatia sheria za nchi.

c. Kuzingatia maadili, mienendo na tabia za uwajibikaji zinazochochea taswira njema ya Taifa na maendeleo ya Taifa.

d. Kuhakikisha mchakato wa utungaji wa sheria unakuwa wa wazi na shirikishi kwa wananchi ili kupata sheria za haki na zinazokubalika kwa wananchi wote.

e. Kuwawajibisha watu wote wanaohusika katika kuvunja sheria za nchi hata kama ni miongoni mwa wanaosimamia sheria zenyewe.

f. Kuunda tume huru itakayokuwa inapokea malalamiko dhidi ya vyombo vya usalama na kuendesha uchugunzi huru.

### 3.2.2 Ukatiba na Katiba Mpya

a) Upatikanaji wa Katiba mpya inayokidhi matakwa ya wananchi, itakayolinda haki za binadamu, uwajibikaji wa umma, mgawanyo wa madaraka, maadili ya umma, mifumo ya uchaguzi, muundo wa muungano, na usimamizi wa rasilimali za Taifa.

b) Kufikia maridhiano ya kisiasa kwa kuanzisha majadiliano ya kitaifa yanayohusisha wadau wote muhimu, wakiwemo vyama vya siasa, asasi za kiraia, viongozi wa dini, na wananchi. Majadiliano haya yawe na lengo la kufikia maridhiano kuhusu mchakato wa Katiba mpya na kuhakikisha maoni ya pande zote yanasikilizwa na kuzingatiwa.

c) Serikali kuweka ratiba mahususi ya kufufua mchakato wa Katiba mpya, ikijumuisha hatua za wazi na zinazotekelezeka. Ratiba hii itangazwe kwa umma na kufuatiliwa kwa uwazi ili kuhakikisha uwajibikaji.

d) Kuweka kipaumbele kwa mchakato wa Katiba na kuhakikisha rasilimali za kutosha zinatengwa. Serikali inaweza pia kushirikiana na wahisani wa kimataifa kwa msaada wa kifedha na kiufundi.

e) Kuboresha mazingira ya uhuru wa kujieleza kwa kuhakikisha vyombo vya habari, wanaharakati wa haki za binadamu, na wananchi wanapata uhuru wa kujieleza bila vitisho au kizuizi. Hii itahakikisha mijadala ya Katiba mpya kuwa huru na maoni mbalimbali yanazingatiwa.

f) Rasimu ya Tume ya Katiba mpya maarufu kama Rasimu ya Warioba ipewe kipaumbele kuwa katiba ya Tanzania kwa kuwa ndio rasimu yenye maoni ya wananchi.

### 3.2.3 Utawala Bora na Mgawanyiko wa Madaraka

a) Kuhakikisha Tanzania inakuwa na mgawanyo wa madaraka na udhibiti wa mamlaka ili kuzuia uonevu wa madaraka kati ya mhimili mmoja dhidi ya mwingine, taasisi moja dhidi ya nyingine na baina ya mtu na mtu.

b) Serikali inayowajibika kwa umma na inayoheshimu mamlaka ya wananchi.

c) Kuhakikisha watumishi wa umma wanawajibika kwa misingi ya weledi na kwa mujibu wa sheria za nchi, bila upendeleo au mlengo wa kisiasa kwa maslahi ya watu au kundi fulani.

d) Kuweka mfumo wa utawala unaotenganisha siasa na biashara binafsi ili kuepuka mgongano wa maslahi.

e) Tunaitaka serikali kuchukua hatua madhubuti za kukomesha ubadhirifu wa fedha za umma kwa kuanzisha mfumo thabiti wa uwajibikaji na uwazi katika matumizi ya fedha za umma na kuhakikisha ripoti za CAG zinazingatiwa na hatua za kisheria zinachukuliwa haraka dhidi ya wote waliopatikana na hatia ya ubadhirifu.

f) Kuongeza uwezo wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kuipatia rasilimali zaidi na kuipa mamlaka ya kuwachukulia wabadhirifu hatua kwa kushirikiana na vyombo vya dola.

g) Kuweka sheria na taratibu zinazozuia Bunge na serikali kuingilia maamuzi ya mahakama, na kuhakikisha maamuzi ya mahakama yanatekelezwa bila upendeleo au vikwazo.

# UCHUMI JUMUISHI NA MAENDELEO ENDELEVU



SURA
YA NNE

# UCHUMI JUMUISHI NA MAENDELEO ENDELEVU

## 4.0 KUHUSU SURA HII

Sura hii inaelezea dhamira ya AZAKI juu ya uchumi jumuishi na maendeleo endelevu kwa Tanzania na Zanzibar kutoka mwaka 2024 hadi 2029. Tunatambua jitihada zilizofanyika kutoka mwaka 2020 hadi 2024 kwa utekelezaji wa ilani ya AZAKI 2019-2024, ikiwa ni pamoja na kubadilika kwa uchumi kutoka wa kipato cha chini hadi kipato cha kati, kupunguza umaskini, na kukuza usawa wa kijinsia. Hata hivyo, kipengele hiki kinabainisha changamoto zinazohitaji kushughulikiwa, kama vile upungufu wa rasilimali fedha, masuala ya utawala, uharibifu wa mazingira, na usawa katika jamii. Kujidhatiti kuboresha usimamizi wa fedha, uvumbuzi na uongezaji wa ajira, ulinzi wa kijamii, na uendelevu wa mazingira ni msingi mkuu katika upatikanaji wa maendeleo endelevu na kufikia ukuaji wa uchumi ulio kamili na jumuishi.

Madhumuni ya kipengele hiki cha ilani hii ni kuangazia hali ya maendeleo ya Taifa na uchumi pia kutoa mapendekezo juu ya mipango ya kimkakati ya kujenga ustahimilivu, kuimarisha uchumi jumuishi na kukuza maendeleo endelevu yenye usawa katika kanda zote. Kuimarisha taasisi, kuendeleza ubia kati ya sekta ya umma na binafsi, na kuwekeza katika miundombinu muhimu na elimu ili kujenga mfumo thabiti unatakaosaidia kuwa na maendeleo endelevu.

## 4.1 UTEKELEZAJI WA ILANI YA AZAKI 2019-2024

### 4.1.1 Uchumi Jumuishi

**a) Jitihada Zilizofikiwa**

i) Tanzania imeonyesha ustahimilivu na maendeleo kuelekea uchumi jumuishi licha ya changamoto za kitaifa na kimataifa. Nchi imepiga hatua kutoka uchumi wa kipato cha chini hadi kipato cha kati mwaka 2020, na kuwa miongoni mwa nchi 20 zenye uchumi unaokua kwa kasi zaidi duniani.

ii) Kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) kimekuwa wastani wa asilimia 5.2 kila mwaka na kinatarajiwa kufikia asilimia 6 ifikapo mwaka 2025. Maendeleo haya yanatokana na utekelezaji mzuri wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III), huku maboresho zaidi yakitarajiwa.

iii) Aidha, kwa kipindi cha hivi karibuni, pato la Taifa kwa kipindi cha Januari hadi Septemba 2023 limeongezeka hadi kufikia shilingi za Kitanzania trilioni 140.0 ikilinganishwa na shilingi za Kitanzania trilioni 124.2 kwa kipindi cha Januari hadi Septemba 2022, sawa na ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa asilimia 5.3, ikilinganishwa na asilimia 5.2 kwa vipindi hivyo. Kwa mujibu wa hutuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji 2024, imeeleza sekta zilizoweza kukua kwa kasi ni pamoja na fedha na bima (16.0%), uchimbaji madini na mawe (10.2%), umeme (10.0%), huduma nyingine na burudani (10.0%), malazi na chakula (8.9%), na habari na mawasiliano (6.9%). Shughuli ambazo zimechangia kiasi kikubwa katika pato la Taifa ni pamoja na kilimo (24.8%), ujenzi (13.6%), uchimbaji madini na mawe (9.7%), biashara na matengenezo (8.4%), uchukuzi na uhifadhi wa mizigo (7.2%), na viwanda (6.9%).

iv) Tanzania imeendelea kuchukua hatua za kuboresha na kuongeza ukuaji wa TEHAMA kwa kuweka mazingira wezeshi, ikiwa ni pamoja na kuwezesha wanafunzi katika ngazi ya elimu ya juu na baadhi ya shule za sekondari kujifunza kwa vitendo. Kuingiza mitaala inayolenga kuongeza ujuzi wa masuala ya TEHAMA kumeinua viwango vya ujuzi na ubunifu katika sekta ya habari na mawasiliano, hatua muhimu kuelekea uchumi wa kidigitali na ushindani katika ngazi za kikanda na kimataifa.

v) Tanzania imechukua hatua madhubuti kuelekea uchumi wa kidigitali, ikionyesha uvumbuzi na kuanzisha programu na mikakati inayohimiza matumizi ya kidijitali katika taasisi za serikali na binafsi. Mwaka 2023, matumizi bora ya mifumo ya TEHAMA yalichangia kukua kwa mauzo katika soko la bima kwa asilimia 6.8 na kufikia shilingi bilioni 1,238.5 ikilinganishhwa na bilioni 1,159.3 kwa mwaka 2022.

vi) Zanzibar imepiga hatua katika sekta mbalimbali za kiuchumi na maendeleo endelevu kupitia Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, unaosisitiza matumizi endelevu ya rasilimali za baharini na ufufuaji wa utalii. Licha ya changamoto za janga la UVIKO-19, sekta ya utalii imeonyesha dalili za kurejea tangu 2023, zikichochewa na kampeni za kukuza utalii na maboresho ya miundombinu muhimu.

vii) Uwekezaji katika uhifadhi wa baharini na mikakati endelevu ya uvuvi umelinda mazingira na pia kuleta nafasi za ajira katika sekta ya uchumi wa buluu. ZADEP, yenye kaulimbiu ya "Uchumi wa Buluu kwa Ukuaji Jumuishi na Maendeleo Endelevu," inakuza maendeleo jumuishi kwa kulenga maboresho makubwa katika afya, elimu, na huduma za kijamii. Hatua hii imeongeza uandikishaji wa watoto shuleni, kuboresha viwango vya kusoma na kuandika, na kuimarisha utoaji wa huduma za afya, hasa katika maeneo ya vijijini.

**b) Changamoto**

Utekelezaji wa Ilani ya AZAKI 2019-2024 umekumbana na changamoto mbalimbali ambazo zimeathiri ufikiaji wa malengo yaliyowekwa kwa Tanzania na Zanzibar kama ifuatavyo;

**i)** **Vikwazo vya Rasilimali na Usimamizi:** Changamoto kubwa imekuwa ni ukosefu wa rasilimali fedha na usimamizi mbaya wa rasilimali za Taifa zilizopo. Juhudi nyingi zinakumbana na vikwazo ikiwemo kukosekana kwa hatua stahiki zinazochukuliwa ili kuwawajibisha wahusika na taasisi zilizo bainika kuhusika na uharibifu au ubadhirifu wa rasilimali na fedha, kama inavyobainishwa na taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG Report). Hali hii imeathiri utekelezaji wa miradi muhimu ya maendeleo na mipango ya kijamii kwa wakati.

**ii)** **Utawala na Urasimu:** Changamoto za utawala, ikiwa ni pamoja na rushwa na urasimu, zmeendelea kuwa changamoto kubwa nchini. Licha ya mipango ya kupambana na rushwa, tatizo hili limekuwa ni endelevu na limesababisha ongezeko la gharama za miradi, ucheleweshaji, miradi isiyokidhi viwango vya ubora pamoja na huduma duni katika sekta mbalimbali. Taasisi kama ZAECA *(Zanzibar Anti-Corruption and Economic Crimes Authority)* na TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) zinahitaji kuimarishwa zaidi ili kushughulikia kesi za rushwa kwa ufanisi.

**iii)** **Ujumuishaji wa Kiuchumi na Ukuzaji wa Ajira:** Hadi kufikia 2021, Ofisi ya Takwimu (NBS) iliripoti ongezeko la ajira mpya 584,333 katika sekta ya umma na binafsi, pamoja na ongezeko hili tatizo la ajira bado linaendelea kutokana na ongezeko la wahitimu kila mwaka. Ukosefu wa ajira ni mkubwa zaidi kwa wanawake, ikiwa ni asilimia 29.7 kwa wanawake Zanzibar ikilinganishwa na asilimia 10.4 kwa wanaume, na asilimia 12.2 kwa wanawake Tanzania Bara ikilinganishwa na asilimia 5.7 kwa wanaume.

Kwa ujumla, kiwango cha ukosefu wa ajira ni asilimia 19.7 Zanzibar, asilimia 9 Tanzania Bara, na asilimia 9.3 kwa Tanzania nzima. Mwaka 2023, TAMISEMI ilitangaza ajira za ualimu na afya, ambapo jumla ya waombaji

171,916 walijitokeza, lakini ni waombaji 18,449 pekee walifanikiwa kupata ajira, ikiwakilisha asilimia 10.7 tu ya waombaji. Hali hii inaonesha ukubwa wa tatizo la ajira, hususani kwa vijana wengi wanaokosa ujuzi na uzoefu wa kuingia kwenye soko la ajira. Juhudi za kukuza na kutanua mafunzo ya ufundi na uzoefu kazini zinaendelea, lakini zinahitaji kuimarishwa zaidi ili kuwa na matokeo thabiti na mapana kwa wakati

iv) **Ujumuishaji wa Kifedha:** Juhudi za kupanua ujumuishaji wa kifedha kupitia huduma za kifedha za kidijitali na programu za elimu ya kifedha zinaendelea, lakini watu wengi, hasa katika maeneo ya vijijini, bado wanakosa fursa za kupata bidhaa na huduma za kifedha. Kuimarisha mifumo ya kifedha na kukuza elimu ya kifedha ni muhimu kuhakikisha kila mtu anashiriki na kufaidika na shughuli za kiuchumi.

v) **Kuporomoka kwa Thamani ya Sarafu:** Kuporomoka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kunaleta changamoto za ukuaji wa kiuchumi. Katika robo ya pili ya mwaka 2024, thamani ya shilingi ilishuka kwa asilimia 2.2 ikilinganishwa na asilimia 1.8 katika robo ya kwanza, na kuathiri uwezo wa ununuzi na utulivu wa kiuchumi wa nchi.

### 4.1.2. Maendeleo Endelevu

#### a) Jitihada Zilizofikiwa

i) Mikakati ya usawa wa kijinsia Tanzania Bara na Zanzibar imepiga hatua kubwa, na sera na programu zinazolenga kuongeza ushiriki wa kiuchumi wa wanawake na nafasi za maamuzi. Mikakati hii imewawezesha wanawake kwa kutoa fursa za elimu, mafunzo ya ufundi, na mikopo midogo, hivyo kuboresha hali zao za kijamii na kiuchumi.

ii) Ujenzi wa miundombinu, ikiwa ni pamoja na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba na ujenzi wa barabara na madaraja mapya, umeongeza muunganiko na kusaidia shughuli za kiuchumi.

iv) kuanzishwa miradi mipya ikijumuisha ujenzi wa reli Lot 3 (Makutupora -Tabora), Lot 4 (Tabora -Isaka), Lot 6 (Tabora - Kigoma) na Lot 7 (Uvinza - Musongati)ambazo hazikuwepo wakati wa utekelezaji wa ilani ya AZAKI 2019/2024.

v) Uboreshwaji wa miundombinu ya bandari ikiwemo kuongeza kina kufikia mita 15.5 na upana mita 200 katika lango la kuingia na kugeuza meli kwa ajili ya kupokea meli kubwa katika bandari ya Dar es Salaam. Kadhalika, utekelezaji wa ilani ya AZAKI 2019/2024 umeambatana na hatua ya ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala ambapo utekelezaji umefikia asilimia 96.0.

vi) Ukamilifu wa mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha jumla ya MW 2,115 ukiwa na takribani asilimia 37 ambapo hadi Aprili 2024 utekelezaji ulikuwa umefikia asilimia 97.43 na kuanza uzalishaji kupitia mtambo namba tisa (9) unaoingiza katika Gridi ya Taifa jumla ya MW 235 na hivyo, kuimarisha upatikanaji wa umeme.

v) Kwa upande kilimo na uhifadhi wa chakula, nchi ilikuwa na uwezo wa tani 250,000 tu sasa katika kipindi cha utekelezaji wa ilani ya AZAKI 2019-2024 tumefikia tani 500,000. Mauzo ya nje yalikuwa wastani wa dola za Marekani bilioni 1.2 leo tuna wastani wa dola za Marekani bilioni 2.3. Utoshelevu wa chakula umefikia asilimia 124 mwaka 2023/24.

**b) Changamoto**

**i) Usawa wa Kijamii:** Licha ya juhudi za kukuza usawa wa kijinsia na kijamii, tofauti bado zipo, hasa katika maeneo ya vijijini, wanawake na watu wenye ulemavu. Makundi yaliyotengwa mara nyingi hukosa fursa za elimu, huduma za afya, na nafasi za kiuchumi, hivyo kuzuia ushiriki wao katika mchakato wa maendeleo. Sheria inayolinda haki ya ajira kwa watu wenye ulemavu inayotaka taasisi au kampuni kuajiri watu watatu wenye ulemavu kati ya 20 bado haizingatiwi. Sera na mipango zaidi ya ujumuishaji zinahitajika ili kushughulikia tofauti hizi na kuhakikisha kuwa sehemu zote za jamii zinanufaika na ukuaji wa uchumi, Idadi ya watu wenye ulemavu wasio na ajira ni 4.4% kwa wanaume ikilinganishwa na 7.2% kwa wanawake (NBS 2020/2021), Maeneo ya vijijini yanakabiliwa na upungufu wa maji safi na huduma za vyoo, jambo linalochangia kuendelea kwa ugonjwa wa utapiamlo, mfano hivi sasa, asilimia 30 ya wanawake na watoto nchini Tanzania wanakabiliwa na viwango vya juu vya utapiamlo.( Ubalozi wa Marekani Tanzania 2024).

**iii) Huduma Za Kijamii:** Maboresho katika huduma za afya na kijamii yamekuwa hayalingani, hasa katika maeneo ya mbali na vijijini. Mfumo wa huduma za afya unakabiliwa na changamoto kama miundombinu duni, upungufu wa vifaa vya matibabu, na uhaba wa wataalamu wa afya. Masuala haya yanapunguza ufanisi wa afua za afya na kuchangia tofauti za huduma za kiafya zinazoendelea, Upungufu wa waalimu na madarasa bado ni tatizo hususani vijijini mfano,***Wilaya ya Mwanga ambayo ina shule za msingi 110 na jumla ya wanafunzi 24,476 wa darasa la awali hadi la saba, ina walimu 650 kati ya 1,027 wanaohitaji na hivyo kufanya upungufu uwe walimu 377.( nukuu, gazeti la mwananchi June 2024).***

iii) **Maendeleo ya Miundombinu:** Licha ya uwekezaji mkubwa katika miundombinu, bado kuna mapungufu, hasa katika uunganishaji wa vijiji. Upanuzi wa barabara, madaraja, na viwanja vya ndege umeboresha upatikanaji wa huduma, lakini maeneo mengi bado yanakosa miundombinu ya kutosha kusaidia shughuli za kiuchumi na huduma za kijamii. Uwekezaji endelevu na matengenezo yanahitajika ili kuziba mapungufu haya na kusaidia kuleta maendeleo endelevu na uchumi jumuishi wa Watanzania

iv) **Teknolojia na Mawasiliano:** Kumekuwa na ushindani mkubwa katika soko la ajira ambapo ajira na fursa nyingi zimeendelea kujitokeza katika sekta ya TEHAMA. Hali hii inapelekea vijana wengi kushindwa kuhusika kwa kukosa msingi bora wa ujuzi. Pia, katika kuelekea uchumi wa kidigitali, taasisi nyingi za serikali na binafsi bado hazina mifumo rafiki ya kuingia katika soko la ushindani. Mwaka 2023, matumizi bora ya mifumo ya TEHAMA yalichangia kukua kwa mauzo katika soko la bima kwa asilimia 6.8 na kufikia shilingi bilioni 1,238.5 ikilinganishwa na bilioni 1,159.3 kwa mwaka 2022.

### 4.1.3 Mazingira na Mabadiliko ya Tabia nchi

#### a) Jitihada Zilizofikiwa

i) Jitihada za kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi zimeimarishwa na Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Zanzibar, ambao unalenga kujenga ustahimilivu na kutekeleza hatua za kulinda jamii na mifumo ya ikolojia.

ii) Katika utekelezaji wa ilani ya AZAKI 2019-2024, Serikali imezindua Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034) ikiwa ni moja ya hatua za awali za kitaifa za utekelezaji wa programu hiyo wenye kulenga kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa watanzania kwa kuimarisha upatikanaji wa malighafi na miundombinu 57 ya uhakika ya nishati safi ya kupikia.

iii) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021-2026) na Mpango wa Taifa wa Hifadhi ya Mazingira (2022-2032) Tanzania ina takribani hekta milioni 48.1 za rasilimali za misitu, sawa na asilimia 55 ya ardhi yote ya Tanzania Bara ambayo ikitumika vizuri kupitia miradi ya biashara ya kaboni ni suluhisho muhimu la kupunguza kasi ya uharibifu na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa.

iv) Aidha, kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kutekeleza Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi Zanzibar (2014-2030) ambao unatekelezwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais yenye dhamani ya mazingira kupitia Mpango huu Kwa mwaka wa fedha 2023/24 Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar imetenga fedha jumla ya shilingi milioni 650 kwa ajili ya tathmini ya awali ili kufanya usanifu wa miundombinu itakayosaidia kurudisha fukwe katika hali yake.

v) Mikakati hii imeendelea kuwa muhimu katika kuamsha hali ya wadau na jamii kushiriki katika afua na mipango mbalimbali yenye malengo ya kuleta, kuendeleza na kukuza ustahimilivu juu ya suala la mabadiliko ya tabia nchi, ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Mwongozo wa biashara ya hewa ukaa Tanzania, (National Carbon Trade Guidelines 2022), ambapo hadi sasa baadhi ya jamii (Wilaya ya Tanganyika Katavi), wamefanikiwa kukusanya jumla ya mapato ya shilingi za Kitanzania bilioni 22 na wanakijiji Wilaya na namtumbo kupata takribani shilingi milioni 200 za Kitanzania 2024.

vi) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara na Wadau wote wenye dhamana iliandaa Mpango wa Taifa wa Dharura wa El Nino na hatua ya matarajio Agosti, 2023 ambao umechangia kupunguza athari za mvua hizo.

vii) Serikali imeanzisha Shahada katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kuhusu masuala ya Hali ya Hewa na Mabadiliko ya Tabianchi, kusaidia kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu nchini hasa kwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

### a) Changamoto

### i) Ukataji Miti

Takribani hekta milioni 48.1 ni eneo la misitu lakini pamoja na hayo takribani hekta 469,420 hupotea kila mwaka kwa sababu ya shughuli za kilimo, makazi, shughuli nyingine za kijamii ikiwemo biashara ya mkaa.

Hadi kufikia mwaka 2015, inakadiriwa kuwa tani milioni 52 za mkaa huzalishwa kwa mwaka duniani, na tani 32.4 huzalishwa Afrika, huku Tanzania ikiongoza Afrika Mashariki na kuwa miongoni mwa nchi saba zinazozalisha mkaa kwa wingi duniani, ikipoteza takribani ekari 150,433 za misitu kila mwaka kwa shughuli hii. Asilimia 71.2 ya wananchi wa Tanzania wanategemea kuni, asilimia 37 wanatumia mkaa, na asilimia 5 wanatumia mafuta ya taa. Inakadiliwa kuwa Dola 350 milioni za Marekani hukusanywa kama mapato ya uuzaji wa mkaa kwa Dar es Salaam pekee, huku mauzo ya kahawa yakifikia Dola milioni 60 tu.

Hii inaonesha kiasi kikubwa cha miti inayopotea, hali inayopelekea mabadiliko ya tabianchi na athari zake, ikiwemo ongezeko la hewa ya ukaa ambayo huchangia kuongezeka kwa joto ikikadiriwa kuwa hadi mwaka 2080, joto hapa nchini litakuwa limeongezeka kati ya nyuzi joto 1.40C hadi 3.60C na kupungua kwa mvua hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi zikiwemo kilimo, ufugaji na uvuvi.

### ii) Athari zitokanazo na miradi ya maendeleo na uhifadhi

Miradi mingi ya maendeleo inaendelea kuwa changamoto kubwa kwa jamii ya Kitanzania, ambapo utekelezaji wake umekuwa ukiacha athari za kimazingira na athari za moja kwa moja katika jamii, ikiwemo kuhamishwa makazi ya kudumu kwa lazima na kutokupata stahiki zao kwa wakati, hali hii inadhihirika katika maeneo kama Ngorongoro, Loliondo, na Msomera, pia maeneo yanayotekeza miradi mikubwa ya uchimbaji madini,  kama Geita, Kahama, Mara na kwingineko, migogoro baina ya wawekezaji, serikali na wanachi imeendelea kuathiri shughuli za kimaendeleo hususani kwa jamii husika. Athari zingine ni pamoja na uchafuzi wa mazingira na madhara ya kiafya kwa viumbe hai.

### iii) Maporomoko ya Ardhi na Mafuriko

Tanzania na Zanzibar zinaendelea kukumbwa na majanga makubwa ya mafuriko na maporomoko ya Ardhi, Hii inadhihirika kwa baadhi ya matukio yaliyotokea hivi karibuni ikihusisha maporomoko makubwa ya ardhi wilaya ya Hanang'i, yaliyopelekea kupoteza maisha ya watanzania wengi, hali ya mafuriko makubwa pia imedhihirika katika eneo la Rufiji Pwani, Dar es Salaam,  Mwanza ,Kigoma baadhi ya mikoa ambako watu wameendelea kupoteza Maisha, Mali, na kuharibika kwa miundombinu

Katika Taarifa ya Waziri Mkuu April 25 2024, ilionesha yakuwa Watu 155 wamepoteza maisha na wengine zaidi ya 230 kujeruhiwa nchini Tanzania kutokana na mvua kubwa zilizoendelea kunyesha kwa kipindi hicho. Aidha takribani watu 200,000 na zaidi ya kaya 51,000 zimeathirika huku miundombinu mbalimbali ikiharibika.

Alieleza pia kuwa zaidi ya nyumba 10,000 sambamba barabara na reli nazo zimeathirika

Mwezi Oktoba hadi Desemba, 2023 kumekuwa na ongezeko kubwa la mvua ambapo jumla ya mililita 534.5 zilipimwa ikilinganishwa na mililita 227.2 kwa mwaka 2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia 135. Hali hii inayopelekea, kupotea kwa nguvu kazi, kuharibika kwa miundombinu na kuchelewa kwa maendeleo huku waathirika wengi wakiwa ni akina mama, watoto, wazee na watu wenye ulemavu.

### iv) Kuongezeka kwa kina cha bahari na maziwa makuu

Wiziri wa Mazingira mwezi Mei 2024 aliripoti yakuwa, utafiti na vipimo vilivyopo katika maji ya Bahari ya Hindi katika pwani ya Dar es Salaam unaeleza kuwa maji yanaongezeka kwa wastani wa kiasi cha milimita 6 kwa mwaka tangu mwaka 2002.Kwa upande wa Zanzibar na pwani yote ya bahari ya hindi ,Hali hiyo hupelekea upotevu wa bioanuwai muhimu ikiwemo mikoko na nyasi bahari ambavyo ni sehemu ya hifadhi ya mazingira.

Madhara mengine ni kupotea kwa ardhi na kuwaacha wananchi bila ya makazi na kushindwa kufanya shughuli za kilimo kutokana na changamoto ya kuongezeka kwa kiwango cha bahari.Visima vya maji baridi mbali na kuingiwa na maji ya chumvi pia miundombinu ikiwemo barabara, gati za bandari na majengo hubomolewa na maji hayo, Hali hii ya madhara hulikumbuka pia ziwa Tanganyika na kupelekea baadhi ya shughuli za kijamii kuathirika, ikiwemo kilimo na uvuvi.

### v) Ufadhili, Mikakati na Utekelezaji Duni

Hadi 2023 ripoti ya kidunia inaonyesha kuwa fedha zinazohitajika kukabiliana na hali ya mabadiliko ya tabianchi katika nchi zinazoendelea ni nyingi zaidi ,zinazokadiriwa kuwa dola za Marekani kati ya bilioni 215 na bilioni 387 kwa mwaka katika muongo huu, Changamoto hii bado inaikumba Tanzania pia ambapo kiasi kikubwa cha shughuli za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hakina ufadhili na fedha za kutosha, Taasisi nyingi hususani AZAKI Zimekuwa mstari wa mbele kujitolea katika shughuli hizi pasipo na bajeti maalumu.

### vi) Madhara ya Kiafya

Ndani ya utekelezaji wa ilani ya AZAKI 2019-2024, Matukio ya mabadiliko ya tabianchi yanayopelekea kuharibika kwa miundombinu na kutapakaa kwa taka yameendelea kushamiri, hali imepelekea kuendelea kwa uibukaji wa magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu, ambapo inakadiriwa kuwa jumla ya watanzania 58, mwezi Januari walipata ugonjwa huu mkoani Mwanza pekee.

### vii) Madhara ya Maendeleo ya Elimu

Matukio Mabadiliko ya tabianchi yameendelea kuathiri shughuli za kimaendeleo ikiwemo elimu, ambapo baadhi ya shule wanafunzi wamekuwa wakishindwa kufika kwa wakati na hata kuhatarisha maisha yao wanapokuwa njiani, baadhi ya matukio yamepelekea athari za moja

kwa moja ikiwemo kubomoka kwa vyumba vya madarasa hali inayopelekea maendeleo ya elimu kudhorota. Hali hii hatarishi inadhihirika kwa katazo la Waziri wa elimu Aprili 25, 2024 kwa lililo zuia wanafunzi kwenda shule mara zinyeshapo nvua kubwa.

**viii) Ukame uliokithiri**

Licha ya kuwepo kwa mvua kubwa na zilizopitiliza, suala la ukosefu wa mvua kwa baadhi ya maeneo limeendelea kuwa changamoto kubwa na kupelekea kuathiri shughuli za kiuchumi na maendeleo ikiwemo kilimo, mnamo mwaka 2023, wakazi wa vijiji viwili vya Mwanamanimba na Mwamatiga Wilayani Meatu Mkoa wa Simiyu walipoteza takribani ekari 100 zilizoungua kwa jua, hali iliyopelekea kuathirika kiuchumi, pia wilayani Simanjiro jumla ya mifugo 62,500 ilikufa kwa kukosa malisho na maji kutokana na ukame uliopitiliza.

**ix) Usalama wa Chakula**

Matukio ya mabadiliko ya tabianchi nchi kwa ujumla wake, ikiwemo joto kali kupitiliza, ukame, mafuriko, maporomoko na mmomonyoko wa ardhi, mlipuko wa magonjwa ya mimea na uharibifu wa miundombinu ya mashambani na usafirishaji, yameendelea kuwa hatarishi katika suala la usalama wa chakula katika baadhi ya nchi, ikiwemo Tanzania na nchi Jirani.

**X) Uzalishaji Taka**

Uzalishaji wa Taka Tanzania hususani taka ngumu umeendelea kuwa changamoto kubwa, athari zake zimeendelea kuathiri maisha ya viumbe wote kwa kupunguza ubora wa ardhi kwa shughuli za kilimo, Kuathiri mifumo ya kiiolojia na kuchafua maeneo ya fukwe za Bahari na Maziwa,Mfano, Jiji la Dar es Salaam linakadiriwa kuzalisha zaidi ya tani 4,600 za taka kwa siku. Kati ya hizo ni asilimia 45 hadi 50 tu zinazopokelewa katika dampo sawa na tani 1,200 – 2,000 ya taka zinazokisiwa kuzalishwa kwa siku ambapo taka zinazobaki huishia kwenye maeneo ya wazi, majini, barabara na makazi.

## 4.2 TAMKO LA ILANI

Sisi, AZAKI, tunahitaji viongozi na serikali ijayo kuzingatia mapendekezo yafuatayo ili kuendeleza, kuongeza na kuimarisha maendeleo endelevu, kujenga uchumi imara na jumuishi, pamoja na kudhibiti changamoto za kimazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa masilahi mapana ya wananchi kupitia AZAKI kama ifuatavyo;

#### 4.2.1.Tamko kuhusu Maendeleo Endelevu

a) Kuhimiza na kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama na huduma bora za usafi wa mazingira.

b) Uwekezaji katika huduma za afya na kijamii ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma hizi kwa wote bila ubaguzi.

c) Serikali itakayowekeza katika teknolojia na mawasiliano kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa na miundombinu bora ya TEHAMA, kuimarisha elimu ya kidijitali, na kukuza ubunifu

d) Kufanya uwekezaji endelevu katika miundombinu muhimu kama barabara, madaraja, na viwanja vya ndege, ni muhimu katika kusaidia shughuli za kiuchumi na kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu.

e) Kuzingatia uunganishaji wa vijijini ili kuhakikisha kuwa ukuaji wa kiuchumi unanufaisha mikoa yote kwa usawa.

f) Serikali kufanya upanuzi wa miundombinu ya kidigitali ili kuboresha uunganishaji na kukuza huduma za kifedha za kidigitali. Kuimarisha programu za uelewa wa kifedha kutahakikisha kwamba watu wote wanaweza kushiriki na kufaidika na shughuli za kiuchumi.

g) Kuboresha uwekezaji katika miundombinu ya afya, vifaa vya matibabu, na mafunzo kwa wataalamu wa afya ili kuboresha upatikanaji wa huduma za afya. Kushughulikia tofauti za huduma za kiafya, hasa katika maeneo ya vijijini na yaliyotengwa, kuhakikisha matokeo bora ya kiafya yenye usawa kwa wote.

h) Kuongeza ubora wa elimu na kupanua upatikanaji wake ili kuhakikisha kwamba watoto wote wanapata elimu bora na kwa usawa.

i) Serikali itakayoweza kuja na mikakati dhabiti ya kutatua tatizo la ajira nchini kwa kutumia vyema rasilimali na ujuzi wa ndani kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za kimaendeleo ndani na nje ya Tanzania. Hii ni pamoja na kuweka kipaumbele kwa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu ili kupelekea Tanzania tuitakayo ya maendeleo endelevu na uchumi jumuishi.

j) Kuisimamia serikali kuimarisha michakato ya utoaji huduma kwa ili kuharakisha maamuzi na kuboresha utoaji wa huduma katika sekta zote.

#### 4.2.2.Tamko Kuhusu Uchumi Jumuishi

a) Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha ili kuhakikisha ugawaji na matumizi ya rasilimali kwa wakati na kwa ufanisi. Pia, kukuza na kutekeleza mifumo madhubuti ya kupambana na usimamizi mbaya wa fedha na

ufisadi, na hivyo kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma.

b) Kuongeza mafunzo ya ufundi na programu za kukuza ujuzi ili kuwapa nguvu wafanyakazi, hasa vijana, kukabiliana na mahitaji ya uchumi ya kisasa.

c) Kuendeleza ujasiriamali na kusaidia biashara ndogo na za kati (SMEs) kwa kuboresha upatikanaji wa fedha na kupunguza vikwazo vya kiuchumi.

d) Kuendeleza na kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi ili kutoa fursa endelevu za ajira na kuchochea ukuaji wa kiuchumi.

e) Kuweka vipaumbele vya upanuzi wa programu za ulinzi wa kijamii ili kulinda makundi hatarishi dhidi ya mitikisiko ya kiuchumi na kuboresha ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi.

f) Kuimarisha sera na programu zinazolenga kufikia usawa wa kijinsia, kuhakikisha wanawake na makundi yaliyo pembezoni wanafikiwa na huduma za elimu, afya, na fursa za kiuchumi.

g) Kuimarisha uwezo wa taasisi kama ZAECA na TAKUKURU ili kushughulikia ufisadi na kudumisha sheria zinazolinda uchumi kwa maendeleo ya Taifa.

h) Kukuza utawala jumuishi kwa kuhakikisha michakato ya maamuzi inayoshirikisha wadau wote, ikiwa ni pamoja na AZAKI.

i) Kuja na sera wezeshi zitakazoweka mbele vipaumbele vya vijana na makundi maalum ikiwemo kuongeza upatikanaji mikopo yenye riba nafuu na elimu ya biashara kwa wahusika.

j) Kuongeza na kukuza uzalishaji kwa bidhaa za viwanda, kukuza soko la uingizaji na utoaji wa bidhaa nchini( import & export market) pamoja na kupunguza viwango vya kodi ili kuvutia wawekezaji na uendelevu wa biashara nchini hali itakayo kuza uchumi wa Taifa na kuongeza ajira hususani kwa vijana

k) Kubuni mikakati thabiti na kuweka Mazingira wezeshi wa vijana kupata ujuzi na kujiajiri wenyewe katika sekta mbalimbali kama kilimo, ufugaji, ufundi na ujasiriamali ili kupunguza mzigo kwa serikali.

l) Viongozi wa Kisiasa kukuza nafasi ya ushiriki wa wataalamu wa uchumi na kada mbalimbali katika maamuzi yanayolenga kupata hatima ya maendeleo ya kiuchumi nchini pia kuongeza ushiriki wa vijana katika kuongoza bodi mbalimbali za taasisi za umma.

m) Kuhimiza jitihada za serikali na ufanisi wa utekelezaji wake katika kukuza teknolojia na ili kukuza ushindani katika Uchumi wa kidigitali.

n) Viongozi wajao kufikiria namna bora ya kupunguza wingi wa idara za serikali ili kuweza kuwa na matumizi bora ya rasilimali za Taifa bila ya kuathiri shughuli zingine za kimaendeleo.

### 4.2.3 Tamko kuhusu Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi

a) Kuongeza mikakati ya kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na kukuza matumizi ya vyanzo vya nishati mbadala.

b) Kuendeleza na kutekeleza mipango kamilifu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kujenga ustahimilivu wa jamii dhidi ya athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi.

c) Kusimamia na kutatua migogoro ya kimazingira ili kuleta hali ya usawa na haki katika jamii yetu.

d) Ni muhimu kuongeza juhudi za kuhifadhi mazingira, ikiwa ni pamoja na upandaji miti, ulinzi wa vyanzo vya maji, na uhifadhi wa bioanuwai.

e) Kukuza kilimo endelevu na uhifadhi wa baharini ni muhimu ili kuokoa rasilimali asili na kuhakikisha usalama wa chakula.

f) Kubuni hatua stahiki na za haraka zinazohitajika ili kuimarisha ustahimilivu wa jamii na kupunguza athari za mabadiliko haya kwa mazingira na maisha ya watu.

g) Kuongeza juhudi za ushirikishaji wa wadau wa ndani na nje ili kuweza kupata rasilimali za kutosha kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi.

h) Kukuza nafasi ya wanajamii na taasisi zao katika kutathimi na kuamua masuala yote ya kimazingira yanayogusa Maisha yao, ikiwemo miradi inayofanyika katika maeneo yao na mikakati inayopangwa kwa ajili ya ustahimilivu na ustawi wao katika Mazingira.

i) Kubuni miradi mbalimbali ndani ya Jiji itakayohusisha wadau mbalimbali inayolenga urejelezaji taka pamoja na masoko ya uhakika ya taka zilizorejelezwa au bidhaa zilizotokana na taka rejea pamoja na usimamizi bora wa sheria na kanuni za Mazingira nchini.

j) Kuhimiza na kuwezesha mipango ya utoaji elimu kwa jamii juu ya athari ya mabadiliko ya tabia nchi zinatokanazo na shughuli zote za binadamu pamoja na mikakati dhabiti ya kukabiliana na changamoto hizo.

# RUSHWA, UWAJIBIKAJI NA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UMMA



SURA
YA TANO

# RUSHWA, UWAJIBIKAJI NA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UMMA

## 5.0 KUHUSU SURA HII

Sura hii inaelezea mambo ambayo asasi za kiraia zinatarajia kuyaona katika "Tanzania Tuitakayo". Sura hii inatoa uchambuzi wa kina wa masuala ya rushwa, uwajibikaji, na usimamizi wa rasilimali za umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha miaka 2020/2021 hadi 2023/2024. Sura hii imejikita katika kutathmini jitihada za serikali katika kupambana na rushwa, kuimarisha uwajibikaji, na kuboresha usimamizi wa mali ya umma. Taarifa zilizotumika katika Sura hii zimetokana na vyanzo mbalimbali vya kuaminika, ikiwa ni pamoja na ripoti za mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za Tanzania na Tanzania - Zanzibar, taarifa rasmi za utendaji kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), pamoja na tafiti huru zilizofanywa na Asasi za Kiraia (AZAKI).

Sura hii inaangazia mafanikio yaliyopatikana, changamoto zinazoendelea kuikabili nchi, na kutoa mapendekezo ya kisera yenye lengo la kuimarisha jitihada za kupambana na rushwa, kuongeza uwajibikaji, na kuboresha usimamizi wa rasilimali za umma. Sura hii inatoa mwanga kuhusu athari za rushwa katika sekta mbalimbali za umma na binafsi, ufanisi wa mikakati ya sasa ya kupambana na rushwa, na umuhimu wa ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia rasilimali za Taifa. Aidha, sura hii inachambua kwa makini jitihada za Tanzania katika kutekeleza malengo ya Mpango wa Taifa wa Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi, pamoja na ahadi za kimataifa zilizotolewa katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Rushwa (UNCAC).

## 5.1 UTEKELEZAJI WA HOJA ZA ILANI YA AZAKI YA MWAKA 2019-2024

### 5.1.1 Rushwa na Uwajibikaji

**a) Jitihada Zilizofikiwa**

i. TAKUKURU imepokea jumla ya malalamiko 38,750 yanayohusiana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Kati ya malalamiko hayo, TAKUKURU imefanikiwa kuchunguza na kufikisha kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) jumla ya kesi 2,315, sawa na asilimia 5.97 ya malalamiko yote yaliyopokelewa. Hii inaonyesha kuongezeka kwa kasi ya uchunguzi na ufikishaji wa watuhumiwa mahakamani ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Aidha, kupitia jitihada zake za kuzuia na kupambana na rushwa, TAKUKURU imefanikiwa kuokoa jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 54.8 ambazo zingeweza kupotea kutokana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi.

ii. Kuanzishwa kwa kitengo maalum cha uchunguzi wa makosa ya kimtandao mwaka 2021. Kupitia kitengo hiki, TAKUKURU imeweza kufuatilia na kuchunguza kwa ufanisi zaidi vitendo vya rushwa vinavyofanyika kupitia mitandao ya kijamii, benki za mtandaoni, na mifumo mingine ya kielektroniki. Hatua hii inaonyesha uwezo wa TAKUKURU wa kubadilika na kukabiliana na changamoto mpya za kiuchumi na kiteknolojia zinazojitokeza katika mapambano dhidi ya rushwa.

iii. Kwa upande wa Zanzibar, ZAECA imetekeleza jumla ya kampeni 450 za elimu kwa umma kuhusu madhara ya rushwa na umuhimu wa kupambana nayo. Lengo la kampeni hizi ni kuongeza uelewa wa jamii kuhusu athari za rushwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na kuwajengea wananchi uwezo wa kutambua na kupinga vitendo vya rushwa.

iv. Katika jitihada za kuimarisha utawala bora na kupunguza mianya ya rushwa katika utumishi wa umma, ZAECA imeanzisha kamati za uhakiki wa wafanyakazi wa serikali katika wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hatua hii imesaidia kubaini na kushughulikia matukio ya watumishi hewa, udanganyifu katika sifa za kitaaluma, na vitendo vingine vya rushwa katika utumishi wa umma.

v. ZAECA imefanikiwa kuokoa jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 5.7 katika kipindi cha 2020/2021 hadi 2023/2024. Fedha hizi ni sehemu ya mali ya umma ambayo ingeweza kupotea kupitia vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi.

### b) Changamoto za Kupambana na Rushwa - Tanzania

i. Mojawapo ya vikwazo vikubwa ni ukosefu wa rasilimali za kutosha katika vyombo vya kupambana na rushwa, hususan TAKUKURU. Hii inajumuisha uhaba wa wataalamu wenye ujuzi wa juu katika uchunguzi wa makosa ya rushwa yanayohusisha teknolojia ya kisasa na miamala ya kifedha ya kimataifa.

ii. Aidha, utegemezi wa teknolojia kutoka nje ya nchi unazorotesha uchunguzi wa kesi ngumu za rushwa.

iii. Changamoto nyingine ni ushirikiano mdogo kati ya taasisi za serikali katika kubadilishana taarifa muhimu, jambo ambalo linapunguza ufanisi wa uchunguzi. Pia, kushindwa kutekeleza vizuri kwa sheria madhubuti za ulinzi wa watoa taarifa (whistleblowers) kunaathiri upatikanaji wa ushahidi wa uhalifu wa rushwa.

iv. Mfumo wa kisheria pia una changamoto zake. Mchakato wa kushughulikia kesi za rushwa mara nyingi ni wa polepole na wenye urasimu mkubwa, hali inayoweza kusababisha uchakavu wa ushahidi au kupotea kwa mashahidi muhimu.

v. Vilevile, adhabu zilizopo kwa makosa ya rushwa hazitoshi kutoa tahadhari ya kutosha. Katika ngazi ya jamii, kuna changamoto ya mtazamo wa wananchi kuhusu rushwa, ambapo baadhi wanaiona kama njia ya kawaida ya kupata huduma au fursa. Elimu ya umma kuhusu madhara ya rushwa bado haijasambaa vya kutosha, hasa katika maeneo ya vijijini.

vi. Sekta binafsi pia inachangia katika changamoto za kupambana na rushwa. Baadhi ya makampuni yanatoa vishawishi kwa watumishi wa umma ili kupata mikataba au huduma kinyume cha sheria. Aidha, kukosekana kwa mifumo madhubuti ya uwajibikaji katika sekta ya binafsi kunaruhusu vitendo vya rushwa kustawi. Jitihada za kupambana na rushwa mara nyingi zinalenga zaidi sekta ya umma, hivyo kuacha pengo katika kushughulikia rushwa katika sekta binafsi. Changamoto hizi zinahitaji mkakati jumuishi na wa muda mrefu ili kukabiliana nazo kwa ufanisi.

vii. Moja ya vikwazo vikuu ni udhaifu wa kitaasisi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA). Taasisi hii inakabiliwa na upungufu mkubwa wa rasilimali watu na fedha, hali inayoathiri uwezo wake wa kufanya uchunguzi wa kina na wa kitaalam katika kesi ngumu za rushwa. Ukosefu wa teknolojia ya kisasa na mifumo ya kidijitali ya kusimamia kesi pia unapunguza ufanisi wa taasisi hii katika kupambana na rushwa.

viii. Ukosefu wa ushirikiano wa kutosha kati ya taasisi za serikali katika kubadilishana taarifa muhimu. Hii inaathiri uwezo wa kufuatilia miamala ya kifedha inayohusishwa na rushwa, hasa katika sekta nyeti kama vile utalii na

uwekezaji wa kigeni. Vilevile, kukosekana kwa sheria madhubuti za kulinda watoa taarifa (whistleblowers) kwa upande wa Zanzibar kunarudisha nyuma juhudi za kupata ushahidi wa vitendo vya rushwa.

ix. Watanzania wengi na wanasiasa wana imani potofu kuhusu rushwa wakati wa uchaguzi. Wengi wanaamini wakati wa uchaguzi ni wakati wa mavuno na kupelekea suala la rushwa wakati wa uchaguzi kuwa kubwa sana. Wanasiasa nao hujiandaa kutoa rushwa wakati wa uchaguzi ili waweze kuchaguliwa kitu ambacho ni kinyume na sheria.

### 5.1.2 Uwajibikaji kwa Jamii (Corporate Social Responsibility) - Tanzania

#### a. Jitihada Zilizofikiwa

i) Tanzania imeshuhudia maendeleo muhimu katika utekelezaji wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2024. Takwimu rasmi zinaonesha kuwa kiasi cha TZS 52,345,678,901.23 kimetumika katika shughuli mbalimbali za CSR katika kipindi hiki. Fedha hizi zimeelekezwa katika miradi ya maendeleo inayogusa sekta muhimu kama vile elimu, afya, miundombinu, na upatikanaji wa maji safi na salama. Maeneo yaliyonufaika zaidi ni Halmashauri 28 zinazozunguka migodi mikubwa, jambo linaloonesha msisitizo uliowekwa katika kuhakikisha jamii zinazozunguka maeneo ya uchimbaji madini zinanufaika moja kwa moja na rasilimali zilizopo katika maeneo yao.

ii) Kuanzisha mfuko wa Maendeleo ya Jamii mwaka 2022 kupitia marekebisho ya sheria ya madini. Mfuko huu umekuwa chombo muhimu cha kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ya CSR, hususan katika sekta ya madini. Uanzishwaji wa mfuko huu umeongeza uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za CSR, na umesaidia kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa inakidhi mahitaji halisi ya jamii husika. Aidha, mfuko huu umetoa mwongozo wa kisera na kisheria kwa makampuni ya madini katika kutekeleza majukumu yao ya kijamii.

#### b. Changamoto

i. **Ukosefu wa Mfumo Madhubuti**: Sheria mpya ya madini (2022) ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, lakini sekta nyingine bado haina sheria nzuri. Kwa upande wa Zanzibar, ingawa Mfuko wa Maendeleo ya Utalii umeanzishwa mwaka 2023, sekta nyingine muhimu za uchumi wa Zanzibar hazina sheria nzuri za CSR.Hii husababisha viwango vya chini vya uwekezaji katika CSR na ukosefu wa vigezo vya kupima ufanisi wa miradi. Changamoto nyingine ni uratibu dhaifu kati ya serikali, makampuni, na jamii, ikisababisha miradi isiyokidhi mahitaji halisi.

ii. **Ugawaji Usio Sawa**: Maeneo yenye rasilimali za madini yanafaidika zaidi, huku maeneo mengine yakikosa maendeleo. Kwa upande wa Zanzibar,

maeneo ya mijini na vivutio vya utalii yanapata faida zaidi kuliko maeneo ya vijijini, hali inayochangia tofauti za kimaendeleo.

iii. **Uelewa na Ujuzi Mdogo**: Jamii na baadhi ya watendaji wa serikali hawana uelewa mzuri kuhusu CSR, na kusababisha matarajio yasiyokuwa ya uhalisia na migogoro. Ukosefu wa ujuzi katika usimamizi wa miradi ya CSR unaathiri ubora na uendelevu wa miradi. Hakuna mfumo wa kitaifa wa kufuatilia na kutathmini miradi ya CSR, hivyo inakuwa vigumu kupima athari za jumla za CSR.

#### 5.1.3 Usimamizi wa Rasilimali za Umma

#### a. Jitihada Zilizofikiwa

i) Katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni, Tanzania imeshuhudia maboresho ya kuridhisha katika usimamizi wa rasilimali za umma. Ukusanyaji wa mapato ya ndani umeonesha mwenendo wa kuridhisha, ambapo kulikuwa na ongezeko la asilimia 22 kutoka Shilingi za Kitanzania trilioni 17.5 katika mwaka wa fedha 2020/21 hadi kufikia Shilingi trilioni 21.3 katika mwaka wa fedha 2022/23. Mafanikio haya yanachangiwa na uboreshaji wa mifumo ya ukusanyaji mapato, pamoja na kuimarishwa kwa usimamizi wa kodi. Sambamba na hayo, kumekuwa na kupungua kwa matumizi yasiyofuata taratibu za fedha za umma, ambapo yameshuka kutoka asilimia 3.2 ya bajeti katika mwaka wa fedha 2020/21 hadi asilimia 1.8 katika mwaka wa fedha 2022/23. Maboresho haya yanaashiria kuimarika kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na uwajibikaji katika taasisi za serikali

ii) Utekelezaji wa miradi ya maendeleo nao umeshuhudia ongezeko la kiwango cha utekelezaji kutoka asilimia 71 mwaka wa fedha 2020/21 hadi asilimia 84 katika mwaka wa fedha 2022/23. Hii inaonesha kuboreshwa kwa usimamizi wa miradi na matumizi yenye tija ya rasilimali za umma katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

iii) Kuanzishwa kwa Tume ya Madini mwaka 2019 kumechangia pakubwa katika kuboresha usimamizi wa sekta ya madini nchini. Matokeo yake, kumekuwa na ongezeko la mapato ya serikali kutoka sekta hii muhimu, ambapo jumla ya Shilingi trilioni 2.1 zimekusanywa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2019 hadi 2024.

iv) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepiga hatua muhimu katika kuboresha usimamizi wa rasilimali za umma katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni. Moja ya mafanikio makubwa ni kuimarika kwa udhibiti wa ndani, ambapo ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) inaonyesha kupungua kwa hoja za ukaguzi kutoka 245 mwaka wa fedha 2020/2021

hadi 178 katika mwaka wa fedha 2022/2023. Hii inaashiria ongezeko la uwajibikaji na usimamizi bora wa fedha za umma. Aidha, Zanzibar imeshuhudia ongezeko la kuvutia katika mapato ya sekta ya utalii, ambapo mapato yameongezeka kutoka shilingi bilioni 38.8 mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 162.5 mwaka 2022/2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia 318.8.

v) Juhudi za kuboresha usimamizi wa deni la Taifa zimezaa matunda, ambapo uwiano wa deni kwa Pato la Taifa umepungua kutoka asilimia 62 mwaka 2020/2021 hadi asilimia 58 mwaka 2022/2023. Hii inadhihirisha usimamizi bora wa mikopo na matumizi ya fedha za umma. Vilevile, uanzishwaji wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi mwaka 2020 umechangia katika kusimamia kwa ufanisi rasilimali za bahari, huku ukiimarisha sekta ya uvuvi na kukuza ajira. Hatua hii imesaidia katika kuongeza thamani ya rasilimali za bahari na kuboresha maisha ya wananchi wanaotegemea sekta hii.

vi) Mafanikio mengine yanajumuisha kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA) mwaka 2021. Taasisi hii imekuwa na mchango mkubwa katika kusimamia utafutaji wa mafuta na gesi asilia, huku ikihakikisha kuwa manufaa ya rasilimali hizi yanawanufaisha wazanzibari. Pia, kukamilika kwa tafiti za awali za utafutaji mafuta mwaka 2023 kumetoa matumaini ya kuimarika zaidi kwa uchumi wa visiwa hivi. Juhudi hizi zote zinaonyesha dhamira ya dhati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuboresha usimamizi wa rasilimali za umma na kukuza uchumi kwa manufaa ya wananchi wake.

### b. Changamoto

i. Moja ya changamoto kuu ni ukosefu wa uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zimeendelea kuonesha matumizi yasiyofuata taratibu, hususan katika sekta za afya, elimu, na miundombinu. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2022/2023, CAG alibaini matumizi yasiyoidhinishwa ya zaidi ya shilingi bilioni 200 katika wizara na idara mbalimbali za serikali. Aidha, usimamizi duni wa mikataba ya serikali umesababisha hasara kubwa ya fedha za umma, ambapo baadhi ya miradi haikukamilika kwa wakati au haikufikia viwango vinavyotakiwa.

ii. Changamoto nyingine ni udhaifu katika mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya serikali. Licha ya jitihada za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuboresha ukusanyaji wa kodi, bado kuna upotevu mkubwa wa mapato kutokana na ukwepaji kodi, hususan katika sekta isiyo rasmi. Pia, usimamizi wa mali za serikali umekuwa na changamoto, ambapo baadhi ya mali hazijasajiliwa ipasavyo au zimechukuliwa na watu binafsi bila kufuata taratibu. Katika

sekta ya madini, licha ya kuanzishwa kwa Tume ya Madini, bado kuna changamoto za kudhibiti uchimbaji haramu mifumo ya kuhakikisha serikali inapata gawio lake stahiki kutoka katika rasilimali hizi.

iii. Usimamizi wa mashirika ya umma umekuwa na changamoto za kiutendaji na kifedha. Baadhi ya mashirika yameendelea kutegemea ruzuku za serikali badala ya kujiendesha kibiashara. Kwa mfano, Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) limeendelea kupata hasara licha ya uwekezaji mkubwa wa serikali. Aidha, udhaifu katika usimamizi wa deni la Taifa umeendelea kuwa changamoto, ambapo deni la Taifa limeongezeka kutoka asilimia 27.5 ya Pato la Taifa mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 39.1 mwaka 2023. Changamoto hizi zinahitaji mikakati madhubuti ya kuboresha mifumo ya usimamizi, kuongeza uwazi, na kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma.

iv. Moja ya changamoto kuu ni ukosefu wa mifumo madhubuti ya udhibiti wa ndani katika taasisi za serikali. Hii inajidhihirisha katika matumizi yasiyoidhinishwa ya fedha za umma, ambapo ripoti ya CAG ya 2022/23 ilibaini matumizi yasiyoidhinishwa ya TZS bilioni 12.3. Aidha, kuna changamoto ya ukusanyaji wa mapato, ambapo TZS bilioni 28.5 hazikukusanywa katika mwaka huo huo wa fedha. Hali hii inaathiri uwezo wa serikali kutoa huduma bora kwa wananchi na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati.

v. Changamoto nyingine ni ukiukwaji wa taratibu za manunuzi ya umma. Ripoti ya CAG ilibaini kuwa 18% ya mikataba iliyokaguliwa haikufuata sheria na kanuni za manunuzi ya umma. Hii inaongeza uwezekano wa kupotea kwa fedha za umma na kupunguza thamani ya fedha katika miradi ya maendeleo. Vilevile, usimamizi wa deni la Taifa unaendelea kuwa changamoto, ingawa kumekuwa na maboresho, bado kuna haja ya kuimarisha mikakati ya kudhibiti ukuaji wa deni. Pia, kuna changamoto ya usimamizi wa rasilimali za bahari, hususan katika sekta ya uvuvi na uchimbaji wa mafuta na gesi, ambapo bado kuna uhitaji wa kuimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji.

vi. Uwezo mdogo wa kiufundi na rasilimali watu katika taasisi za usimamizi ni changamoto inayoathiri ufanisi wa usimamizi wa rasilimali za umma. Hii inajidhihirisha katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ambapo baadhi ya miradi inachelewa kukamilika au haikidhi viwango vinavyotakiwa. Aidha, kuna changamoto ya uratibu baina ya taasisi mbalimbali za serikali zinazohusika na usimamizi wa rasilimali za umma, jambo ambalo linapelekea kuwa na mwingiliano wa majukumu na kupunguza ufanisi. Changamoto hizi zinahitaji mikakati madhubuti na ya muda mrefu ili kuboresha usimamizi wa rasilimali za umma na kuhakikisha manufaa yanawafikia wananchi wote wa Zanzibar.

## 5.4 MATAMKO KUHUSU RUSHWA, UWAJIBIKAJI NA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UMMA

a) Asasi za Kiraia zinahimiza uimarishaji wa uwezo wa TAKUKURU na ZAECA kwa kuongeza rasilimali watu na vifaa vya kisasa. Hii ijumuishe uajiri wa wataalamu wa teknolojia ya habari, wachunguzi wa makosa ya kifedha, na wataalamu wa uchambuzi wa data. Aidha, mafunzo ya mara kwa mara yaandaliwe ili kukabiliana na mbinu mpya za rushwa. Vifaa vya kisasa vya uchunguzi, pamoja na programu za kompyuta za uchambuzi wa data, vipatikane ili kuongeza ufanisi katika uchunguzi wa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi.

b) Tunapendekeza utekelezaji wa haraka wa Sheria ya Ulinzi wa Watoa Taarifa (Whistleblower Protection Act) ili kulinda watu wanaotoa taarifa za vitendo vya rushwa. Sheria hii ihakikishe ulinzi wa kimwili, kisheria, na kiuchumi kwa watoa Taarifa. Ianzishe mfumo salama wa kutoa taarifa, ikiwemo njia za kidijitali, na itoe fidia kwa watoa Taarifa wanaoathirika kutokana na ushirikiano wao. Aidha, sheria hii iainishe adhabu kali kwa wanaojaribu kulipiza kisasi dhidi ya watoa taarifa na iweke utaratibu wa kushughulikia taarifa za uongo.

c) Asasi za Kiraia zinapendekeza uboreshaji wa mfumo wa kidijitali wa manunuzi ya umma, unaowezesha ufuatiliaji wa mchakato mzima wa zabuni. Mfumo huu uwe wazi kwa umma na uwe na vipengele vya kutoa tahadhari za moja kwa moja kwa vyombo vya udhibiti. Uwezo wa kuchambua data moja kwa moja (automatically) uongezwe ili kutambua misamaha isiyo ya kawaida katika michakato ya zabuni. Mfumo huu pia uunganishwe na kanzidata za taasisi nyingine za serikali ili kurahisisha uhakiki wa Taarifa za makampuni yanayoshiriki katika zabuni za serikali.

d) Tunahimiza uimarishaji wa elimu ya uraia kuhusu madhara ya rushwa na umuhimu wa uwajibikaji. Hii ijumuishe kuingiza masomo ya maadili na utawala bora katika mitaala ya elimu kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu. Pia, kampeni za uhamasishaji wa umma ziandaliwe kwa kutumia vyombo vya habari na majukwaa ya mitandao ya kijamii. Mashindano ya kitaifa ya ubunifu katika kupambana na rushwa yafanyike kila mwaka, huku vikundi vya kijamii vikihimizwa kuanzisha miradi ya kupambana na rushwa katika ngazi ya jamii.

e) Asasi za Kiraia zinapendekeza kuimarisha jukwaa la wadau la kusimamia utekelezaji wa miradi ya Uwajibikaji wa Wawekezaji kwa Jamii (CSR). Jukwaa hili lihusishe wawakilishi wa serikali, sekta binafsi, AZAKI na jamii husika. Liwe na mamlaka ya kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya CSR, ikiwemo uwekaji wa viwango vya chini vya uwekezaji katika CSR. Jukwaa hili pia litoe mwongozo wa kitaifa wa CSR, lihakikishe uwazi katika matumizi ya fedha za CSR, na litoe ripoti za mara kwa mara kuhusu athari za miradi ya CSR kwa jamii.

f) Tunadai kuimarishwa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kuongeza rasilimali na uhuru wake wa kiutendaji. CAG apewe mamlaka ya kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yake na kutoa taarifa za mara kwa mara. Ofisi hii ipewe uwezo wa kufanya ukaguzi wa kidijitali na iwe na kitengo maalum cha kuchunguza matumizi mabaya ya fedha za umma. Aidha, CAG apewe uwezo wa kufikisha moja kwa moja mahakamani wale wanaobainika kutumia vibaya fedha za umma, badala ya kusubiri mamlaka nyingine kuchukua hatua.

g) Asasi za Kiraia zinataka kuboresha mfumo wa ufuatiliaji wa rasilimali za umma kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Mfumo huu utumie teknolojia ya blockchain kusajili na kufuatilia mali zote za umma, ikiwemo ardhi, majengo, na vifaa. Utasaidia kufuatilia matumizi ya fedha za umma, mikataba ya serikali, na usimamizi wa mali za umma kwa uwazi zaidi. Mfumo huu uunganishwe na mifumo ya kifedha ya serikali ili kuwezesha ufuatiliaji wa moja kwa moja wa matumizi ya fedha za umma na kubaini miamala isiyofaa.

h) Tunapendekeza kuimarisha uwezo wa mahakama zilizopo kushughulikia kesi za rushwa na uhujumu uchumi kwa haraka na ufanisi. Hii ijumuishe mafunzo maalum kwa majaji na kuanzisha vitengo maalum vya kushughulikia kesi hizi. Teknolojia ya kisasa itumike katika kusikiliza na kusimamia kesi, ikiwemo matumizi ya mikutano kwa picha mjongeo (video conference) na mifumo ya kidijitali ya usimamizi wa kesi. Aidha, sheria zihuishwe ili kurahisisha utoaji wa ushahidi katika kesi za rushwa na uhujumu uchumi, huku zikihakikisha haki za watuhumiwa zinalindwa.

i) Asasi za Kiraia zinahimiza uimarishaji wa ushirikishwaji wa jamii katika maamuzi ya usimamizi wa rasilimali za umma. Hii ijumuishe kuanzishwa kwa mikutano ya mara kwa mara ya uwajibikaji kati ya viongozi na wananchi katika ngazi zote za serikali. Mfumo wa bajeti shirikishi uimarishwe, ukitumia teknolojia ya kisasa kuwezesha ushiriki wa wananchi katika mchakato wa bajeti. Pia, jukwaa la kidijitali la wazi lianzishwe ili wananchi waweze kutoa maoni yao kuhusu sera na miradi ya serikali, na kufuatilia utekelezaji wake.

j) Tunadai kuanzishwa kwa mfumo wa tathmini ya athari za rushwa (Corruption Impact Assessment) kwa sera na sheria zote mpya zinazopitishwa. Tathmini hizi ziwe za lazima na zifanywe na timu ya wataalam huru. Matokeo yake yawekwe wazi kwa umma kupitia tovuti maalum na yajadiliwe katika vikao vya bunge. Mfumo huu ujumuishe pia tathmini ya athari za rushwa kwa miradi mikubwa ya umma na mikataba ya uwekezaji. Ripoti za tathmini hizi zitumike kama msingi wa kuboresha sera na sheria ili kuziba mianya ya rushwa.

k) Mikataba yote hapa nchini, michakato yake iwe ya wazi na mingine ipite bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa na bunge.

# USAWA WA KIJINSIA NA MAKUNDI MAALUM



SURA
YA **SITA**

# USAWA WA KIJINSIA NA MAKUNDI MAALUM

## 6.0 KUHUSU SURA HII

Sura hii inatathmini ulinzi na utekelezaji wa haki za makundi maalum na usawa wa kijinsia kama inavyoainishwa katika mikataba ya kimataifa, sera, sheria, kanuni, mikakati, taratibu, na miongozo ya kitaifa. Sura hii inalenga siyo tu kuwakumbusha wenye mamlaka na viongozi wanaotokana na uchaguzi juu ya wajibu wao, bali pia kuhakikisha haki na vipaumbele vinazingatiwa kulingana na mahitaji ya kila kundi. Hii inatilia mkazo utekelezaji wa haki za makundi yote ili kuwezesha maendeleo jumuishi na yanayozingatia usawa wa kijinsia.

## 6.1 UTEKELEZAJI WA ILANI YA AZAKI 2019-2024.

### 6.1.1 Usawa Wa Kijinsia

**a) Jitihada Zilifikiwa**

Katika kipindi hiki cha miaka mitano, miradi ya kijinsia ikiwemo Mradi wa Maliza Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji kwa Wanawake na Wasichana (TOKOMEZA) na Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia (Advancing Gender Equality in Tanzania) vilianzishwa ili kutokomeza vitendo vya kikatili kwa wanawake na watoto lakini pia kuleta usawa katika jamii.

Pamoja na juhudi hizi, upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi umeimarika na vifo vya uzazi vimepungua. Mkakati wa Kuzuia na Kutokomeza Ukeketaji 2020/21-2024/25 ulianzishwa na jitihada nyingi za kutokomeza ukeketaji zikaungwa mkono huku nyumba salama 11 zikitoa hifadhi kwa wahanga. Elimu kwa wasichana imeimarika na idadi yao shule za sekondari imeongezeka, na marekebisho ya Sheria ya Ardhi yameimarisha umiliki wa ardhi kwa wanawake. Kwa upande wa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatoa huduma za nyumba salama kwa wahanga wa udhalilishaji, na vituo vya afya 352 vimejengwa, kuboresha upatikanaji wa huduma za afya.

Elimu kwa wasichana imeimarika, huku asilimia yao shule za sekondari ikiongezeka kutoka 52.3% mwaka 2020 hadi 54.7% mwaka 2023. Vifo vya uzazi vimepungua kutoka 556/100,000 mwaka 2015 hadi 432 mwaka 2022 kutokana na juhudi za kuboresha huduma za afya ya uzazi. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeendelea kutoa huduma za nyumba salama kwa wahanga wa udhalilishaji, jumla ya wahanga 66 walihifadhiwa hadi Machi 2024. Vituo vya afya 352 vimejengwa kote nchini, kupunguza muda wa kufuata huduma za afya.

### b) Changamoto

i) Kukosekana kwa utashi wa kisiasa wa kutenga bajeti ya kutekeleza afua za kijinsia, kushamiri kwa mila na desturi gandamizi zinazowanyima wanawake, vijana na watu wenye ulemavu haki ya kushiriki katika uongozi; elimu; kukosekana kwa fursa za uwezeshaji wa kisiasa, kijamii na kiuchumi kwa wanawake, mgawanyo usio sawa wa majukumu kati ya mwanaume na mwanamke katika kaya; upatikanaji mdogo wa teknolojia sahihi na wanawake kukosa haki ya kumiliki mali.

ii) Takwimu za UNICEF (2021) zinaonyesha kuwa asilimia 31 ya wasichana Tanzania huolewa kabla ya kufikisha miaka 18. Hii inazuia elimu yao na kuwaweka katika mazingira hatarishi kiafya na kiuchumi. Ingawa kiwango cha ukeketaji kimepungua, bado ni tatizo kubwa katika mikoa kama Manyara (58%) na Dodoma (47%).

iii) Uwiano wa kipato kati ya wanawake na wanaume unakosekana, wanawake wakipata 63% tu ya kipato cha wanaume kwa kazi sawa (ILO, 2022). Hii inaendelea kutengeneza utegemezi unaochochea vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na jamii kwa ujumla.

iv) Unyanyasaji wa Kijinsia hasa ukatili wa majumbani unaendelea kushamiri huku wanawake na watoto wakiwa wahanga wakubwa hali inayoendelea kuathiri afya na ustawi wa wanawake.Ukatili wa kijinsia kwenye mitandao unaendelea kushika kasi hii inaambatanisha lugha za matusi hususani kwa Jinsia Ke, na usambazaji wa picha zinazotweza utu wao.

## 6.1.2 Ulinzi na Ustawi wa Wazee

### a) Jitihada Zilizofikiwa

Katika utekelezaji wa ilani ya AZAKI iliyopita, serikali imeongeza huduma za afya kwa wazee, ikiwa ni pamoja na vitambulisho vya wazee, bima za afya, na kipaumbele cha matibabu. Kampeni ya "MPISHE MZEE KWANZA" imeanzishwa, na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ( SMZ) imeanzisha mfumo wa pensheni kwa

wazee wenye umri wa miaka 70 na kuendelea, lengo likiwa ni kuboresha hali ya maisha ya wazee na kutatua changamoto zinazowakabili.

**b) Changamoto**

i) Changamoto za upatikanaji wa bima za afya, vitambulisho vya wazee, na hali duni za kiuchumi zinaendelea kutatiza maisha yao.

ii) Wazee wengi wanakabiliwa na upweke kutokana na kutokuwa na msaada wa familia na jamii, hali inayosababisha msongo wa mawazo na matatizo ya kisaikolojia.

iii) Kulingana na sensa ya 2022, Tanzania ina asilimia 6 ya wazee, wengi wao wakiwa vijijini na wakikabiliwa na changamoto za huduma duni za afya, ukatili, na kipato cha chini.

iv) WHO 2022 inaripoti kwamba asilimia 93 ya wazee wenye zaidi ya miaka 60 hawana hifadhi ya jamii, hali inayohatarisha maisha yao.

### 6.1.3 Haki, Ulinzi, Usalama na Ustawi wa Mtoto

**(a) Jitihada Zilizofikiwa**

i) Kuongeza ulinzi wa watoto, serikali imezindindua Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwa wanawake na watoto (MTAKUWWA II), kuanzishwa kwa mabaraza ya watoto katika ngazi ya shule na kata. Pia kumekuwepo Mwongozo wa program za malezi katika ngazi ya shule, kata na kaya.

ii) SMZ kupitia Wizara imefuatilia uendeshaji wa vituo 50 (Unguja 40 na Pemba 10) vya Malezi ya kutwa kwa watoto (Day Care Centres). Hatua hiyo ni kwa mujibu wa sheria na taratibu za Serikali. Aidha, taratibu za kuhamasisha uanzishwaji wa vituo zinaendelea ambapo mikutano ya wadau wa vituo vya makuzi na malezi ya awali ya mtoto (ECD) ilifanyika Unguja na Pemba.

iii) Muongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa Mabaraza na Klabu za Watoto umeandaliwa ili kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya mabaraza. Jumla ya washiriki 66 (wanawake 43 na wanaume 23) wameshiriki vikao hivyo Unguja na Pemba.

iv) Serikali imeanzisha vituo 2,833 vya kulelea watoto mchana ili kutoa huduma ya malezi na kuhakikisha ulinzi wa watoto wakati wazazi na walezi wao wakijihusisha na shughuli za kiuchumi.

v) Serikali imeendelea kufuatilia na kudhibiti makosa ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia ikiwemo ubakaji, ulawiti, kutupa watoto, wizi wa watoto, ukeketaji na vipigo kupitia Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto. Takwimu zinaonesha kuwa vitendo vya ukatili vimepungua kutoka matukio 41,416 (Me 13,471 na 27,945) mwaka 2017/2018 hadi kufikia 29373( me 8476 na ke 20897) kwa mwaka 2021.

**(b) Changamoto**

i) Tatizo la watoto wa mitaani linaongezeka kutokana na changamoto za familia na jamii, ikiwa ni pamoja na hatari ya unyanyasaji kingono, uraibu wa madawa ya kulevya, uhalifu, na ombaomba.

ii) Watoto nchini Tanzania wanakumbana na hatari nyingi kama unyanyasaji mtandaoni na matangazo ya vitendo vyenye athari za kijinsia. Utafiti wa 2021 ulibaini kuwa watoto wapatao 200,000 walikumbana na unyanyasaji wa kijinsia mtandaoni, ambapo wengi wao hawakuutambua.

iii) TDHS 2022 ilionesha kuwa asilimia 34 ya wasichana walikumbana na FGM kabla ya miaka 5, na asilimia 28 kati ya miaka 10-14.

iv) Ndoa za watoto pia ni tatizo, ambapo asilimia 11.9 ya wasichana na asilimia 0.7 ya wavulana wenye umri wa miaka 15-19 walikuwa wameolewa.

v) Taarifa za polisi zinaonyesha takriban Watoto elfu kumi wana bakwa kila mwaka na Watoto 3000 wanalawatiwa kila mwaka.

vi) Utekaji na upoteaji wa Watoto umeshamiri nchini , taarifa ya THRDC inaonyesha vitendo vya utekaji vimeongezeka na kupelekea Watoto zaidi ya 100 kupotea na kutekwa kwa mwaka.

vii) Taasisi zinazosimamia masuala ya Watoto hasa ustawi wa jamii nchini hazina ufahamu wa kutosha juu ya sheria ya mtoto na pia ni wachache sana nchini kinyume na matakwa ya sheria. Asilimia 90 ya kata nchini hazina watumisi wa ustawi wa jamii wanaopaswa kusimamia masuala yote ya Watoto.

### 6.1.4 Haki, Ustawi na Ujumuishwaji wa Vijana

**a) Jitihada Zilizofikiwa**

i) Serikali ya Tanzania imeongeza juhudi za kuwajumuisha vijana katika miradi ya maendeleo kupitia mafunzo ya ujuzi na ufundi stadi, na mikopo ya Halmashauri inayojulikana kama 4-4-2.

ii) Zanzibar pia imeanzisha Baraza la Taifa la Vijana na mipango ya uwezeshaji kiuchumi. Ilani ya 2019/2024 ilihimiza mapitio ya Sera ya Vijana ya 2007, na serikali imetoa Sera mpya ya Vijana 2024, ikilenga ushiriki wa vijana katika maendeleo endelevu. Programu ya Building Better Tomorrow: Youth Initiative in Agribusiness (BBT-YIA) imewezesha vijana 812 katika kilimo biashara, huku asilimia 34.73 wakiwa wanawake.

iii) Aidha, utafiti wa Afya ya Vijana na Watoto umeanzishwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Ofisi za Takwimu, THPS, na UNICEF, ili kuboresha mipango na huduma za maendeleo ya vijana nchini.

**b) Changamoto**

i) Vijana bado wanakabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo tatizo la upatikanaji wa ajira ambapo uhitaji ni mkubwa sana kwa wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu, ujumuishwaji wa vijana katika vyombo vya maamuzi, kukosekana mfumo rasmi wa kukuza vipaji vya vijana na kuendeleza ubunifu wa vijana.

ii) Ukosefu wa ajira umeendelea kuwa changamoto kubwa hapa nchini,kwa sensa ya mwaka 2022, asilimia 35 ya watanzania ni vijana, vijana hawa wengi wanaujuzi na elimu lakini wanakosa ajira rasmi hivyo kujiingiza kwenye vitendo vya ubakaji, ulevi, wizi na udanganyifu.

iii) Tafiti za Viashiria vya maambukizi ya VVU 2023 nchini zinaonyesha kuwa asilimia 40 ya hali ya maambukizi mapya ya VVU ni kwa vijana wenye umri wa miaka kati ya 15 na 24 huku wasichana wakiwa hatarini zaidi.

iv) Vijana wengi bado wanakosa fursa na nafasi za ushiriki katika nafasi za uongozi, kwa sekta za kisiasa, serikali na kijamii hali ambayo inaelendelea kupelekea kukosa ushiriki katika masuala yanayo amua kesho yao.

**6.1.5 Haki, Ulinzi na Ustawi wa Watu wenye Ulemavu**

**(a) Jitihada Zilizofikiwa**

i) Serikali ya Mapinduzi Zanzibar(SMZ) imepiga hatua ya kufanya mapitio ya sheria ya watu wenye ulemavu ya 2006, na kuunda baraza la watu wenye ulemavu lenye hadhi ya utendaji na uendeshaji wa shughuli za watu wenye ulemavu.

ii) SMZ Kupitia Wizara ya maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeendelea kutoa msaada kwa watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi ambapo hadi Mwaka 2023, jumla ya familia 235 zilipokea msaada na

hadi kufikia Machi 2024 idadi ya wanufaika imeongezeka na kufikia 283, sawa na ongezeko la familia 48.

iii) Kupungua kwa mtazamo hasi dhidi ya watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu wamekuwa wakijumuishwa katika mambo mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi, hii inatafsiri jamii kutambua nafasi ya watu wenye ulemavu na mchango wao katika kuchagiza maendeleo na ustawi wa jamii kwa ujumla. Kwa mfano, uwepo wa wabunge wenye ulemavu bungeni na katika nafasi mbalimbali za uongozi kitaifa na uwepo wa watu wenye ulemavu kwenye sekta ya ajira.

iv) Serikali imeongeza wigo mpana wa elimu kwa watu wenye ulemavu kwa kuzingatia mahitaji yao muhimu na kurahisisha mchakato wa kujifunza na kuweka mazingira wezeshi ikiwemo majengo fikivu, vifaa saidizi na kuanzisha taasisi mbalimbali za elimu ya juu zenye kuzingatia ujumuishi ikiwa ni Pamoja na vyuo vya ufundi stadi (VETA) ili kuwapa nafasi watu wenye ulemavu ambao wanakosa nafasi za kuendelea na elimu ya juu wapate kujifunza stadi mbalimbali na kuweza kukidhi mahitaji yao.

v) Kutengwa kwa bajeti zinazo zingatia watu wenye ulemavu. Serikali imekuwa ikitenga bajeti maalumu kwaajili ya watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kiuchumi, kielimu na kijamii, mfano katika mikopo ya asilimia 10 kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ambapo watu wenye ulemavu wana asilimia mbili (2%) pia gawio (ruzuku) wanalotoa kwa shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu.

**(b) Changamoto**

i) Idadi kubwa ya watu wenye ulemavu haijafikiwa kikamilifu katika nyanja tofauti. Mathalani, hakuna mfumo maalumu wa kitaifa wa kuwajumuisha watu wenye ulemavu katika nafasi za uongozi achiliambalia juhudi binafsi za vyama vya siasa.

ii) Watu wenye ulemavu wengi hawajapata elimu, huduma ya afya imekuwa ni changamoto kutokana na watu wenye ulemavu wengi kuwa maskini na hawana BIMA za afya zenye hadhi ya rufaa

iii) Kuna uhaba wa wataalamu wa masuala ya watu wenye ulemavu katika sekta muhimu kama afya na elimu.

iv) Mikataba, Sheria na kanuni zinazohusu haki na mahitaji ya watu wenye ulemavu na kuhimiza kujumuishwaji kwa watu wenye ulemavu katika nyanja zote za kijamii hazijatekelezwa kikamilifu.

v) Zaidi, watu wenye ulemavu hasa wenye ualbino wamekuwa ni wahanga wa vitendo vya kikatili kuuwawa kikatili (kukatwa viungo) hasa kila zinapokaribia chaguzi.

vi) Uelewa mdogo na imani potofu kwa jamii dhidi ya watu wenye ulemavu. Hii inapelekea mauaji ya watu wenye ualbino kwa dhana za kupata nafasi za uongozi na utajiri wa mali. Pia kuuawa kwa Watoto waliozaliwa na ualemavu kutokana na jamii kuamini kuwa kuzaa mtoto mwenye ulemavu ni mkosi au laana.

vii) Miundombinu isiyo rafiki na yenye kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu. Miundombinu mbalimbali ikiwemo majengo, usafiri na kadhalika imekuwa ni changamoto kubwa katika ufikiwaji na watu wenye ulemavu, hii imetokana na utekelezwaji hafifu wa sheria na miongozo mbali mbali inayohusu ufikiwaji kwa watu wenye ulemavu. Mathalani, sheria na miongozo inaelekeza kuwa majengo yote ya huduma za kijamii yasiwe kikwazo kwa mtu mwenye ulemavu kupata huduma husika.

viii) Lakini pia miundombinu ya usafiri kama vituo vya usafiri wa umma na usafiri wa umma kwa ujumla vimekuwa ni kikwazo kwa watu wenye ulemavu wanaotumia viti-mwendo.

ix) Uelewa mdogo wa haki na mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa mamlaka zinazosimamia ulinzi na usalama Pamoja na mamlaka zingine. kwa mfano jeshi la polisi katika kutekeleza majukumu yake hasa ukamataji hawazingatii watu wenye ulemavu kulingana na mahitaji yao mathalani mtu mwenye ulemavu wa kusikia ni vigumu kusikia amri na maelekezo hvyo kupelekea madhara makubwa kwake ikiwemo kujeruhiwa.

x) Tanzania haijawasilisha ripoti ya utekelezaji wa mkataba wa kimataifa wa watu wenye ulemavu (UNCRPD) tangu ilipo ridhia mkataba huo mwaka 2009. Hii inapelekea kutokujua hali halisi (status) ya utekelezwaji wa mkataba huo na pia kuzuia wadau kuingilia kati katika utekelezwaji wa haki na ustawi wa watu wenye ulemavu.

## 6.2 MATAMKO YA ILANI

### 6.2.1 Tamko Kuhusu Usawa wa Kijinsia

a) Serikali inahitaji viongozi watakao imarisha uwakilishi wa wanawake katika nafasi zote za uongozi na maamuzi kwa kufikia lengo la 50/50. Viongozi hawa wataboresha mazingira ya elimu kwa watoto, hasa wasichana, ili kuongeza idadi ya wanawake katika masomo ya STEM na kuhakikisha elimu bora kwa wote.

b) Ni muhimu kufanya mapitio na marekebisho ya sheria gandamizi kwa wanawake, kama Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, Sheria ya Mirathi ya mwaka 1865, na Sheria za Kimila Na. 4 ya mwaka 1963. Serikali itasimamia utekelezaji wa sheria zote za kikatiba na kimila ili kuondoa ubaguzi na ukandamizaji dhidi ya wanawake na wasichana.

c) Viongozi wadhibiti mifumo inayowapa wenye mali madaraka makubwa ya kisiasa, kuimarisha demokrasia shirikishi, na kuongeza ushiriki wa wanawake na wanaume maskini katika maamuzi ya kitaifa.

d) Viongozi kupiga marufuku matumizi ya lugha za kashfa, matusi, na udhalilishaji kwenye chaguzi ili kuhakikisha ushiriki wa makundi yote bila vikwazo.

e) Viongozi kuongeza kasi ya kupambana na ukatili wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na rushwa ya ngono dhidi ya wanawake.

### 6.2.3 Tamko Kuhusu Watoto.

a) Itungwe sheria na kuandaa miongozo ya kuwalinda watoto dhidi ya utandawazi usiokuwa na maadili ikiwa ni pamoja na elimu ya magharibi yenye masuala yaliyo kinyume na mila na desturi za mtanzania

b) Vyombo vya dola vianze mara moja kufuatilia, kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya kupotea na kutekwa kwa watoto. Hii ikiwa ni sambamba na Serikali kuja na mkakati wa kukuzihuisha Kamati za MTAKUWWA kila Mtaa na Kijiji, na kamati zipewe majukumu yake ikiwa ni pamoja na kutambua mfumo wa kutoa taarifa kwa kila wiki kwa Halmashauri za vijiji/kamati za Mtaa na Kamati za maendeleo ya Kata (WDC) zianzishe vikundi vya rafiki wa watoto ndani ya jamii na kuviwezesha kukutana na kuwasilisha taarifaa kwa mamlaka zinazohusuka kila wiki ili kubaini viashria vya Vitendo vya Ukatili kabla ya kutokea na kuleta madhara, vitasaidiana na mamlaka husika katika ulinzi wa mtoto na kushauri juu ya usalama wa watoto.

c) Serikali ije na mkakati madhubuti wa kuondoa watoto wa mtaani wenye umri wa kwenda shule na kutenga Bajeti ya kutekeleza Mkakati wa kutokomeza tatizo hili katika miji na majiji.

d) Serikali iendelee kuhimiza miundo mbinu ya shule inayojengwa izingatie mahitaji jumuishi ya watoto wenye ulemavu hasa kwa kuwa na ngazi mterezo mahali penge ngazi sambamba na choo maalumu kwa watoto wenye ulemavu.

e) Serikali ije na mkakati wa ulinzi na malezi jumuishi kwa mtoto wa kiume

ili kumuepusha na vitendo viovu, ukatili wa kijinsia ili kumkukuza katika maadali.

f) Kuanza kutoa elimu ya haki za binadamu kuanzia shule za awali zikilenga kumjenga mtoto kuhusu haki za binadamu na hasa haki zake kama mtoto na namna bora ya kukabiliana na ukiukjwaji wa haki za mtoto.

g) Serikali kupeleka ustawi wa jamii kwa kata zote nchini na kuwapa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu sheria ya mtoto, haki za mtoto na namna bora ya kutatua migogoro ya ndoa/wenza.

### 6.2.2 Ulinzi, Usalama na Ustawi wa Wazee

a) Wakati wa mchakato wa uchaguzi wa serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu, vyama vya siasa vihakikishe kuna usalama kwa wazee wanaoshiriki shughuli za kisiasa ili wasibughudhiwe, kuumizwa, kudhalilishwa na kufanyiwa ukatili wa aina yeyote.

b) Viongozi watakaoingia madarakani ianzishe utaratibu wa kuhakikisha taasisi za udhibiti wa jamii zinaelekeza huduma zao katika sekta isiyo rasmi.

c) Serikali ihakikishe inapata takwimu sahihi kuhusu wazee na kuwaunganisha na mifuko ya hifadhi ya jamii pamoja na fursa nyingine.

d) Serikali ianzishe utaratibu wa kuelimisha na kuwajengea uelewa jamii kuhusu kutunza na kulinda haki za wazee katika ngazi ya familia ili kupunguza kasi ya kujengwa kwa makazi ya wazee.

e) Wafanyakazi wa afya wapate mafunzo maalum ya kutunza, kuwapokea na kuwahudumia wazee na hasa umuhimu wa kuupa kipaumbele utunzaji wa afya kwa wazee.

### 6.2.4 Tamko Kuhusu Vijana

i. Uanzishwaji wa fursa za za ajira, na kuweka mifumo rafiki ya mchakato wa uombaji na upatikanaji wa ajira katika sekta za umma na binafsi

ii. Kuboresha mfumo wa elimu kwa vijana, wanapate elimu na Mafunzo kwa vitendo yanayowapa ujuzi na maarifa ya kuwawezesha kuwa wabunifu na zaidi kuwaweza kujiajiri/ ujasiriamali

iii. Uanzishwe utaratibu wa kuwapa nafasi vijana kushirki kwenye michezo inayokuza na kuendelea vipaji vyao

iv. Serikali itekeleze program za uwezeshaji wa vijana usio na ubaguzi kwa misingi ya kiitikadi ili kuwapa fursa wote kushiriki katika shughuli za uzalishaji na kujipatia kipato

v. Uandaliwe mfumo wa kuwezesha vijana wote kushiriki shughuli za uchumi na kupata ujira stahiki/bila kunyonywa.

vi. Viongozi waanzishe utaratibu wa kutambua vijana wenye vipaji na ubunifu katika maeneo tofauti na kuviendeleza waweze kuongeza thamani ya vipaji hivyo viwaingizie kipato.

### 6.2.6 Haki na Ujumuishwaji wa Watu wenye Ulevamvu

i) Viongozi watakaochanguliwa wanapaswa kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu, hasa wenye ualbino, wanatambuliwa na kuimarishwa ulinzi dhidi ya vitendo vya kikatili katika maeneo wanayoishi.


ii) Viongozi wanapaswa kusimamia ubora wa elimu wanayopata watu wenye ulemavu katika mazingira rafiki na jumuishi, wakihakikisha upatikanaji wa vifaa saidizi na walimu wa elimu maalum wa kutosha.

iii) Serikali itakayoingia madarakani inapaswa kuupa kipaumbele mchakato wa kuhuisha Sera, Sheria, na Miongozo inayosimamia masuala ya watu wenye ulemavu, pamoja na mifumo ya usimamizi wa utekelezaji wa matakwa ya kisheria.

iv) Serikali itoe maelekezo ya kuboresha miundo mbinu katika taasisi za umma na majengo ya huduma kwa umma ili kuwa na viwango vya ufikivu kwa watu wenye ulemavu, ikiwemo uandaaji wa mwongozo wa ufikivu na ukaguzi wa miundo mbinu. Aidha, somo la lugha ya alama linapaswa kujumuishwa kwenye vyuo vya mafunzo kwa wataalamu wa elimu, afya, na ustawi wa jamii.

v) Serikali itakayoingia madarakani inapaswa kuhakikisha kwamba nafasi zote za maamuzi zinajumuisha watu wenye ulemavu na kuanzisha mfumo wa motisha ya nafuu ya kodi kwa taasisi binafsi zinazowaajiri watu wenye ulemavu, huku zikiweka mazingira rafiki kwa utekelezaji wa majukumu yao ya kazi.

vi) Tanzania iwasilishe ripoti ya utekelezaji wa mkataba wa kimataifa wa watu wenye ulemavu (UNCRPD).


KUIMARISHA UPATIKANAJI WA HUDUMA MUHIMU ZA KIJAMII KWA WANANCHI WOTE

SURA YA **SABA**

# KUIMARISHA UPATIKANAJI WA HUDUMA MUHIMU ZA KIJAMII KWA WANANCHI WOTE

## 7.0 KUHUSU SURA HII

Sura hii inalengo la kuainisha maeneo ya kisera ambayo Asasi za Kiraia zinahitaji kuona zikiimarishwa ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii kwa wananchi wote. Aidha, sura hii imeonesha jitihada zilizofanywa, changamoto zilizopo pamoja na kutoa matamko ya kiilani ili viongozi wajao watekeleze ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za kijamii.

Ni wazi kwamba, kila mwananchi ana haki ya kupata huduma bora za kijamii kama vile elimu, afya, maji safi na salama pamoja na hifadhi ya Jamii. Serikali ina wajibu wa kuhakikisha huduma za kijamii zinapatikana kwa watu wote kwa urahisi ili kujenga jamii inayojali na jumuishi. Kuna ulinganifu wa karibu kati ya maendeleo ya mtu mmoja mmoja, jamii na kiwango cha upatikanaji wa huduma za kijamii. Hata hivyo, pamoja na kwamba serikali inajitahidi kuimarisha upatikaji wa huduma za kijamii bado hali hairidhishi. Kwa mfano kwa miaka ya karibu tumeshuhudia wananchi wengie wakijitokeza kwenye huduma za matibabu zinazohusisha watu wengi zinazotolewa kwenye makambi kwasababu ya kukosa uwezo wa kugharamia matibabu kwenye hospitali. Kwa ujumla, kuna ushirikishwaji mdogo wa wananchi katika kuchagia, kubuni, kufuatilia na kuendeleza utoaji wa huduma za kijamii. Baadhi ya sera zinazotekelezwa zinawafanya wananchi kuwa wapokeaji zaidi kuliko washiriki hai katika kuboresha huduma za kijamii.

## 7.1 SEKTA YA AFYA

### a) Jitihada Zilizofikiwa

i) Kuongezeka kwa uwekezaji katika miundombinu ya kutolea huduma za afya ambapo vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 8,549 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 9,610 Machi 2024. Hii ni sawa na ongezeko la vituo 1,061.

ii) Maboresho ya miundombinu ya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na ujenzi wa majengo mapya, ukarabati na kukamilisha ujenzi wa hospitali mpya katika mikoa mipya mitano. Maboresho hayo yamegharimu jumla ya Shilingi Trilioni 1.02

iii) Ongezeko la vituo vya kutoa huduma za afya nchini na maboresho ya miundombinu yaliyofanyika yamewezesha kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi.

iv) Wananchi wanapata huduma za afya ndani ya kilometa 5 ya maeneo yao wanayoishi ikiwa lengo ni kufikia asilimia 95 ifikapo mwaka 2030

v) Huduma za kipimo cha CT Scan sasa zinapatikana katika Hospitali 27 kati ya Hospitalii 28 za rufaa za Mikoa nchini. Kwa mwaka 2023, jumla ya wagonjwa 15,386 walipatiwa huduma za kipimo cha CT Scan katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ambapo huduma hizo zilikuwa hazitolewi katika hospitali za Rufaa za Mikoa hapo awali.

vi) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya huduma za Mama na Mtoto (Maternity Blocks) kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa ambazo ni Sekou Toure (Mwanza), Geita, Simiyu, Mawenzi, Njombe na Songwe ambazo zimegharimu kiasi cha shilingi bilioni 71.1.

vii) Kuanzisha wodi maalum kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wagonjwa (Neonatal Care Units - NCU), ambapo hadi kufikia desemba 2023 jumla ya Hospitali 189 zinatoa huduma za NCU ikilinganishwa na Hospitali 165 mwaka 2022 na Hospitali 14 tu mwaka 2018.

viii) Kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto ambapo upatikanaji wake katika Vituo vinavyomilikiwa na Serikali umeongezeka kutoka asilimia 82.5 mwaka 2021 hadi asilimia 88.2 mwaka 2023.

ix) Kuimarisha huduma za Saratani ya mlango wa kizazi, ambapo jumla ya mashine 140 (Thermalcoagulator) za uchunguzi wa Saratani zimenunuliwa na kusambazwa kwenye vituo 140 vya kutolea huduma za afya katika Halmashauri 104 katika Mikoa 26. Vifaa hivi vina thamani ya jumla ya shilingi Bilioni 1.1

x) Kumeimarisha huduma za Upasuaji wa Wajawazito kwa Kuongeza vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni(CEMoNC) kutoka vituo 340 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 523 mwaka 2023.

xi) Kufanikiwa kufanya ununuzi wa vifaa tiba kwaajili ya uchunguzi zaidi ya Bil. 290, Huduma za Kipimo cha CT-Scan kinapatikana katika Hospitali

za serikali za rufaa 27 kati ya 28, Vituo vya kiutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka 8,549 (2021) hadi 9,610 mwaka 2024 na mengine.

**b) Changamoto**

i) Kwa mujibu wa Wizara mahitaji halisi ya watumishi wa afya nchini ni 348,923, lakini hadi Machi mwaka huu kulikuwa na watumishi wa afya 126,925 katika ngazi ya afya ya msingi na hospitali za rufaa za mkoa, kanda na Taifa.

ii) kwa mwaka 2023/24 taarifa ya wizara inaonesha Serikali imetoa vibali vya ajira za watumishi wa afya 13,187 tu, na kwa mwaka 2024/24 taarifa ya Wizara haijaeleza kwa kina ni ajira ngapi zimepangwa kutolewa ili kukabiliana upungufu.Hali hii inafanya upungufu wa watumishi wa afya nchini kuwa kwa asilimia asilimia 64 hali ambayo ni changamoto kubwa kwa ustawi wa wananchi iii) Hivi sasa taarifa ya wizara inaonesha kuwa ni asilimia 15 tu ya watanzania ndio wamejiunga na Mifumo ya Bima za Afya. Kati ya hao wanufaika wa NHIF asilimia 8, CHF na Bima Binafsi asilimia 7.

iii) katika taarifa ya Wizara ya bajeti kwa mwaka 2024/25 hakuna maelezo ya kina yaliyotolewa juu ya tarehe mahususi ya kuanza kwa bima ya afya kwa wote, badala yake Serikali imetoa maelezo ya kuahidi kuendelea na ukamilishaji wa mchakato huo.

iv) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado imeendelea kukumbwa na changamoto ya upatikanaji wa vifaa tiba na dawa. Mara nyingi vituo vya afya vinakabiliwa na uhaba wa vifaa muhimu kama vile dawa, vifaa tiba, na vifaa vya kinga.

v) Miundombinu duni katika Hospitali nyingi za umma imeendelea kuwa changamoto inayoathiri upatikanaji kwa wakati na wa ufanisi wa huduma za Afya katika Maeneo Mengi hapa nchini.

vi) Changamoto ya Tatizo la Afya ya Akili imeendelea kuwa changamoto ya Kitaifa, mfano, Inakadiriwa hadi mwaka 2024, kumekuwa na wagonjwa wa Afya ya akili takribani 5000 Zanzibar na 138625 kati ya July 2022 na Machi 2023 Tanzania Bara

vii) Baadhi ya Watoa huduma, wanafanya kinyume na maelekezo waliopewa na ZHSF jambo ambalo linasabisha kuwepo kwa viashiria vya udanganyifu.

viii) Kwa Upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), baadhi ya Watoa huduma wamekuwa wakiwaandikia wagonjwa dawa zisiohusiana na maradhi yao hivyo kuwatengenezea usugu wa dawa sambamba na kuwasababishia maradhi mengine ikiwemo kufeli kwa figo.

ix) Ufinyu wa bajeti kwa sekta ya Afya SMZ na Tanzania Bara imeendelea kuwa changamoto na kufanya huduma kwa wananchi kutokuwafikia sawa na mahitaji na wakati, pia hali hii inapelekea jamii husussani watu wa chini kushindwa kumudu gharama za huduma binafsi hali inayohatarisha zaidi ustawi wa jamii zetu hususani kwa watoto na akina mama.

x) Takwimu zinaonyesha uhaba mkubwa wa vituo vya afya vya msingi, hususan katika maeneo ya vijijini. Zaidi ya asilimia 40 ya zahanati zinazohitajika katika vijiji, hali ambayo ni mbaya zaidi katika ngazi ya kata, ambapo asilimia 79 ya vituo vya afya vinavyohitajika havipo. Ukosefu huu wa miundombinu ya afya una athari kubwa kwa afya ya wanawake,watoto na wazee wa kiume na kike ikiwemo matatizo wakati wa ujauzito na kujifungua, magonjwa ya zinaa, mimba zisizotarajiwa na utoaji mimba usio salama.

xi) Huduma za Afya kwa Watoto bado ni changamoto kubwa sana kwa sasa baadaya bima ya Afya Toto kuondolewa.

xii) Bango Kitita cha Bima ya Taifa ( NHIF) bado kina changamoto nyingi kwa jamii na watoa huduma za afya.

## 7.2. UPATIKANAJI WA HUDUMA YA MAJI, USAFI NA MAZINGIRA

### a) Jitihada Zilizofikiwa

i) Kupitia Kampeni ya ***"Tua mwanamke Ndoo kichwani"*** ambayo iliendeshwa na mashirika kadhaa yanayotetea Haki za Wanawake na Usawa wa Kijinsia na kupokelewa na serikali, imesaidia wanawake kutua mzigo wa kazi za huduma na malezi ambazo hazina malipo kama kuchota maji ambazo zinachangia kudhohofisha jitihada za kujikwamua kiuchumi kwa wanawake.

ii) Kwa kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya AZAKI ya mwaka 2020-2024, serikali imejitahidi kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo ya vijijini. Mikakati mbalimbali imetekelezwa ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Jumuiya za Watumiaji Maji ambazo zinajumuisha asilimia 50 ya uwakilishi wa wanawake katika nafasi za maamuzi.

iii) Kumekuwa na ongezeko kubwa la vituo vya kusambaza maji (water points) hali inayosaidia kupunguza muda unaotumiwa na wanawake kuteka maji na hivyo kuwapunguzia uzito wa kazi. Kutokana na jitihada hizi, jumla ya vijiji 10,639 vimeanzisha kamati za maji zenye jukumu la kushughulikia masuala ya upatikanaji wa maji safi na salama. Vilevile, jumla ya vituo 138,987 vya maji vimeanzishwa ambapo vituo 96,952 vinafanya kazi na vinahudumia wakazi wapatao 25,456,436 sawa na asilimia 70.1 ikilinganishwa na wakazi 16,308,651 mwaka 2005.

**b) Changamoto**

i) Jitihada za kuimarisha utoaji wa huduma ya maji safi na salama zinakabiliwa na changamoto nyingi hususan upatikanaji hafifu wa maji uliokithiri katika jamii na hivyo kukwamisha maendeleo ya wanawake.

ii) Idadi ya watu wapatao milioni 20 waishio vijijini hawajafikiwa na vyanzo bora vya maji. Kero ya upatikanaji wa maji inahusisha mgawanyo usio sawa wa maji katika maeneo mbalimbali, tofauti za kijamii (matajiri na masikini), ongezeko la mahitaji ya maji katika sekta mbalimbali, uharibifu wa vyanzo vya maji unaosababishwa na uchafuzi wa mazingira, matumizi yasiyo sahihi ya ardhi, uvamizi wa ardhi kwa ajili ya kilimo, ufugaji na makazi, ukuaji wa miji na maendeleo ya viwanda. Katika muktadha huu, ni muhimu Serikali kuwekeza katika kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama na usafi wa mazingira hususan katika maeneo ya vijijini sambamba na kupunguza gharama za huduma ya maji.

iii) Usafi wa Mazingira, hususani mijini bado imeendelea kuwa changamoto, hivyo kupelekea milipuko ya magonjwa ya Mara kwa Mara

iv) Huduma za maji Safi na umeme umefikia maeneo mengi ya vijijini, hata hivyo zaidi ya asilimia 30 ya maeneo bado hayajafikiwa na huduma hizi hivyo kuendelea kuwa changamoto katika kutekeleza shughuli za kimaendeleo na ustawi bora wa jamiii.

## 7.3. ELIMU

**a) Jitihada Zilizofikiwa**

i) Kuna mafanikio ya kiwango fulani katika kutekeleza hoja za ilani ya Azaki za mwaka **Mwaka 2019-2025**. Serikali imefanya maboresho katika elimu kwa kuhusisha Sera ya elimu na Mitaala ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na jamii.

ii) Msisitizo umewekwa katika kutoa elimu itakayowawezesha wahitimu kuwa na uwezo wa kukabili maisha yao ya kila siku.

iii) Elimu ya amali imepewa kipaumbele ingawa utekelezaji wake hauridhishi sana kutokana na uhaba wa raslimali watu na vifaa. Ni shule 98 tu za sekondari za Tanzania bara ambazo zilianzisha mkondo wa amali, 28 za serikali na 68 katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mtaala.

iv) Wigo wa elimu ya juu ya sekondari umetanuliwa kwa kuongeza TAHASUSI ambazo kwa mujibu wa mtaala wa mwaka 2023 zipo 78 kutoka 16

zilizokuwa zimezoeleka. Baadhi ya TAHASUSI sio mpya, zilipendekezwa tangu mwaka 2007 ila utekelezaji haukifanyika.

v) Serikali imeruhusu wasichana walioacha shule kwa sababu ya ujauzito na wengine kurejea shuleni, Zanzibar mwaka 2006 na Tanzania Bara mwaka 2021 hata hivyo, wasichana wangine hawarudi kwenye mfumo rasmi kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo udhalilishaji, wengi wanapendelea mfumo usio rasmi.

vi) Uandikishaji wa jumla kwa ngazi mbalimbali za elimu Tanzania Bara umeongeza, elimu ya msingi kutoka asilimia 96.90 (2016/17) mpaka asilimia 109.7(2020/21), na uandikishaji halisi kutoka asilimia 84.0 mwaka 2016 mpaka asilimia 95.4 mwaka 2019. Pia uandikishaji watoto wenye ulemavu umeongezeka kutoka 54,294 mwaka 2019 mpaka 60, 823 mwaka 2021. Uandikishaji sekondari umeongezeka kwa kidato cha I-IV kutoka 1, 648, 359 mwaka 2015 mpaka 2, 185, 037 mwaka 2019 na kidato V-VI kutoka 126,024 mpaka 153, 420 mwaka 2019.

b) **Changamoto**

i) Pamoja na maboresho yaliyofanyika kwenye mfumo wa Elimu bado kuna vikwazo vingi katika kutoa elimu itakayowawezesha wahitimu kujenga umahiri unaohitajika katika karne ya 21 na ulimwengu umebadilika kama ifuatavyo:

ii) Maandalizi hafifu ya utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa ikiwemo bajeti na mafunzo kwa walimu

iii) Kuna uhaba wa walimu wa Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari, mwaka 2023 kwa Tanzania Bara kulikuwa na upungufu wa asilimia 51 ya walimu wa sekondari

iv) Kuna uhaba wa wahadhiri

v) Kuna upungufu wa vitabu wa kiada na ziada

vi) Kuna uhaba wa miundo mbinu muhimu kama vyumba vya madarasa na vyoo, Tanzania bara uwiano wa wanafunzi kwenye madarasa ya elimu ya msingi ni 1:74 badala ya 1:45.

vii) Kuna uhaba mkubwa wa vifaa vya TEHAMA kama vile computa za mezani na mpakato

viii) Kuna uelewa mdogo wa sera, miongozo na mikakati miongoni mwa watelezaji,

ix) Kuna uelewa mdogo wa mtaala wa umahiri miongoni mwa walimu na watekelezaji wakuu

x) Kozi zinazotolewa kwenye vyuo vya kati na juu haziongozwi na mpango wowote wa kitaifa wa mahitaji ya rasilimali watu

xi) Kukosekana kwa usawa katika kujifunza na upimaji kutokana matumizi ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia katika ngazi ya sekondari na vyuo

xii) Mfumo wa elimu bado hauna uwezo wa kuandaa vijana wanaoweza shindana katika soko la ajira la kimataifa na pia vijana wengi wanahitimu bila kuwa na ujuzi wa kazi na uwezo wa kujiajiri

xiii) Elimu ya haki za binadamu haipewi kipaumbele katika mfumo wetu wa elimu kunzia ngazi za chini hadi vyuo vikuu.

## 7.4. UHIFADHI WA JAMII

### a) Jitihada Zilizofikiwa

i) Mifuko umerahisisha huduma kwa wanachama kwa kuwa na; kituo cha huduma kwa wateja, dawati la malalamiko katika ofisi zote, mitandao ya kijamii na tovuti, mfano huduma za PSSSF kiganjani, PSSSF popote ulipo mtandaoni na Pamoja App, elimu kwa wanachama kupitia semina na matangazo.

ii) Imeendelea kupunguza umasikini kwa wananchi, kuleta ustawi wa nchi na ukuaji wa uchumi ambapo inawaweka wananchi katika hali ya usalama kwa kuwa wana uhakika wa kufanya shughuli za maendeleo.

iii) Watumishi ambao ni wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) sasa watapata mafao ya mkupuo kwa kikokotoo cha asilimia 40 badala ya asilimia 33 iliyoibua malalamiko na sekta binafsi walioko Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) nao wanatarajiwa kushuhudia ongezeko la mafao ya mkupuo, wakiwa na kikokotoo kipya cha asilimia 35 badala ya asilimia 33 iliyopo kisheria hivi sasa.

iv) Serikali imeendelea kuhakikisha malimbikizo ya kimshahara na yasiyo ya kimshahara ya watumishi wa umma yanalipwa kwa wakati. Kwa miaka mitatu, Sh. bilioni 98.63 zimelipwa kama malimbikizo ya watumishi wa umma.

**b) Changamoto**

i) Idadi ya watu wanaofikiwa na mifumo rasmi ya hifadhi ya jamii ni ndogo sana hususani wanawake

ii) Matumizi yasiyo sahihi ya fedha za mifuko

iii) Kutokuwa na wataalamu wa kutosha kutoa elimu ya mfumo wa hifadhi ya jami

iv) Wafanya kazi wengi waliojiajiri kwenye sekta binafsi hawajiungi na kuchangia katika mifuko ya kijamii na hivyo kukosa pensheni ya uzeeni. Hali hii, inasababisha wazee wengi kuishi maisha magumu kutokana na kushindwa kugharamia huduma muhimu za kijamii.

v) Ucheleweshaji wa mchakato wa malipo ya pensheni kwa wastaafu au watu wenye dharura zinazopelekea kusitisha ajira, hali hii inasababisha mifuko ya Jamii kupoteza mantiki yake ya kusaidia jamii Wakati wa uhitaji.

vi) Serikali na wadau wengine kuendelea kukopa kiasi kikubwa cha fedha bila ya kufanya marejesho kwa wakati, mfano hadi 2024 Serikali imekuwa na deni la hadi Trilioni 2 za Kitanzania, hali inayokwamisha ulipaji wa mafao kwa wakati.

vii) Wafanya kazi wengi wanadai kurudi kwenye kanuni ya awali ya 1/540 badala ya 1/580 inayotumika kwa sasa, ikiwa kanuni hii ya sasa imekuwa na athari za moja kwa moja kwa wanufaika.

## 7.5 MATAMKO

### 7.5.1 Tamko La Ilani Kuhusu Huduma Za Afya

a) Serikali iongeze uwekezaji katika huduma bora za afya za mama, mtoto mchanga na watoto zenye vifaa vya kutosha na watumishi waliobobea.

b) Pia tunasisitiza serikali kuzingatia kasi ya ongezeko la watu wakati wa kutenga fedha kwa sekta hiyo.

c) Kuimarisha mifumo ya uwajibikaji inayohusisha ushiriki wa wananchi katika kufuatilia mikakati na utekelezaji

d) Serikali iendeleze na kuimarisha ushiriki wa jamii katika utoaji wa huduma za afya. Kuziimarisha Bodi za Afya za Halmashauri (CHSB) na Kamati za Usimamizi wa Afya za Vituo ya Afya (FGC).ili zitekeleze majukumu yake kikamilifu

e) Serikali iongeze bajeti ya sekta hadi asilimia 15 kama inavyotakiwa na Azimio la Abuja (2020) na kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya Afya.

f) Waziri wa Fedha atoe maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha zahanati zote na vituo vya afya vina wodi za kujifungulia zilizotengwa na zenye vifaa vya kutosha kama vile vifaa vya kujifungulia, maji, nishati ya mwanga (Umeme au sola), vichomea taka na wahudumu.

g) Huduma za afya kwa wazee, wanawake, watoto na wanaume masikini hasa wa vijijini zitazamwe ikiwa ni pamoja na kushughulikia utekelezaji wa sheria ya Bima ya Afya kwa wote ili kila mtanzania apate matibabu kwa haki na usawa bila ubaguzi.

h) Ili kuboresha hali hii, ni muhimu kukusanya taarifa sahihi kuhusu upungufu wa huduma katika vituo vilivyopo, kuongeza uwekezaji katika sekta ya afya, hasa katika maeneo ya vijijini, na kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi mahitaji ya wanawake, watoto na wanaume masikini. bado kuna changamoto kubwa ya kibajeti katika sekta ya afya, ikiwepo ukoswefu wa rasilimali za kutosha kumalizia miradi iliyokwisha anza huko nyuma.

i) Kurudisha Toto Afya Bima kwa ajili ya kuhakikisha Watoto wote nchini wanapata matibabu

j) Kurekebisha Bango Kitita cha NHIF ili kuboresha ufikiwaji wa huduma za afya hapa nchini na kuondoa matumizi ya fedha taslimu katika matibabu ya umma.

### 7.5.2 Tamko Kuhusu Upatikaji Wa Maji Safi, Usafi Na Mazingira

a) Kuimarisha upatikanaji wa maji safi na kuhamasisha usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini na kupunguza gharama za upatikanaji wa maji ikiwa ni pamoja na gharama za kuunganishiwa huduma za maji pamoja na vifaa;

b) Kujengea jamii uelewa mpana kuhusu usafi na utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji ili kuzuia magonjwa ya mlipuko yatokanayo na maji yasiyo salama;

c) Kila shule ya Msingi iwe na miundombinu salama ya uhakika ya upataikanaji wa huduma za maji safi,afya na usafi wa mazingira (SWASH), ili kuvutia utoaji wa huduma.

d) Serikali itakayoingia madarakani iweke misingi imara ya mamlaka za serikali za Mitaa, kutenga bajeti kwaajili ya kuboresha hali ya upatikanaji wa maji kwenye vituo vya kutolea huduma za afya (hasa kwenye wodi za wazazi), shule, na kusogeza maji karibu na makazi ya watu.

e) Serikali iweke bajeti kwa ajili ya kuwezesha ubunifu na matumizi ya vifaa vya kisasa vya kiteknolojia kama vile pampu na vyoo vya kisasa ili kuimarisha huduma za usambazaji wa maji na utunzaji wa mazingira.

f) Suala la kulinda mazingira, kuthuibiti matumizi ya kuni kwa kupunguza bei za nishati ya kupikia ya gesi asilia ili kupunguza matumizi ya kupikia kwa kuni na mkaa lipewe kipaumbele. Serikali itenge bajeti kwaajili ya kutoa ruzuku kwenye mitungi ya gesi ya kupikia ili kila mwananchi aweze kununua.

g) Serikali itenge bajeti kwaajili ya kujengea uwezo na uelewa kwa Halmashauri, vikundi vya kijamii, Sekta Binafsi na jamii zilizopo kwenye mazingira magumu hususani wanawake, wanaume na hasa jamii za wakulima na wafugaji kuhusu utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

h) Kuhakikisha Mzigo wa kutafuta maji kwa kutembea umbali mrefu unaondolewa, gharama za maji ziwe nafuu ili kila mmoja aweze kuyapata, maji yanayopatikana yawe safi na salama, maji yapatikane katika vituo vya kutolea huduma za afya kama zahanati, Vituo vya afya, na pia maji yapatikane kwenye shule kwaajili ya kuwezesha wasichana kupata masomo vizuri pindi wanapokuwa shuleni. Sambamba na hilo, suala la Usafi wa mazingira na huduma ya maji taka inatakiwa kuboreshwa ili kuwa na jamii yenye ustawi na afya bora.

### 7.5.3 Matamko kuhusu Elimu

a) Uandaliwe mfumo madhubuti wa kuongoza maboresho katika elimu ili kuepuka kuwa na mabadiliko ambayo hayatekelezike kwa ufanisi.

b) Bajeti ya elimu iongezwe ili kuwezesha utekelezaji wa maboresho makubwa yaliyofanyika katika mfumo wa elimu mwaka 2023.

c) Taaluma ya ualimu iongezewe hadhi yake kwa kuhakikisha kuwa bodi ya kitaalamu ya walimu inaanza kazi.

d) Wigo wa uandishi wa vitabu vya kiada utanuliwe kwa kushirikisha wadau wengi zaidi ili kuruhusu ushindani katika kuandika vitabu vyeme ubora na kukuza uwezo wa viwanda vya ndani vya uchapishaji.

e) Elimu ya juu iboreshwe ili baadhi ya vyuo na taasisi ziwe na hadhi ya kimataifa kwa kuweza kudahili wanafunzi kutoka nchi za nje

f) Upimaji wa kitaifa wa stadi muhimu ufanyike badala ya kuweka msisitizo kwenye mitihani peke yake.

g) Utoaji wa elimu katika makazi duni au yasiyo rasmi mjini ni eneo ambalo linapaswa kuingizwa katika mipango wa mandeleo ya elimu

h) Kuhakikisha ulinzi na usalama wa watoto shuleni na kwenye jamii

i) Kuhuisha sheria ya ya elimu ya mwaka 1978 na sheria ya ndoa ya mwaka 1971 ili kuimarisha utekelezaji wa kuwarejesha shuleni wanafunzi walioacha shule kwasababu ya ujauzito

j) Walimu waandaliwe kwa mujibu wa mahitaji ya nchi na kuweka utaratibu wa kuwatumia wahitmu wa ualimu ambao hawajapata ajira

k) Mafunzo ya wakufunzi wa vyuo vya ualimu yaboreshwe ili waweze kufundisha kwa lugha ya Kiswahili

l) Kiswahili kitumike kama lugha ya kufundishia na upimaji kwa wanafunzi walio tayari katika elimu ya sekondari na vyuo.

m) Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 pamoja na kanuni zake zirekebishwe ili kujumuisha yaliyo afikiwa kwenye waraka wa elimu na. 2 wa 2021.

n) Serikali ibadilishe pia vifungu vya sheria ya ndoa ya 1971 kama uamuzi wa mahakama ya rufaa ilivyoagiza ili kutokomeza ndoa za utotoni kama kichochezi kikubwa cha mimba za utotoni kinachochangia ukatizaji wa masomo kwa Watoto wa kike.

o) Huduma ya ushauri na unasihi ihusishe pia wazazi na walezi wa watoto waliokatiza masomo ili kuweza kuwasaidia kukubaliana na hali ya watoto wao na kukubaliana na hali halisi ili waweze kuwapa msaada stahiki wanafunzi hao.

p) Kutenga bajeti ya kujenga mabweni ya wasichana kwenye shule za Kata, au kuongeza shule za sekondari kwa kila kata, ili kupunguza umbali wa kutembelea kwenda shule kwa lengo la kupunguza au kuzia vitendo vya ubakaji, mimba na ndoa za utotoni kwa wasichana.

q) OR-TAMISEMI inandae mwongozo wa uandaaji wa vipaumbele vya Bajeti ngazi ya Halmashauri utakaozitaka Halmasahuri zote kutenga Bajeti kwaajili ya kununua vifaa vya hedhi salama kama vile taulo za kike kwa wasichana wa shule za msingi na sekondari wanaozihitaji ili kubioresha mazingira ya kujifunzia.

r) Kufanya mfumo wa elimu uwe na uwezo wa kutambua vipaji vya Watoto , kuwajengea ujuzi na uwezo wa kuajirika katika nyanjza za kimataifa.

s) Kurudisha na kuboresha michezo katika ngazi zote za elimu hapa nchini

t) Kufanya somo la haki za binadamu kuwa somo la lazima katika ngazi zote za elimu hapa nchini.

### 7.5.4 Matamko Kuhusu Hifadhi za Jamii

a) Kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa hifadhi ya jamii

b) Kuandaa mfumo wa kuwezesha watu wote kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii

c) Serikali kuendelea kutathimi ufanisi wa kanuni mpya ya 1/580 na kubuni njia sahihi za kutatua changamoto hizi.

d) Kuhimiza ulipaji wa madeni kwa wakati katika mifuko husika ili kuleta tija na ufanisi wa mifuko hiyo kwa jamii.

e) Kushughulikia kikamilifu changamoto za ucheleweshaji wa malipo ya pensheni kwa wastaafu na watu wenye dharura za kusitisha ajira.

f) Kuongeza muda wa wastaafu kupata malipo yao ya posho za kila mwezi kwani wengi wao wameendelea kuishi kwa tabu Mara baada ya muda wao wa kulipwa unapokoma na Maisha yakiwa yanaendelea.

# AMANI, USALAMA, UMOJA NA MSHIKAMANO WA TAIFA



SURA YA **NANE**

# AMANI, USALAMA, UMOJA NA MSHIKAMANO WA TAIFA

## 8.0 KUHUSU SURA HII

Sura hii inaangazia masuala ya amani, usalama, umoja na mshikamano wa Taifa. Pia inaangazia jitihada zinazofanywa na nchi katika kudumisha amani, umoja na mshikamano wa Taifa. Vilevile inaangazia changamoto zilizopo katika masuala ya amani, umoja na mshikamano wa Taifa kwa lengo la kuwezesha kutatuliwa kwa changamoto hizo ili kujenga Taifa imara lenye uchumi usioyumba.

Toka kuasisiwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1964, Tanzania imeendelea kutambulika kuwa ni kisiwa cha amani na utulivu duniani na katika bara zima la Afrika. Tanzania inaendelea kuwa na nafasi ya juu katika masuala ya amani duniani na nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kwa mujibu wa ripoti ya Masuala ya Amani Duniani ya Mwaka 2024 (Global Peace Index 2024), Tanzania iko nafasi ya 7 kwa nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara na nafasi ya 65 kidunia ikiwa imepanda kwa nafasi 11. Tanzania imefanikiwa kutokomeza matukio mengi yaliyokuwa yakihatarisha amani na usalama kama vile matukio ya ujambazi wa kutumia silaha, utekaji na mauaji katika maeneo mbali mbali. Kutokana na utulivu huu, Tanzania imekuwa ni kimbilio na kivutio cha wageni wengi ikiwa ni pamoja na wahitaji kama vile wakimbizi kutoka nchi za Jirani.

Ili kuendelea kusifika kuwa nchi ya amani, Tanzania inahitaji mikakati na mbinu jumuishi katika misingi ya mshikamano kutatua changamoto zinazoathiri amani, usalama, umoja na mshikamano wa Taifa. Hivyo, AZAKI zinawataka viongozi kuwekeza nguvu zaidi kwenye kuimarisha na kulinda amani, usalama, umoja na mshikamano ili kujenga Taifa imara lenye upendo, kuheshimiana na uchumi usioyumba.

## 8.1 HALI YA UTEKELEZEZAJI WA ILANI YA AZAKI YA MWAKA 2019-2024

### 8.1.1 Amani na Usalama

**a) Jitihada Zilizofikiwa**

i) Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazosifika katika kudumisha amani, usalama, umoja na mshikamano wa Taifa.

ii) Tanzania inajivunia jinsi ambavyo imeweza kutatua migogoro yake yenyewe kwa njia ya mazungumzo bila uhitaji wa kutumia silaha au msaada wa nchi nyingine. Kwa mfano, Tanzania imeweza kudhibiti matendo ya wizi na ujambazi wa kutumia silaha; utekaji wa magari na abiria, mauaji, uvunjaji wa maduka na mabenki. Matukio haya yameweza kudhibitiwa na vyombo vya dola kwa ushirikiano na wananchi kupitia programu maalumu iliyoanzishwa na jeshi la polisi inayojulikana kama "Polisi jamii".

iii) Hali kadhalika, nchi imefanya jitihada za makusudi katika kujenga uwezo wa wananchi kushiriki katika kutunza amani ikiwemo, kutambua viashiria vya mapema vya uvunjifu wa amani, pia kufanya maboresho ya kisheria, kimuundo na kiutawala kwa kuongeza nguvu kwenye maeneo hatarishi kwa amani ya nchi hususani maeneo ya mipakani.

iv) Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Bungeni wakati wa uwasilishaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya 2024/2025, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 makosa makubwa ya Jinai yaliyoripotiwa katika Vituo vya Polisi yamepungua kutoka 45,485 hadi 43,146 sawa na asilimia 5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Hii inaonyesha kuimarika kwa jitihada za kuhakikisha ulinzi wa raia na mali zao kunakopelekea amani kutawala nchini na kuwezesha wananchi kufanya kazi zao za kiuchumi na kijamii.

v) Kuundwa kwa Tume Maalumu ya Kuangalia jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai, ni hatua muhimu iliyochukuliwa na serikali ili kuboresha mifumo wa haki jinai nchini. Mifumo hii ikiboreshwa ipasavyo kama ilivyopendekezwa na Tume hiyo, itachagiza uwepo wa amani, usalama, umoja na mshikamano wa kitaifa.

vi) Falsafa ya R nne pia ya Rais Samia imechangia kurudisha amani ya Taifa ambayo ilitoweka katika awamu ya tano kutokana na sehemu kubwa ya jamii kuumizwa na utendaji wa awamu ile ya tano.

**b) Changamoto**

i) Hata hivyo, hivi karibuni yamejitokeza matukio mbalimbali ya uvunjifu wa amani, usalama, umoja na mshikamano wa kitaifa. Matukio ambayo yamegusa wabunge wa vyama vyote, wananchi, waandishi wa habari, watetezi wa Haki za Binadamu, wanasiasa, wanamuziki wakizuiwa kutumia haki yao ya uhuru wa kujieleza, wakitekwa, kupigwa na kuumizwa, na hata kuuawa. Matukio kama haya pia yameripotiwa kwa upande wa Zanzibar na yamekuwa yakihusishwa na masuala ya kisiasa na visasi vya kibiashara.

ii) Matukio mengine ni kama kuhamishwa kwa wakazi wa KIA – Kilimanjaro na wakazi wa Ngorongoro kwenda Msomera – Morogoro na ambapo kunaripotiwa kwamba kumeleta migogoro katika eneo la Msomera na hata kuathiri amani, usalama, umoja na mshikamano katika eneo hayo. Matukio haya yanaendelea kuathiri amani na utulivu kwa kiasi kikubwa hapa chini.

iii) Pia limeibuka wimbi la jeshi la polisi kuhusishwa na matukio ya utekaji wa wananchi, waandishi wa habari, watetezi wa haki za binadamu kwa lengo la kuwatesa na hata kuwaua. Mara kadhaa kumeripotiwa taarifa za watu kutekwa au kupotea katika mazingira ya kutatanisha, ambayo yamekuwa yakihatarisha hali ya usalama na kuzua taharuki miongoni mwa wananchi. Matukio haya yameripotiwa Tanzania Bara na Zanzibar. Haya ni baadhi ya masuala yanayofifisha amani, usalama, umoja na mshikamano nchini.

iv) Japokuwa kuna taarifa kwamba mapendekezo ya Tume ya Haki jinai yameanza kufanyiwa kazi, lakini bado utekelezaji huo haujaanza kuonekana kivitendo. Bado kuna maeneo na sheria nyingi ambazo hazijafanyiwa marekebisho au kutungwa ili kuakisi utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai.

### 8.1.2 Umoja na Mshikamano

**a) Jitihada Zilizofikiwa**

i) Serikali ya awamu ya sita chini ya Mh. Dkt Samia Suluhu Hassan imekuja na falsafa ya 4R kwa maana ya maridhiano, ustahimilivu, mabadiliko na kujenga upya ambayo inalenga kudumisha umoja na mshikamano kwa nchi.

ii) Utekelezaji wa falsafa hii umeshuhudiwa kwa vitendo ambapo tumeona mabadiliko mbalimbali yaliyofanywa katika sheria mbalimbali ili kuendana na falsafa hii. Kwa mfano, marekebisho ya sheria zinazosimamia masuala ya chaguzi, sheria ya Habari, sheria za uwekezaji na manunuzi ya umma, sheria za kodi, sheria ya afya na nyingine nyingi.

iii) Ushirikishwaji wa wananchi katika masuala muhimu ya nchi ni njia mojawapo ya kuendeleza umoja na mshikamano kwa nchi. Kwa mfano ushirikishwaji katika kuandaa dira ya Taifa ya maendeleo 2050 ni alama thabiti inayoonyesha kwamba serikali inaheshimu mchango wa wananchi katika maendeleo ya nchi yao na hivyo inapelekea kuwepo kwa umoja na mshikamano kama nchi.

iv) Kuundwa kwa Kikosi Kazi cha Kuratibu Maoni ya Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa nchini Tanzania ni hatua muhimu ambayo ilichukuliwa na serikali ili kuboresha demokrasia, mazingira ya wanasiasa na vyama vya siasa kufanya shughuli zao kwa uhuru. Hii ilipelekea kuondolewa kwa makatazo ya vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara na mikutano yao ya ndani. Hali hii inachagiza kuongezeka kwa amani, usalama, umoja na mshikamano wa kitaifa.

**b) Changamoto**

i) Hata hivyo, mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Kuangalia hali ya siasa hayajafanyiwa kazi yote ipasavyo. Tanzania imeendelea kuwa na sheria zilezile zinazonyima uhuru kamili wa vyama vya siasa kufanya shughuli zao bila kuingiliwa na vyombo vya usalama.

j) Pia bado kumeendelea kuwepo kwa sheria mbalimbali zinazogandamiza uhuru wa kujieleza, kukutana, kushirikiana na kujumuika. Marekebesho yaliyofanyika hivi karibuni katika sheria za masuala ya chaguzi zimeendelea kulalamikiwa na wananchi kwamba bado zina changamoto nyingi ambazo hazijatatuliwa ikiwa na Pamoja na TAMISEMI kuendelea kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

ii) Matukio mengi ya waziwazi ya uvunjaji wa haki za wananchi yamechangia kwa kiasi kikubwa kufifisha umoja na mshikamano katika jamii. Mfano haki za wafugaji, wakulima, wafanya biashara, walimu, wafanyakazi, wastaafu na makundi maalumu kama wanawake, watoto, walemavu na vijana zimekuwa zikiendelea kukiukwa katika maeneo mbalimbali na kupelekea wananchi kutokuwa na imani na serikali yao au viongozi wao. Hali hii hupelekea kuwepo kwa mifarakano kadha wa kadha katika jamii. Kuminywa kwa haki hizi hakuwezi kuleta watu pamoja na wakawa na mshikamano. Hivyo basi, juhudi za makusudi zinahitajika ili kuhakikisha haki zinatolewa kwa usawa ili kuleta umoja wa kitaifa na mshikamano.

iii) Baadhi ya viongozi wa serikali wameshindwa kutekeleza kwa vitendo falsafa ya 4R na kupelekea kuonekana matendo ya waziwazi yanayofifisha falsafa hiyo. Kwa mfano matukio ya hivi karibuni

ya kukamatwa kwa viongozi wa upinzani na vyama vya upinzani kukutazwa kufanya mikutano yao ya hadhara na ya ndani ni ishara kwamba falsafa hiyo ya 4Rs haitekelezwi kwa utimilifu hali inayopelekea kuvunjika kwa amani, umoja na mshikamano.

iv) Ushirikishwaji wa wananchi katika mambo muhimu ya kitaifa bado ni hafifu na ushirikishwaji huo unafanywa kwa nia ya kuonekana wananchi wameshiriki lakini mawazo yao ya msingi mara nyingi yamekuwa yanapuuzwa. Hali hii inapelekea kupunguza ari ya wananchi kushiriki katika mambo muhimu ya kitaifa na kupelekea kufifisha umoja na mshikamano.

v) Kutengwa na kunyimwa kwa huduma za kijamii kwa jamii ya wamasai katika Tarafa ya Ngorongoro Wilayani Ngorongoro kunachangia chuki katika jamii.

## 8.2 TAMKO LA ILANI KUHUSU AMANI, USALAMA, UMOJA NA MSHIKAMANO

Ili kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa kisiwa cha amani na kufikia Tanzania tuitakayo, AZAKI tunawataka viongozi wote kuzingatia na kutekeleza yafuatayo:-

### 8.2.1 Amani na Usalama

a) Kuwajibisha vyombo vya dola kulinda raia wote na mali zao bila upendeleo

b) Kuundwa chombo cha kusimamia weledi wa jeshi la polisi na vyombo vya dola venye mamlaka ya kusimamia sheria nchini kama ilivyopendekezwa na Tume ya kuboresha taasisi za Haki Jinai.

c) Katiba iwe na Ibara inayoweka na kusisitiza ulinzi, amani, usalama, umoja na mshikamano wa kitaifa.

d) Serikali na Viongozi walazimike kuchukua hatua za makusudi ili kulinda haki za AZAKI, watetezi wa haki za binadamu, waandishi wa habari, wafanyakazi, wafanya biashara, wafugaji, wakulima, wastaafu, wavuvi, wanaharakati wa kisiasa na watu wote kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania.

e) Kuwepo mikakati ya kutambua migogoro mapema kabla haijatokea au kabla haijaleta madhara makubwa katika jamii kwa kuanzisha kamati za maridhiano.

f) Wote wanaohusika na ukiukwaji wa haki za binadamu wawajibishwe kwa mujibu wa sheria bila kuwalinda

g) Matukio yote ya utekaji yakomeshwe nchini na wote wanatuhimiwa wakamatwe na kufukishwa mahakamani

h) Tanzania iridhie mikataba ya kupinga ukatili ya upoteaaji wa watu ( Connvention against torture and convention on enforced disappearance)

### 8.2.2 Umoja na Mshikamano

a) Kuhuisha sera na sheria zinazokinzana katika kulinda na kudumisha umoja na mshikamano wa kitaifa.

b) Kutekeleza kwa vitendo falsafa ya 4Rs ili kudumisha umoja na mshikamano

c) Kushirikisha wananchi katika maendeleo ya nchi yao na kuhakikisha michango yao ya msingi inaakisiwa katika mipango na vipaumbele vya serikali ili kujenga na kudumisha umoja na mshikamano

d) Kuhakikisha fedha na rasilimali za nchi zinatumika na kunufaisha wananchi wote bila ubaguzi wa maeneo ili kuchochea umoja na mshikamano

e) Kufanyia kazi mapendekezo yote yaliyotolewa na Kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa Demokrasia ya vyama vingi vya Siasa na yale ya Tume maalumu ya kuangalia jinsi ya kuboresha taasisi za Haki jinai ili kujenga na kudumisha umoja na mshikamano.

# DIPLOMASIA NA MAHUSIANO YA KIMATAIFA



SURA
YA **TISA**

# DIPLOMASIA NA MAHUSIANO YA KIMATAIFA

## 9.0 KUHUSU SURA HII

Sura hii inaangazia jinsi Tanzania inavyoshirikiana na mataifa mengine na taasisi za kimataifa ili kufanikisha malengo yake ya kitaifa. Inalenga kueleza mafanikio na changamoto katika mahusiano ya kidiplomasia, na kutoa mapendekezo ya kuimarisha diplomasia ya kiuchumi na ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa maendeleo endelevu ya nchi.

Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania iliyotungwa mwaka 2001, na kuhuishwa 2015 na vile vile kufanyiwa tathmini 2021-2024 inalenga kurekebisha juhudi za kidiplomasia za nchi ili ziweze kutumikia vyema maslahi ya kiuchumi, kisiasa, na kijamii katika anga za kimataifa. Kwa kutilia mkazo diplomasia ya kiuchumi, sera hii inalenga kuboresha ushiriki wa Tanzania katika masuala ya kikanda na kimataifa, na hivyo kuchochea maendeleo endelevu na ushirikiano wa kimataifa.

## 9.1 UTEKELEZAJI WA ILANI YA AZAKI YA MWAKA 2019-2024

### 9.1.1 Uwakilishi wa Nchi Katika Mikutano ya Kikanda

#### a) Jitihada Zilizofikiwa

Katika muktadha wa kikanda, mahusiano ya Tanzania na majirani zake, ikiwa ni pamoja na Kenya na Msumbiji, yameimarishwa zaidi chini ya uongozi wa Rais Dr. Samia Suluhu Hassan. Tanzania inashiriki vyema jukwaa la wazi la kukuza uongozi wa taasisi kwa kuridhia mikakati mbalimbali kama vile Mkataba wa Biashara Huria, au *Tripartite Free Trade Agreement (TFTA)*, kurejesha ushiriki wa kikamilifu katika masuala ya usuluhishi na kutatua migogoro, na kuonyesha kujiunga tena na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na kuhusu kujiunga tena Mpango wa Ubia wa Serikali Huria yaani Open Government Partnership (OGP).

Tanzania imeendelea kutimiza wajibu wake wa kuwasilisha ripoti kwa Tume ya Afrika kuhusu hali ya haki za binadamu nchini. Tanzania imekuwa ikishiriki katika vikao vya Tume ya Afrika, ikitoa maoni na taarifa kuhusu haki za binadamu. Pia, Tanzania imepokea na kutekeleza baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na Tume hiyo kwa ajili ya kuboresha hali ya haki za binadamu nchini.

Katika ushiriki wa mikutano kikanda, Tanzania imeendelea kushiriki na kuratibu mikutano kama sehemu ya kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia:

i. Tanzania imekuwa ikishiriki katika vikao vya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR) ambapo imewasilisha ripoti zake za utekelezaji wa haki za binadamu na kujibu maswali kutoka kwa wajumbe wa kamati.- Vilevile mwaka 2023 Tanzania ilikuwa mwenyeji wa vikao vya tume hii. Ushiriki huu umeimarisha sifa ya Tanzania katika kulinda na kukuza haki za binadamu katika awamu ya sita.

ii. Tanzania ni mshiriki hai wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na SADC, ikijitahidi kuboresha ushirikiano wa kikanda katika nyanja za uchumi, siasa, na jamii. Kupitia SADC, Tanzania imeshiriki katika miradi ya kikanda yenye lengo la kuboresha miundombinu, biashara, na maendeleo endelevu.

iii. Tanzania imekuwa ikishiriki kikamilifu katika mikutano na vikao vya Umoja wa Afrika (AU) na kuchangia mijadala muhimu kuhusu amani, usalama, maendeleo ya kiuchumi, na masuala ya haki za binadamu barani Afrika. Ushiriki huu umeongeza ushawishi wa Tanzania katika sera za bara.

iv. Tanzania pia imewasilisha ripoti kuhusu utekelezaji wa mikataba ya kikanda kama vile Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) na kuanza mchakato wa uwasilishaji wa taarifa kuhusu Mkataba wa Mapambano Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia na Unyanyasaji (Maputo Protocol).

v. Serikali ya Tanzania inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM).

**b) Changamoto**

i. Ingawa Tanzania ni mwanachama wa EAC, utekelezaji wa baadhi ya maamuzi kutoka katika mahama pamoja na vyombo vingine vya EAC umekuwa na kasi ndogo kutokana na kukosekana kwa ushirikiano wa kutosha kati ya serikali kuu, taasisi za umma, na sekta binafsi. Hii imeathiri utangamano wa biashara na usafirishaji wa bidhaa huru katika ukanda wa EAC.

ii. Tanzania imeshindwa kutekeleza kikamilifu Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi (EPA) kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Umoja wa Ulaya (EU). Hii ni kutokana na mabadiliko ya sera na hofu juu ya athari kwa sekta za ndani, kama vile viwanda vya ndani na kilimo. Hatua hii imepelekea Tanzania kuchelewa kusaini au kutekeleza kikamilifu mkataba huu, huku nchi nyingine za EAC zikichukua hatua mbele.

iii. Tanzania imekuwa ikikumbana na changamoto ya ufuatiliaji na usimamizi duni wa utekelezaji wa maamuzi ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACPR) Pamoja na Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki (EACJ) ambazo zina makao yake makuu Arusha, Tanzania. Baadhi ya maamuzi ya mahakama hizi hayajatekelezwa kikamilifu na serikali, jambo linaloleta changamoto katika utekelezaji wa haki za binadamu kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo Tanzania imeridhia.

iv. Pamoja na kuanza mchakato wa uwasilishaji wa taarifa kuhusu Mkataba wa Mapambano Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia na Unyanyasaji (Maputo Protocol) mwaka 2021, bado Serikali ya Tanzania haijakamilisha mchakato huo mpaka.

v. Tanzania hadi sasa haijarudi au kuridhia wananchi binafsi na mashirika ya kijamii kuendelea kupeleka mashauri katika mahakama ya Afrika. Tanzania ilijitoa katika mahakama hii ambayo ina makao makuu yake Mjini Arusha mwaka wa 2019.

Changamoto hizi zinaathiri uwezo wa Tanzania kunufaika kikamilifu na ushirikiano wa kimataifa na kikanda. Kupitia ushirikiano wa karibu na wadau mbalimbali, pamoja na kuimarisha sera na taasisi, Tanzania inaweza kuimarisha utekelezaji wa mikataba na maamuzi ya kimataifa na kikanda.

### 9.1.2 Ushiriki wa Tanzania Katika Michakato ya Kimataifa

#### a) Jitihada Zilizofikiwa

i. Tanzania inaendelea kutekeleza baadhi ya mikataba ya kimataifa kama Mkataba wa Haki za Mtoto (CRC), Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW); Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi (Paris Agreement); Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR); Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni (ICESCR); Mkataba wa Umoja wa Mataifa Dhidi ya Rushwa (UNCAC) pamoja na mingine japokuwa kumekuwa na changamoto juu ya utekelezaji kamili.

ii. Tanzania imekuwa ikiwajibika kuwasilisha ripoti za hali ya haki za binadamu kwa kamati mbalimbali za Umoja wa Mataifa kama Kamati ya Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) na Kamati ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni (ICESCR). Ripoti hizi zinachambua hatua zilizopigwa na serikali katika kutimiza haki mbalimbali za binadamu nchini.

iii. Tanzania inashiriki katika mchakato wa Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa (UPR) kwa kuwasilisha ripoti ya hali ya haki za binadamu nchini. Katika duru ya tatu, Tanzania iliridhia mapendekezo 187 kati ya 252 yaliyotolewa mwaka 2021. Ushiriki huu umewezesha Tanzania kupokea mapendekezo na ushauri kutoka kwa nchi nyingine kuhusu jinsi ya kuboresha hali ya haki za binadamu.

iv. Vilevile Tanzania ilishiriki katika mchakato wa VNR wa Umoja wa Mataifa, ambapo ilitoa tathmini ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) mpaka mwaka 2023. Ripoti hii ya VNR Imeonyesha maendeleo yaliyopatikana na changamoto zilizopo, na kuimarisha ushirikiano na washirika wa maendeleo.

v. Tanzania ilishiriki katika kikao cha 78 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Jijini New York Marekani na kuwasilisha taarifa yake kuhusu utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

vi. Lakini vilevile Tanzania ni mshirika mzuri wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake (CSW) ya Umoja wa Mataifa pamoja na Jukwaa la Usawa wa Kizazi (Generation Equality Forum).

### b) Changamoto

i. Ingawa Tanzania iliridhia mapendekezo mengi (187) 167 yakikubaliwa yote na 20 yakikubaliwa kwa kiasi katika duru ya tatu ya UPR, kutekeleza mapendekezo haya mara nyingi kumekua changamoto kutokana na ukosefu wa mikakati ya utekelezaji, rasilimali, na ushirikiano wa vyombo vya serikali. Kwa upande wa SDGs (Mpango wa Maendeleo Endelevu 2030), ingawa Tanzania imewasilisha ripoti za VNR na kupokea ushauri, utekelezaji wa Malengo ya SDGs mara nyingi hukumbana na changamoto za upungufu wa rasilimali, uratibu duni kati ya wadau, na usimamizi wa miradi.

ii. Tanzania inakukumbana na changamoto katika kutekeleza ahadi za kibiashara au kiuchumi kutokana na hali ya uchumi wa ndani, mifumo ya ushuru, au viwango vya masharti yasiyokubalika.

iii. Lakini vilevile Tanzania bado haijawasilisha ripoti ya baadhi ya Mikataba muhimu iliyoridhiwa mfano Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu

wenye Ulemavu (CRPD) ambao uliridhiwa tangu 2009. Ingawa Tanzania imeridhia mikataba ya kimataifa kuhusu haki za binadamu, utekelezaji wa ahadi hizi mara nyingi huhitaji kubadilisha sera za kitaifa, ambayo imekua changamoto kutokana na maslahi ya kisiasa na jamii.

iv. Kwa upande wa Mikataba ya Mabadiliko ya Tabianchi mfano the Paris Agreement, Tanzania imekua nyuma kutokana na kutokana na vikwazo vya kifedha, ukosefu wa teknolojia, na hali ya hewa.

### 9.1.3 Diplomasia ya Uchumi

#### a) Jitihada Zilizofikiwa

Katika diplomasia ya uchumi, Serikali imefanikiwa kuandaa makongamano mbalimbali yaliyolenga kuimarisha diplomasia ya uchumi ikiwa na pamoja na Kongamano la Biashara na Uwekezaji baina ya Tanzania na Uturuki lililofanyika mjini Istanbul, Uturuki April 2024; Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Ubeligiji May 2024; mwezi Mei 2024 Serikali iliratibu na kufanikisha kuanza kwa majadiliano ya kibiashara baina ya Tanzania na Marekani; Kongamano la Biashara baina ya Uganda na Tanzania May 2024; Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Brazil mwezi April 2024, Pamoja na Kongamano la Uchumi na masuala ya kibinadamu baina ya Afrika na Urusi Julai 2023.

Tanzania imeendelea kukuza Diplomasia yake kiuchumi ambapo imeratibu na kushiriki mikutano kadhaa iliyolenga kukuza diplomasia ya uchumi katika mifano michache ifuatayo:

i. Tanzania ilikua mwenyeji wa mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika uliojumuisha Marais na Wakuu wa Nchi na Wadau wa Kilimo na Chakula kutoka nchi mbalimbali za Afrika na kwingineko duniani uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, Septemba 7, 2023.

ii. Tanzania ilishiriki vyema katika mkutano wa Viongozi wa Afrika na Marekani uliofanyika Jijini Washington DC nchini Marekani mwezi Desemba 2022.

iii. Kama kituo cha Utalii kwa Afrika, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa Kimataifa wa 23 wa Baraza la Utalii Duniani (WTTC) uliofanyika jijini Kigali, Rwanda Mwezi Novemba, 2023

iv. Mahusiano haya yameleta mafanikio makubwa makubwa ambayo Tanzania imepata kupitia diplomasia ya uchumi, ikijikita katika kuvutia uwekezaji, kuboresha miundombinu, na kukuza biashara ya kikanda. Kwa mifano michache tu;

v. Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa Kigeni (FDI) umeongezeka kwa asilimia 20 hadi kufikia dola za Kimarekani bilioni 1.1 mwaka 2022, ikilinganishwa na dola bilioni 0.9 mwaka 2021.

vi. Katika miundombinu, Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza umegharimu zaidi ya Shilingi trilioni 14.2, na unatarajiwa kuimarisha usafirishaji wa bidhaa na kupunguza gharama za usafirishaji kwa asilimia 40. Mradi wa Bwawa la Julius Nyerere lenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 za umeme pia ni mfano mkubwa wa mafanikio ya diplomasia ya kiuchumi, ukiwa umegharimu zaidi ya Shilingi trilioni 6.5.

vii. Katika Sekta ya Utalii kwa mwaka 2024, Tanzania inatarajia kupokea watalii zaidi ya milioni 2.0, huku mapato kutoka sekta hiyo yakikadiriwa kufikia dola bilioni 3.1. Kuongezeka kwa watalii kunachangiwa na kampeni za kimataifa za utalii na kuboresha huduma za utalii nchini.

viii. Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (EACOP): Mradi wa bomba hili kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania unatarajiwa kuzalisha zaidi ya ajira 10,000 na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika mapato ya serikali kupitia ushuru na kodi.

ix. Hii ni matokeo ya juhudi za kuboresha mazingira ya biashara na kuimarisha usalama wa uwekezaji.

**b) Changamoto**

i. Kukosekana kwa Utaalam wa Kisasa mfano katika ripoti ya WEF Global Competitiveness Index 2023, Tanzania ilishika nafasi ya 113 kati ya nchi 141 katika sekta ya ujuzi wa nguvu kazi. Upungufu huu wa utaalam unakwamisha maendeleo katika sekta za teknolojia, viwanda, na huduma, na hivyo kupunguza uwezo wa Tanzania kunufaika na diplomasia ya uchumi.

ii. Ushindani wa Kikanda mfano, Kenya inashika nafasi ya juu katika uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni (FDI) katika EAC, ambapo ilivutia FDI yenye thamani ya dola bilioni 2.4 mwaka 2023, ikilinganishwa na Tanzania iliyo na dola bilioni 1.5. Ushindani huu unafanya Tanzania kulazimika kuboresha zaidi mazingira yake ya biashara ili kushindana kikamilifu.

iii. Madeni na Mipango ya Kifedha, Mfano Kufikia mwisho wa mwaka 2023, deni la Taifa la Tanzania lilifikia dola za Kimarekani bilioni 39.2, ikiwa ni asilimia 40 ya Pato la Taifa (GDP). Hii imeweka shinikizo kwa serikali katika kutafuta mikopo zaidi ili kufadhili miradi ya miundombinu, jambo linaloweza kuathiri utekelezaji wa sera za kiuchumi kwa muda mrefu.

iv. Migogoro ya Kikanda mfano, Mgogoro wa usalama Mashariki mwa DRC imeathiri biashara kupitia Bandari ya Dar es Salaam na usafirishaji wa bidhaa kupitia reli ya TAZARA.

## 9.2 TAMKO LA ILANI

### 9.2.1 Tamko Kuhusu Uwakilishi wa Nchi Katika Michakato na Mikutano ya Kimataifa na Kikanda

a) Tunahimiza serikali na viongozi kushiriki kikamilifu katika majukwaa ya kikanda na kimataifa ili kuhakikisha maslahi ya Tanzania yanalindwa na kuendelezwa lakini pia, mipango ya maendeleo haipishani na mipango ya kikanda na kidunia.

b) Tunatoa wito kwa serikali na viongozi kufuatilia na kuwezesha utekelezaji wa mikataba ya kimataifa, kuhakikisha Tanzania inafuata viwango vya kimataifa na inapata msaada unaohitajika kwa utekelezaji.

c) Tanzania kurejea kwenye Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ili kuimarisha ushirikiano katika kulinda haki za binadamu na kuboresha hali ya haki za binadamu nchini.

d) Tanzania kurejea tena kwenye Mpango wa Ubia wa Serikali Huria yaani Open Government Partnership (OGP) kama ilivyoahidi mwaka 2023

e) Serikali kuhakikisha kuwa taarifa za haki za binadamu zinatolewa kwa uwazi na kwa wakati. Tunasisitiza umuhimu wa kuwepo kwa mifumo thabiti ya ufuatiliaji, uchunguzi, na utoaji wa taarifa huru kuhusu hali ya haki za binadamu, ili kuimarisha uwajibikaji na kulinda haki za raia wote.

f) Serikali iendelee kuwekeza zaidi katika elimu na mafunzo ya kiufundi na kitaaluma, hasa katika sekta za teknolojia, sayansi, na uhandisi. Pia, serikali inaweza kuanzisha mpango wa kuvutia wataalam wa Kitanzania walioko ughaibuni kurudi na kuchangia katika maendeleo ya Taifa.

g) Ili kushindana kikamilifu na nchi jirani kama Kenya katika kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni (FDI), Tanzania inahitaji kuboresha mazingira ya biashara kwa kuondoa urasimu, kuboresha miundombinu, na kuhakikisha utulivu wa kisiasa na kisera. Serikali inapaswa pia kuanzisha vivutio maalum kama vile kodi za chini kwa wawekezaji wakubwa na kuimarisha maeneo maalum ya uwekezaji yaani Special Economic Zones (SEZs) ili kuongeza ushindani wa kikanda.

h) Tanzania inapaswa kuimarisha diplomasia yake ya kikanda na kushirikiana na jumuiya za kikanda kama SADC na AU ili kutafuta suluhu za kudumu kwa migogoro katika nchi jirani kama DRC. Kuanzisha majadiliano ya kibiashara na serikali za nchi jirani kuhusu mikakati ya kukabiliana na athari za migogoro itasaidia kupunguza usumbufu wa biashara na kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kunufaika na ushirikiano wa kikanda.

### 9.2.2 Tamko Kuhusu Diplomasia ya Uchumi

a) Tunatoa wito kwa serikali na viongozi watakaochaguliwa kuhakikisha diplomasia ya kiuchumi inakuwa kipaumbele, kwa kuvutia uwekezaji wa kigeni na kuimarisha biashara ya kimataifa ili kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi.

b) Tunasisitiza serikali na viongozi kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa sera za kidiplomasia. Maamuzi yanapaswa kufanywa kwa uwazi na kushirikisha wananchi katika mchakato wa maamuzi bila kutoa matamshi yanayohatarisha mahusaiano ya kidiploamsia.

c) Tunahimiza serikali na viongozi kuhakikisha sera za mambo ya nje zinajumuisha na kuakisi maslahi ya Watanzania wote, ikiwemo makundi ya pembezoni na yale yasiyokuwa na uwakilishi wa kutosha.

d) Kukuza Amani, Usalama, na Ushirikiano, tunatoa wito kwa serikali na viongozi kuchukua hatua za kukuza amani, usalama, na ushirikiano ndani ya kanda na duniani kote, ili kujenga mazingira imara ya ukuaji na maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

e) Serikali na viongozi kuitekeleza kikamilifu Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania, ili kuhakikisha mahusiano ya kimataifa yanawanufaisha wananchi kwa ujumla na kuchangia maendeleo endelevu ya Taifa. Balozi za Tanzania kuwasilisha mipango kazi yao na ripoti  za utendaji kazi zinazoonyesha zimeinufaisha vipi Tanzania.

SURA
YA **KUMI**

# WITO KWA MAKUNDI MBALIMBALI

## 10.1 KUHUSU SURA HII

Kufuatia ukweli kwamba uchaguzi ni mchakato unaohusisha karibu kila mtu na kila kundi au wadau mbalimbali, hivyo haina budi kila mdau kushiriki na kutekeleza ipasavyo majukumu yake sawa na sheria na taratibu za nchi zinavyowaongoza. Sehemu zilizopita za ilani hii zimeeleza kwa kina masuala kadhaa ambayo serikali kupitia vyombo vyake vya dola na vyombo vya usimamizi wa uchaguzi vinapaswa kufuata. Aidha viongozi watarajiwa wametakiwa kuelekeza mawazo na uwezo wao katika masuala mbalimbali ambayo AZAKI Zimebainisha katika matamko ya ilani hii ya 2024/2029. Sehemu hii kuelekea mwisho wa ilani inaeleza masuala ya ziada kwa kwa kuzingatia wadau wengine ambao hawakutajwa zaidi katika maelezo yaliyotangulia. Ikiwa pia ni sehemu ya hitimisho la ilani hii.

## 10.2 Wito kwa kwa makundi mbalimbali

### 10.2.1 Wananchi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Tanzania Bara.

a) Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni wadau muhimu zaidi na wahusika zaidi katika uchaguzi wa wa serikali za Mitaa 2024 na uchaguzi na Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2025. Itakumbukwa kuwa katika uchaguzi mkuu mwaka 2020, jumla ya wananchi milioni **29.8** waliojiandikisha kupiga kura, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza watanzania milioni **14.8** sawa na asilimia **49.8** hawajakujitokeza kupiga kura. Hali hii inawanyima haki wao wenyewe kwa kumpata kiongozi mwenye sifa na wamtakaye, Hivyo basi ni Wito wa AZAKI kuhakikisha yakua, Watanzania wote wenye sifa za kupiga kura wanajitokeza siku hiyo ili kuweza kupata viongozi wanaostahili.

b) Ili kuwa na viongozi bora na dhabiti, watakao weza tulitea Tanzania tuitakayo 2024-2029, Wananchi wanatakiwa kusikiliza sera kikamilifu na kuzifanyia kazi kikamilifu ikiwa ni kupitia kushiriki katika kampeni za wagombea wote kutoka vyama vyote vya siasa ili wakati wa upigaji kura wafanye maamuzi sahihi.

c) Tunapoelekea chaguzi za 2024/2025 wito wa AZAKI kwa wananchi wote ni kutaka wajenge pia wajengewe uelewa kwamba viongozi wasiofaa mara nyingi huweza kupita na kuteuliwa hadi kwenye nyadhifa za umma kutokana na kutojali kwa wapiga kura kama watu wengi wanavyofanya kutojitokeza kupiga kura.

d) Ili kuwa na Viongozi bora kwa masilahi ya Umma, Wananchi wote wanajukumu la kupinga vitisho vyovyote vya wanasiasa ambavyo vinaweza kupoteza haki yao ya kupigia kura viongozi wanaowapenda na wenye vigezo sahihi.

e) Kuepuka vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi na kuchagua watu bila kutegemea rushwa

f) Baada ya viongozi waliochaguliwa kuapishwa, wananchi wanapaswa wawe tayari kushiriki kila hatua za mchakato wa maendeleo badala ya kuwaacha wanasiasa waamue na kutekeleza miradi yao ya maendeleo kwa niaba yao kwani hii hufifisha hali ya uwazi na uwajibikaji wa viongozi hao.

g) Wananchi ni lazima wafuatilie kwa karibu utendaji kazi wa viongozi na watendaji wao, na wachukue hatua kwa wale ambao hawawezi kutekeleza na kutimiza ahadi zao.

h) Tunapoelekea Chaguzi za 2024/2025 Wananchi wanapaswa kuepuka kujihusisha na vitendo vyovyote vya vurugu na lazima wakatae kutumiwa kisiasa kwa lengo la kuleta maslahi ya kisiasa ya mgombea fulani.

i) Kama ilivyo sisitizwa katika ilani ya AZAKI 2019-2024, bado ni wito wetu kwamba, wananchi ni lazima washiriki kikamilifu kufuatilia ilani ya uchaguzi ya vyama vya kisiasa, kusikiliza ahadi mbalimbali alizotoa mgombea ili wakati wa upigaji kura waweze kufanya maamuzi sahihi.

### 10.2.2 Kwa Vyama vya Siasa

a) Ni Wito wa AZAKI kwa Vyama vya kisiasa kufanya kampeni zao kwa njia ya kistaarabu kwa kuheshimu kanuni, sheria na siasa za ushindani zinazotambua na kuridhia matokeo yoyote.

b) Katika chaguzi za 2024/2025 Hakuna mtu anayepaswa kutishwa, kutukanwa au kubaguliwa wakati wa kampeni badala yake kampeni zinatakiwa ziendeshwe kwa mtindo wa kistaarabu na ambazo zinaheshimu na kuzingatia maadili ya vyama vya siasa.

c) Vyama vya kisiasa vinapaswa kusikiliza na kushirikisha maoni ya AZAKI na mahitaji ya watu katika uchaguzi wao.

d) Ili kujenga uelewa bora kwa wananchi wapiga kura, Vyama vya siasa vihakikishe vinasambaza ilani zao za uchaguzi kwa wingi ili watu wasome.

e) Ni jukumu mahususi la chama cha siasa kitakachoibuka mshindi kuifanya serikali iweze kutekeleza ahadi zote zilizoandikwa kwenye ilani ya chama chao.

f) Kutokana na kushamiri kwa matukio ya ukatili wa kijinsia katika utekelezaji wa ilani ya AZAKI 2019-2024, Ni wito wetu kwa vyama vya Siasa kuzingatia usawa wa kijinsia katika michakato yao ya ndani na kupitisha majina ya wagombea katika uchaguzi wa serikali za Mitaa na Uchaguzi mkuu katika nafasi zote za kisiasa ili kuongeza chachu ya kupambania suala la usawa katika jamii.

g) Kiwango cha watu wenye ulemavu nchini kimeongezeka hadi asilimia 11.2 mwaka 2022 kutoka asilimia 9.3 ilivyokuwa mwaka 2012, Bunge limeelezwa. Vyama vya kisiasa vinapaswa kutoa fursa sawa kwa watu hawa wenye ulemavu kugombea nafasi tofauti na kuwa na uwakilishi wa kutosha sawa na ongezeko lao.

### 10.2.3 Kwa Wagombea

a) Tunatoa wito kwa wagombea kuzingatia ajenda za watu sanjari na ilani za vyama vyao na kuacha kuwabembeleza wananchi kwa ahadi tupu wanazojua hawawezi timiza.

b) Aidha, tunatoa wito kwa mgombea kuacha kuwahonga wananchi fedha na njia nyinginezo zisizofaa kwa lengo la kuwarubuni wapige kura kwa niaba yao.

c) Ni wito kwa wagombea wote kuepuka kutoa matamshi ya chuki, vitisho kwa wagombea wenzao na kusambaza habari za uongo. Wagombea lazima waheshimu sheria na kanuni za uchaguzi, na waheshimiane kwa kufuata maadili ili waweze kuepuka kuzua vurugu miongoni mwa wafuasi wa vyama vyao.

d) Wagombea lazima waheshimu uamuzi wa watu na kukubali matokeo yoyote ya uchaguzi ambayo yatatangazwa, na wakati wowote wasiporidhika, lazima wafuate hatua zilizowekwa kisheria, ikiwa ni pamoja na taratibu za kupinga matokeo, ili kuepuka hatua yoyote inayoweza kuhatarisha amani

### 10.2.4 Vyombo vya Kusimamia Uchaguzi INEC, ZEC na TAMISEMI

a) Ni wito wa AZAKI katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na uchaguzi Mkuu 2025, Tume za uchaguzi na TAMISEMI kutekeleza majukumu yao kwa uhuru na kwa mujibu wa kanuni na sheria zilizokubaliwa na vyama vya siasa na kwa vyovyote vile kujiepusha na upendeleo wowote wa chama chochote cha siasa katika hatua yoyote ya mchakato wa uchaguzi.

b) Vyombo vya Usimamizi wa Uchaguzi vihakikishe kuwa maafisa wote na wasimamizi wa uchaguzi wanamepewa mafunzo ya kina na kuwachunguza kabla ya kugawiwa vituo vyao vya kazi, hii itasaidia kushughulikia makosa yoyote ambayo huenda yalipuuzwa wakati wa usajili wa wapigakura.

c) Vyombo vya usimamizi zitafanye mipango yote muhimu mapema, kama vile kusambaza vifaa mapema ili kuepusha usumbufu wakati wa siku ya kupiga kura hivyo kupelekea baadhi ya wapiga kura kujiondoa.

d) Zihakikisha kwamba wapiga kura wote wanaostahili ambao hawajajiandikisha katika PVR kutokana na sababu mbalimbali wanandikishwa na kupiga kura zao.

e) Kuhakikisha watanzania wote halali wanahusishwa katika zoezi la uandikishwaji na upigaji wa kura bila ya ubaguzi wa kisiasa, kimazingira, kikabila, Rangi, Dini wala mipaka ya aina yoyote.

f) Ni wito wa AZAKI kwa kila eneo , jimbo la uchaguzi lisimamiwe na msimamizi huru wa uchaguzi badala ya Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya na Manispaa kama ilivyoelekezwa na mahakama.

g) Vyombo hivi vishirikiane na AZAKI pia wadau wengine katika kutoa elimu ya kiraia ya mpiga kura ili kuongeza uelewa kwa Wananchi.

h) Kuhakikisha waendesha uchaguzi kwa uwazi na kutangaza matokeo kwa mgombea aliyeshinda pekee na si vinginevyo.

i) Vituo vya kupigia kura vitangazwe mapema ili mpiga kura aweze kujua mapema na kuepuka usumbufu wa aina yoyote.

j) Zihakikishe zinashirikiana na AZAKI katika kuhakikisha watanzania wanapata elimu sahihi kuhusu uchaguzi.

### 10.2.5 Vikosi vya Majeshi na Usalama

a) Vyombo vya ulinzi na usalama vitekeleze majukumu yao kwa weledi na kwa utulivu ikiwa ni pamoja na kuepuka kuwatisha wapiga kura na wananchi kwa ujumla.

b) Ni wito wa AZAKI Vikosi vya usalama kutotumia nguvu, vitisho na silaha nzito wakati wa kampeni na siku ya kupiga kura.

c) Majeshi yasijielekeze upande wowote au vyama vya kisiasa kwa njia yoyote badala yake watende haki kwa vyama vyote vya siasa, wananchi na wagombea binafsi ikiwa ni pamoja na kukataa kuhudumia kwa maslahi ya taasisi yoyote ya kisiasa au mamlaka yoyote kinyume na sheria inayowapa mamlaka ya kutekeleza majukumu yao.

d) Tunalishauri Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Polisi Tanzania kujiepusha kujihusisha na mchakato wa uchaguzi kuanzia hatua za maandalizi ya uchaguzi, kampeni, upigaji kura halisi na hata baada ya matokeo kutangazwa.

e) Usalama wa Taifa na vikosi vya kijeshi vitumie taaluma ya hali ya juu wakati kuzuia vurugu za kisiasa wakati wa kampeni za uchaguzi.

### 10.2.6 Washirika wa Kimataifa

a) Ni wito wetu kwa Washirika wote wa kimataifa kuendelea kutoa usaidizi wa kitaalamu na kifedha kwetu na kwa serikali ili kuwezesha mchakato wa uchaguzi huru na wa haki.

b) Washirika wa kimataifa waendelee kufanya kazi kwa karibu na AZAKI ili kufikia lengo lililowekwa la kusambaza elimu ya uraia na mpiga kura kwa wananchi.

c) Waepuke kuingilia kati mambo ya ndani ya vyama vya siasa.

d) Wapunguze kutoa fedha kwa mashirika yao wenyewe wakati wa uchaguzi badala yake watoe kwa AZAKI za kitanzania zinazofanya kazi kubwa wakati wa uchaguzi.

### 10.2.7 Watumishi wa Umma

a) Watumishi wa umma wanaotamani kushika Nyadhifa mbalimbali za kisiasa wasiruhusiwe kutumia rasilimali za umma wakati wa michakato yote ya ndani ya vyama vya siasa na wakati wa uchaguzi.

b) Watatumie haki yao ya kikatiba kuchagua viongozi wanaowapenda bila kulazimishwa au kutishwa kufanya hivyo kutoka kwa chombo chochote ndani na nje ya serikali.

c) Watumishi wa umma hawatopaswa kuonyesha hadharani kupendezwa kwao na chama chochote cha kisiasa.

d) Pia hawatajihusisha na aina yoyote ya kampeni kwa mujibu wa Nyadhifa zao.

e) Waachie nafasi zao za sasa kama wanataka kushiriki michakato ya uchaguzi kama wagombea.

### 12.2.8 Vyombo vya habari

a) Vyombo vya habari na waandishi wa habari wanapaswa kuzingatia maadili yao ya kitaaluma kwa kuhakikisha kwamba wanaripoti kwa umma bila upendeleo kwa mgombea au chama chochote cha kisiasa.

b) Kuchanganua sera za vyama mbalimbali vya siasa na jinsi zinavyoendana na ustawi wa wananchi.

c) Vile vile vyombo vya utangazaji vya umma na magazeti ambayo yanafadhiliwa na walipa kodi wanapaswa kujitahidi kutoa haki kwa wagombea wote na vyama vya siasa.

d) Watumishi wa umma lazima wawe huru wakati wote wa mchakato wa uchaguzi na lazima watumie haki yao ya kikatiba ya kuwapigia kura viongozi wanaowapenda bila kushurutishwa kufanya hivyo na mtu yeyote ndani au nje ya serikali.

e) Vyombo vya habari vinapaswa kuelimisha, na kuhabarisha umma juu ya ushiriki wa watu katika yote michakato ya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu kuanzia kampeni hadi upigaji kura halisi.

f) Pia Vyombo vya Habari vina wajibu wa kuonya, kukosoa na kupinga ukiukaji wowote wa sheria za uchaguzi au vurugu katika mchakato wa uchaguzi.

g) Vyombo vya habari vihakikishe kuwa vinasambaza habari za kweli, na watu wanazipata taarifa zilizofanyiwa utafiti na uwiano kuhusu wagombea na vyama vyao.

### 10.2.9 Viongozi wa Dini

a) Viongozi wa dini wanatakiwa kuhubiri amani kwa wafuasi wao na ni lazima wajiepushe na kutoa tamko lolote la kumpendelea mgombea au chama chochote cha siasa katika maeneo yao ya ibada, kwenye majukwaa ya kisiasa au katika maeneo ya umma.

b) Hata hivyo, AZAKI tunawahitaji kuendelea kutoa ushauri au elimu ya uraia kwa wafuasi wao na Taifa kwa ujumla wake bila kuegemea itikadi yoyote ya kisiasa.

c) Viongozi wa kidini pia wanatakiwa kuonya, kukemea na kupaza sauti zao dhidi ya ukiukwaji wowote wa sheria au matukio ya unyanyasaji kupitia wafuasi wao au wasimamizi wa uchaguzi.

### 10.2.10 Msajili wa Vyama vya Siasa

a) Msajili wa Vyama vya Siasa na Ofisi yake wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi bila upendeleo au kuegemea upande wowote wa vyama vya siasa.

b) Kutoa miongozo, maelekezo na ushauri kwa vyama vyote ili vitekeleze wajibu wao nyakati za kampeni, uchaguzi, utungaji wa sera n.k.

c) Kutokubana vyama siasa wakati wa uchaguzi

Mikocheni B, Eyasi Road, P.o.box 105926,
Dar Es Salaam, Tanzania

+255 769 642208

info@thrdc.or.tz

www.thrdc.or.tz

Like us on

TANZANIA HUMAN RIGHTS DEFENDERS COALITION

Follow us on

@thrdcoalition

Follow us on

@thrdcoalition